# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## Kikao cha Tano – Tarehe 3 Februari, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwashilishwa mezani na: -

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 70

### Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kila Mkoa

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, Mikoa mingapi ina vituo vya kuwezesha wananchi kiuchumi, huduma zipi zinatolewa na wananchi wangapi wananufaika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Januari 2025, jumla ya Vituo 27 vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi vimeanzishwa katika mikoa 11 ya Shinyanga (vituo vitatu), Geita (vituo viwili), Kigoma (vituo nane), Katavi (kituo kimoja), Rukwa (kituo kimoja), Dar es Salaam (kituo kimoja), Tanga (kituo kimoja), Pwani (kituo kimoja), Morogoro (kituo kimoja), Dodoma (vituo saba) na Singida (kituo kimoja).

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma zinazotolewa katika vituo hivyo, kwanza ni mafunzo ya ujasiriamali ambapo jumla ya wananchi 70,804 waliotembelea vituo hivyo wamepatiwa mafunzo hayo. Pili, kujenga uwezo kwa wafanyabiashara/wakulima ambapo jumla ya wananchi 18,708 walijengewa uwezo kupitia vituo hivyo. Tatu, kurasimisha biashara, ambapo jumla ya biashara 19,796 zimeweza kurasimishwa. Nne, kutoa ushauri wa kitaalamu ambapo jumla ya wananchi 8,806 wamepewa huduma za ushauri wa kitaalam. Tano,

kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo wajasiriamali 6,653 wamepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 36.6. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri na ya uhakika kutoka Serikalini. Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais ameifungua nchi kwa kiwango kikubwa sana kiuchumi na kwa kuwa, vituo hivyo sasa havijaweza kufikia mikoa yote ukiwepo Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo wananchi wanasubiri kwa hamu sana kufikiwa na vituo hivyo, kwani yote yanayotolewa na vituo hivyo ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu kwa kasi. Swali la kwanza, je, ni lini Mkoa wa Kilimanjaro utafikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, yote yanayofundishwa katika vituo hivyo, yangetakiwa yawe yameshafundishwa, lakini tumechelewa. Je, Serikali iko tayari kwa mafunzo haya ya nadharia yaende pamoja na kutoa miradi midogodogo kwa akinamama, wakiwemo akinamama wa Wilaya ya Same, Mwanga, Rombo, Hai, Siha, Moshi Vijijini na Moshi Mjini ili waweze kwenda kwa kasi katika maendeleo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Shally kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya, lakini nimhakikishie, Mkoa wa Kilimanjaro uko kwenye hatua za mwisho kabisa kuelekea kupata eneo, kwa ajili ya kujenga Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mkoa umefanya jitihada za kupeleka baadhi wa Madiwani wa Manispaa ya Moshi na Halmashauri ya Moshi, pamoja na watu kutoka ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa, ili kwenda kujifunza. Wamejifunza Nyang'hwale na Kituo cha Kahama, ili waone namna ya kufanya kwa hiyo, Kilimanjaro tuko mbioni kuanzisha kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunapokea pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuendelea kuwawezesha

wananchi, lakini nimhakikishie, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi chini ya Mama Beng'i Issa, tutaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta ili kuweza kuhakikisha kwamba, wananchi hawa wanapata fursa mbalimbali na tumeendelea kufanya hivyo kwenye vituo vyote. Pia, tutaendelea kuangalia ile 4-4-2 ya wananchi wanayoipata, kuunganisha na hivi vituo, ili waweze kunufaika zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Mara nyingi tumekuwa tukishauri hii mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi iunganishwe kuliko kuwa na mifuko mingi, ili iweze kuleta tija. Sasa Serikali ina mkakati gani wa kuziunganisha pamoja na kutumia hivyo vituo ambavyo tunafikiri kuvianzisha ili kuwe na tija kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimjibu Mheshimiwa Paresso kwamba, kwenye eneo la kuunganisha mifuko; ipo mifuko ambayo tayari tumeiunganisha, lakini kuna mifuko ambayo tuliona haina tija, tumeifuta na tunaendelea kufanyia kazi eneo hili. Tunakushukuru sana kwa swali lako na tutaendelea kuboresha katika eneo hili ili tuweze kuleta tija zaidi kwa wananchi, lakini tunawahamasisha wananchi waendelee kutumia programu hizi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa, elimu ni jambo moja na mitaji ni jambo lingine. Ni kwa namna gani Serikali inaunganisha vituo hivi vya kuimarisha wananchi kiuchumi na mifuko inayotoa fedha, kwa ajili ya kuwapatia mitaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi tunaleta huduma zote, tunaleta hata watu wa benki, *BRELA*, *SIDO* na taasisi mbalimbali, ili kuendelea kuwafunza wananchi kwenye vituo hivyo namna ya kuweza kupata hizo fedha. Kwenye vituo ambavyo tayari vinafanya kazi, jambo hili lipo. Mheshimiwa Husna kwa kuwa unatoka Tanga, pale Tanga Mjini, kwa Mheshimiwa odo Ummy, kipo kituo hiki ukifika unaweza ukaona zaidi, lakini tunakushukuru kwa kuendelea kuuliza swali hili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Kamani.

Na. 71

**Uendelevu kwa Vijana Wanaonufaika na Program za Ujuzi na Stadi za Kazi**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutengeneza uendelevu kwa vijana wanaonufaika na programu mbalimbali za kukuza ujuzi na stadi za kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kuwa, kunakuwa na uendelevu kwa vijana wanaonufaika na programu mbalimbali za kukuza ujuzi na stadi za kazi ni ifuatavyo:-

(i) Kuwezesha vifaa/mtaji kwa vijana 1,621 walionufaika na mafunzo ya ufundi kupitia Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi;

(ii) Kushirikiana na Halmashauri zote nchini kupitia asilimia 10 ya fedha zinazotolewa au zinazokusanywa na Halmashauri kama pato ghafi, ili kuhakikisha wanufaika wote waliopata mafunzo ya ufundi kwa njia ya uanagenzi na urasimishaji wa ujuzi, nje ya mfumo rasmi, wanapewa kipaumbele kupata mikopo na zabuni zinazotangazwa katika Halmashauri hizo; na

(iii) Kuhakikisha mikopo inayotolewa na Mfuko wa Maendeleo wa Vijana unawawezesha vijana walionufaika na Programu ya kukuza ujuzi wanapata mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, programu hii ilianzishwa tangu mwaka 2021 na mpaka sasa ninavyozumza zaidi ya vijana 600,000 wamekwishanufaika na programu hii, lakini bado vijana hawa wanapata changamoto kubwa sana ya mitaji pale wanapomaliza kupata mafunzo hayo. Majibu ya Serikali ni mazuri, lakini nini Kauli ya Serikali katika mkakati wake wa kutengeneza *coordination* nzuri kati ya Mifuko hii ya Uwezeshaji wa Vijana ili wanapomaliza haya wapate mitaji ya moja kwa moja na kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, Taifa kwa ujumla limeshuhudia uzinduzi wa Sera mpya ya Elimu ambayo imeweka mkazo mkubwa sana katika elimu ya mafunzo kwa vitendo.

Sasa ni nini Kauli ya Serikali juu ya uendelevu wa programu hizi za mafunzo ingali kwamba, vijana watapata mafunzo hayo katika elimu ya moja kwa moja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Damas Kamani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maagizo yake mahususi, Mheshimiwa Rais, aliliona hilo na akatambua kwamba, ni kweli kuna vijana ambao wanapata mafunzo kwenye mifumo rasmi na isiyo rasmi, ambayo inaratibiwa na Serikali na fedha nyingi zinakwenda kule. Changamoto kubwa ilikuwa ni hiyo kweli, wakitoka hapo pengine hawana mitaji kama *starter capitals* za kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Samia Suluhu Hassan alianzisha mpango wa utoaji wa mikopo kila sekta, ili kuweza kukutana na vijana wengi zaidi. Kwenye Sekta ya Elimu unafahamu kwamba, tuna bodi ya mikopo ambayo inatoa zaidi ya shilingi bilioni 734. Kwenye Madini wapo ambao tunawapa vitalu na wanakopeshwa vifaa vya kuanzia kazi hiyo, kama ile Programu ya *Mining for Brighter Tomorrow*. Vilevile kwenye kilimo tuna *Building Better Tomorrow,* kwenye michezo pia, fedha zimekuwa zikitolewa, kwa ajili ya kuwasaidia waweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wale ambao wako kwenye mifumo ya kibiashara na ujasiriamali asilimia 10 ya fedha za mapato ghafi ya halmashauri zimeendelea kuwasaidia ikiwa ni sambamba na mfuko wa maendeleo ya vijana, ambapo vijana hawa tunawatambua na kuweza kuwasajili, lakini pia, kuwahudumia kwa maana ya kuwapa mikopo na kuwasaidia kwenye biashara ambazo wanazianzisha, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi napo pia, kuna programu maalum ya uchumi wa bluu. Utakumbuka Mheshimiwa Rais alikabidhi boti nyingi na kule Mwanza, Mheshimiwa

Kamani ulienda kuhakikisha vijana wanafanya kazi nzuri ya programu ya ufugaji samaki kupitia vitalu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inazidi kuangalia namna gani itaweza kuwafikia vijana kwa wingi zaidi katika haya maeneo yote, ikiwa ni pamoja na kutengeneza programu za upendeleo kwenye tenda zinazotolewa kwenye Halmashauri, asilimia 30 zimepewa kampuni za vijana ambazo pia, zinakopesheka. Kwa hiyo, maelezo ni mengi, lakini kwa sababu ya muda, itoshe kwa swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa namna gani kwamba, baada ya kupitisha Sera ya Elimu ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameipitisha na kwa kweli tumekuwa wa mfano kwa Afrika, tumekuwa wa kuigwa na nchi nyingine. Kwa sababu, Sera mpya ya Elimu inaenda kuangalia zaidi katika kuwajaza ujuzi vijana na maarifa ya kazi kuliko kuwa tegemezi. Kwa hiyo, hata anapopata…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hilo, katika mipango hii na programu ambazo zipo, Mheshimiwa Rais ameahidi na ataendelea kutoa fedha kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambapo Mheshimiwa Naibu Waziri, dada Ummy, ameeleza vizuri kwamba, programu hii itaendelea kuwakuta vijana wengi zaidi na kuweza kuwasaidia wanapotoka kwenye elimu. Kwa taarifa tu iliyopo tayari kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zaidi ya shilingi trilioni 2.7 zimetolewa kwa wananchi zaidi ya milioni 24 wa Tanzania wakiwemo wanawake, vijana na makundi mbalimbali, kwa ajili ya kuwawezesha kwenye shughuli za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba, jitihada zinazofanywa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kubwa. Yeye ninamshukuru kwa sababu, amekuwa sehemu kubwa sana ya kuweza kuhakikisha na kuhamasisha, vijana

tunawaangalia pamoja na makundi mengine wakiwemo watu wenye ulemavu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

Na. 72

**Kukarabati Barabara za Mitaa**

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kufanya ukarabati wa barabara za mitaa ili kuondoa usumbufu unaojitokeza wakati wa mvua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali iliongeza bajeti ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini kutoka shilingi bilioni 275 hadi shilingi bilioni 870.3, sawa na ongezeko la asilimia 216, ili kuiwezesha kuhudumia barabara zake. Aidha, Serikali hutenga fedha ya dharura, shilingi bilioni 21 kila mwaka, ili kukabiliana na athari za mvua. Vilevile, katika mwaka 2024/2025, Serikali ilitoa fedha ya dharura shilingi bilioni 84.36, kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye barabara zilizoathiriwa na mvua za *El-Nino*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuiongezea bajeti *TARURA* kadiri ya upatikanaji wa fedha ili ifanye ukarabati wa barabara za mitaa na kuziimarisha, ziweze kustahimili athari zinazoweza kuletwa na mvua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Serikali haioni ipo haja ya kuachana na ujenzi wa barabara za lami na kujenga barabara za zege ambazo ni imara zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zikisanifiwa vizuri, zikifanyiwa marekebisho na matengenezo kwa wakati hazina shida. Ndiyo maana Serikali kwa wakati huu inajielekeza katika kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami kwenye maeneo yaliyo mengi na kwenye yale maeneo ambayo ni korofi, hasa kwenye maeneo yenye vilima vikali, ndiyo Serikali inajielekeza kujenga barabara za zege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama pia kwa gharama. Gharama ya ujenzi wa lami inaweza ikaenda mpaka takribani shilingi bilioni moja mpaka shilingi bilioni mbili kwa kilomita moja, lakini ujenzi wa barabara za zege una gharama mara mbili zaidi. Kwa hiyo, Serikali inafahamu umuhimu mkubwa sana wa kuwa na miundombinu mizuri na imara na kwa sababu, Serikali inafanya usanifu na kujiridhisha maeneo ambayo lami inaweza ikafanya kazi vizuri, basi itaendelea kuzingatia yale maeneo ambayo ni korofi, yenye vilima vikali, ndiyo yatajengwa kwa kiwango cha zege, lakini maeneo mengine yataendelea kujengwa kwa lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, Mheshimiwa Sophia na Mheshimiwa Malecela, jiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Boma Ng'ombe – Chekimaji – Kikavuchini, lakini eneo la Nkwarungo – Longoi, halipitiki kabisa na wananchi wanapata shida kubwa sana eneo lile. Je, ni lini Serikali itajenga kile kivuko cha Nkwarungo na maeneo yale korofi ili barabara hii iweze kutumika? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada kuhakikisha inarejesha mawasiliano katika maeneo yote ambayo mawasiliano yamekatika kwa kujenga vivuko na kufanya matengenezo. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kupitia fedha za dharura kipande hiki katika kivuko cha Nkwarungo kitajengwa, ili wananchi katika eneo hili waweze kupata barabara iliyo nzuri ambayo itawawezesha kufanya shughuli zao za kiuchumi kufikia huduma za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Jimbo la Rungwe ni Jimbo lenye mvua zaidi ya miezi nane kwa mwaka, Kata ya Ikuti, Kijiji cha Kyobo hakina barabara kabisa na kukata mawasiliano ya wananchi kuja upande wa Halmashauri. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha zaidi *TARURA* ili waweze kutengenezewa barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba barabara nyingi zilipata athari kubwa kutokana na mvua za *El-Nino*. Serikali imekuwa ikifikia maeneo kadha wa kadha kwa ajili ya kurudisha mawasiliano kwa kujenga barabara na kuzirekebisha. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari Serikali imeshatumia zaidi ya jumla ya shilingi bilioni 84 kama fedha za dharura kwa ajili ya kwenda kufikia maeneo korofi kama aliyoyataja. Ninamhakikishia kwamba, Serikali itaendelea kufika katika maeneo yote ambayo yameharibiwa kutokana na mvua za *El-Nino* ili iweze kuyarekebisha na wananchi waweze kupata barabara nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malecela, Mheshimiwa Sophia, Mheshimiwa Mabula.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Kwanza ninaomba niipongeze sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutoa pesa nyingi sana kutengeneza barabara za vijijini. Ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri hivi, mimi nina tarafa mbili, Tarafa ya Gonja na Tarafa ya Mambavunda ambazo ni za milimani sana, barabara zote za Tarafa hizi mbili sasa hivi hazipitiki, wananchi wanaathirika sana kiuchumi.

Mheshimiwa Waziri, unaweza kuwaambia nini wananchi wangu ambao sasa hivi wanabaki nyumbani hawalimi wala hawasafiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inafanya uwekezaji mkubwa sana katika sekta ya barabara na hususan hizi barabara za *TARURA* ambazo ni barabara za Wilaya. Ndiyo maana bajeti ya *TARURA* katika kipindi cha Awamu ya Sita imeongezeka kutoka shilingi bilioni 275 mpaka kufikia shilingi bilioni 710. Kila mwaka fedha hizi zinatoka kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya barabara zetu za Wilaya inaboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kufika katika maeneo mengi zaidi katika mtandao huu wa barabara za Wilaya ili kuendelea kuziboresha. Ninamhakikishia Serikali itafika katika Jimbo lake kuendelea kwa sababu tayari fedha zinakuja hata kwenye Jimbo hili Serikali itaendelea kufika kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii ya barabara za Wilaya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula, Mheshimiwa Sophia.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, tarehe 30 Januari, 2024, katika mkutano wa vijana pale Mwanza, tulimwomba

Mheshimiwa Rais kilometa 12 na akatuthibitishia kwamba atatupa kilometa hizo. Moja ya barabara ni Barabara ya Pasiansi – Lumala – Kiseke ambayo inaelekea katika maeneo ya maziko ambako sasa wanashindwa kabisa kwenda kwa sababu barabara imeharibika na mvua ndiyo zinaendelea kunyesha. Je, ni lini kilometa hizo 12 zitajengwa kwa kiwango cha lami ikiwemo hii barabara ambayo ni maeneo ya huduma na wananchi wanaitegemea sana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia fedha nyingi sana kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ya barabara zetu za wilaya na ndiyo maana bajeti ya *TARURA* imeongezeka kwa kiwango kikubwa. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wakuu ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili lipo katika mikono ya Serikali, linafanyiwa kazi ili ahadi hii ya kilometa 12 iwezwe kutimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge awafahamishe wananchi wake, Serikali itafika kuhakikisha inajenga hizi kilometa 12 za lami. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ongezeko la bajeti ya *TARURA* imekuwa kubwa, lakini changamoto hapa ni fedha hizo zimekuwa haziendi. Je, ni lini mtamalizia hicho kiasi ambacho Bunge tulitenga ziende zikafanye kazi kwa wananchi ikiwemo Wilaya ya Nkasi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika,

ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Bunge lilipanga bajeti na Serikali inaendelea kutafuta fedha kuzipata na kuzileta katika maeneo tofauti tofauti nchini kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu ya barabara zetu. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Aida Khenani, Serikali ipo kazini na ndiyo maana tunaona kazi kubwa inafanyika katika sekta ya miundombinu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara zetu za Wilaya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Anastazia Wambura.

Na. 73

**Barabara Kati ya Mkangala – Kawawa – Namahyakata**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha mawasiliano ya Barabara kati ya Mkangala – Kawawa – Namahyakata katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali ilitumia shilingi milioni 57.2 kurejesha mawasiliano katika Barabara ya Mkangala – Kawawa - Namahyakata kwa kujenga mifereji yenye urefu wa mita 200 na kuweka kifusi cha changarawe kilomita 1.5 sehemu korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuiboresha barabara hii kwa kutenga fedha za matengenezo kila mwaka, ambapo katika mwaka 2024/2025 shilingi milioni 17.7 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya kilomita 11.8. Pia, Serikali inakusudia kuiwekea shilingi milioni 29 katika mpango na bajeti wa mwaka 2025/2026 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi kilomita

mbili. Lengo ni kuhakikisha barabara hii inawahudumia wananchi wa maeneo husika katika kipindi chote cha mwaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali kupitia *TARURA* kumekuwa na changamoto ya wakandarasi kutokulipwa kwa wakati na hasa zile fedha za Mfuko wa Jimbo, hili limepelekea kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya miradi. Je, ni lini Serikali itaondoa changamoto hii ya kutokuwalipa wakandarasi kwa wakati? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Anastazia Wambura kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi ambazo zinasimamiwa na *TARURA* kwa maana ya barabara za hadhi ya Wilaya. Ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha barabara hizi zinajengwa na zinakuwa katika hali nzuri ili ziweze kuwahudumia wananchi na ziweze kutumika katika kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya hivyo na tunawasiliana na kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwa wakati na zinaweza kuwalipa wakandarasi wetu ili waweze kukamilisha miradi ya ujenzi wa barabara hizi muhimu kabisa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hilo ndiyo jibu la barabara zote za Tanzania, zitajengwa. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Charles Muguta. *(Makofi)*

Na. 74

**Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana – Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule ya Sekondari ya Wasichana Jimbo la Mwibara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa iliyopokea shilingi bilioni 4.1 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sayansi za wasichana kupitia Mradi wa *SEQUIP*. Shule hii imejengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda yenye Majimbo ya Mwibara na Bunda Vijijini. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kujenga shule za sekondari za kutwa katika kila kata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kujenga shule hiyo katika Jimbo la Mwibara. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa majengo ya shule hiyo ambayo hayajakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Charles Kajege kwamba, Serikali Kuu kupitia Mradi huu wa *SEQUIP* tayari imeshaleta jumla ya shilingi bilioni 4.1 kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo yote yanayohitajika katika shule hii ya wasichana ya mkoa ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii adhimu kabisa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, kutoa msisitizo na

kumkumbusha Mkurugenzi na timu yake ya elimu wahakikishe majengo yote ya shule hii yanakamilika, kwa sababu fedha zote zimeshapelekwa kwa ajili ya majengo yote yanayohitajika kwenye shule hii, hakutakiwi kuwa na jengo hata moja ambalo halijakamilika. Kama fedha imepungua watenge fedha kupitia mapato yao ya ndani ya Halmashauri, waweze kukamilisha majengo haya kwa haraka sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa ukuta katika Shule ya Wasichana Mkoa wa Arusha, Longido Samia Girls? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zina wajibu wa msingi wa kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta hii ya Elimu. Serikali Kuu inaleta fedha kama nyongeza, kwa hiyo jukumu la msingi la kufanya uendelezaji wa miundombinu muhimu kama hii ipo katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Zaytun Swai kwamba Serikali kupitia fedha za Serikali Kuu na mapato ya ndani ya Halmashauri itakuja kujenga ukuta katika Shule hii ya Longido Girls ili kutengeneza mazingira salama kwa ajili ya wanafunzi wetu kusomea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa *Eng*. Stella Martin Manyanya.

Na. 75

**Hitaji la Gari Ofisi ya Ardhi Wilaya ya Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, lini Ofisi ya Ardhi Wilaya ya Nyasa itapatiwa gari ili kudhibiti uendelezaji holela hasa katika Mji wa Mbamba Bay?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ilipokea shilingi milioni 175 kwa ajili ya ununuzi wa magari mawili (2) aina ya *Toyota Double Cabin*. Magari hayo yalinunuliwa kupitia kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA)* na yanatumika kwa shughuli za uratibu na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kudhibiti uendelezaji holela katika Mji wa Mbamba Bay.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa iko katika hatua za matengenezo ya magari mengine manne (4) ili kuongeza ufanisi wa shughuli za usimamizi katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Ardhi katika eneo la Mbamba Bay. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**MHE. *ENG*. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ambayo nimepata. Suala la ardhi ni nyeti sana katika nchi yetu na limekuwa na vurugu mara kwa mara, pia limesababisha miji yetu kukua kiholela. Ni lini ardhi tena siyo tu kwa TAMISEMI, hata kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kama ambavyo Wizara ya Afya inashirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupata magari kama *ambulance* kwa ajili ya shughuli hizo maalum. Kwa nini Wizara ya Ardhi haijapewa gari maalum la kufanya shughuli hizo, matokeo yake inabaki kudandia dandia na wakati mwingine wanakuwa hawapati na ndiyo maana nikafikia kuuliza swali kama hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani hiyo siyo kwa Wilaya ya Nyasa tu, ni maeneo mengi. Ni lini ofisi za ardhi zitapewa magari maalum kwa ajili yao ili wafanye kazi zao za upimaji na uendelezaji wa ardhi bila usumbufu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa *Eng*. Stella Manyanya kwa namna ambavyo anafuatilia sana ustawi wa wananchi wa Jimbo la Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa sana ya kununua magari kwa sekta mbalimbali katika halmashauri zetu. Tumenunua magari ya elimu, afya, barabara na magari hayo mengine ambayo yanafanya kazi za usimamizi ni pamoja na usimamizi wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba magari ambayo yapo kwenye Halmashauri zetu yanafanya kazi za sekta zote zilizoko ndani ya halmashauri ikizingatiwa kwamba upimaji na upangani wa matumizi ya ardhi ni jukumu nyeti la halmashauri zetu. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia kwamba tutaendelea kusisitiza matumizi ya magari hayo ipasavyo. Pia, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua magari kwa ajili ya huduma hizo za ardhi.  Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mkenge.

Na. 76

**Ujenzi wa Kingo za Mto Mpiji**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kingo za Mto Mpiji zilizopanuka kutokana na mvua kubwa na kuhatarisha nyumba za wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kudhibiti madhara ya mmomonyoko na kupanuka kwa kingo za Mto Mpiji kutokana na mvua kubwa na kuhatarisha makazi ya wananchi wanaoishi kandokando ya mto huo. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na:

(a) Kutumia njia za asili za kudhibiti mmomonyoko wa kingo za mito kwa kupanda miche 5,000 aina ya michikichi, migomba, miti maji na matete katika kingo za mito eneo lenye ukubwa wa ekari 1,000 katika Kata ya Mabwepande.

(b) Kuweka utaratibu maalum wa uondoaji wa mchanga kwa kuunda vikundi 12 vya wapakia mchanga na wakandarasi 14 wa uchimbaji wa mchanga kwa utaratibu unaojulikana kama "kusafisha mto ili kuruhusu utiririshaji wa maji kwa njia ya asili".

(c) Aidha, kwa mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Wizara ya Maji imepanga kutenga shilingi millioni 552 kwa ajili ya ujenzi wa kingo za Mto Mpiji. Ujenzi huo utekelezwaji wake utaanza katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ukiachilia mbali uharibifu unaofanywa na mvua za *El-Nino*, Mto Mpiji kuna wachimbaji mchanga wanachimba kiholela na kusababisha kingo za mto huo kumomonyoka. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti watu hawa ili tusipate uharibifu huu mkubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami kwenda pale Daraja la Mpiji katika Kata ya Mapinga kuona uharibifu ambao unaendelea ili Serikali iweze kuchukua hatua? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Muharami Mkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mazingira, Sura 191, Kifungu 57(2) kimempa mamlaka Mheshimiwa Waziri kutunga kanuni ndogondogo pamoja na miongozo. Hivi tunavyozungumza tayari kuna kanuni na mwongozo wa usafishaji mito na maeneo mengine kwa ajili ya kutoa michanga na tope na mfumo au mkakati huu tayari umeweka hatua mbalimbali ambazo Serikali tumechukua ambazo zimeelezwa humo. Kwanza kufanya doria mbalimbali kupitia *taskforce* maalum ambayo imeundwa. Pia, kuzuia mali *in case* kama tunawakuta wachimbaji wa mchanga labda gari za ng'ombe au gari za kawaida. Vilevile, kupigwa faini, *in case* tukiwakuta wanachimba mchanga na kuzuia vibali kwa sababu wapo ambao tumewapa vibali kwa ajili ya kutoa michanga kwenye mito hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi tunaendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na wenzetu wa Manispaa na Halmashauri mbalimbali, Serikali za Vijiji ili wananchi wafahamu umuhimu wa uwepo wa mchanga katika maeneo hayo ili kuepuka mmomonyoko huo na kutuama kwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, tayari nimeshafanya ziara na Mheshimiwa Waziri katika Mto Tegeta na Mto Msimbazi na ninamwahidi kupitia huu Mto Mpiji kuelekea Jimboni kwake tutakuja baada ya Bunge hili kwa ajili ya kuja kuona changamoto hii na kiasi ambacho wananchi wameathirika. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Baada ya Bunge gani sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumalizika kwa Bunge hili, tutakwenda tukaone hiyo hali.

**NAIBU SPIKA:** Siyo baada ya uchaguzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana siyo baada ya uchaguzi, baada ya Bunge hili. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mbogo.

Na. 77

**Uhitaji wa Umeme Vijiji vya Jimbo la Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Kijiji cha Msamba-Masokolo, Izinga na Lyele na katika Vitongoji vya Kisenga na Lupata vilivyopo katika Kijiji cha Lyapinda – Nkasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi ina jumla ya vijiji 90 ambapo vyote vimepatiwa huduma ya umeme vikiwemo Vijiji vya

Lyele na Lyapinda. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya umeme katika Vijiji vya Msamba-Masokolo na Izinga umekamilika na kazi za kukagua miundombinu kwa ajili ya kuwasha zipo katika hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitongoji cha Lupata kilichopo katika Kijiji cha Lyapinda vile vile kitapata umeme kupitia Mradi wa Vitongoji 15 vya Mbunge utakaotekelezwa na mkandarasi aitwaye *M/S STEG International Services Limited* ambaye ameshakamilisha hatua za awali za upimaji na usanifu. Uhakiki wa Kitongoji cha Kisenga umekamilika na Kitongoji hiki kitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Vitongoji *(HEP-IIB)*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VICENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Sina swali la nyongeza kwa sababu Jimbo la Nkasi Kusini lilikuwa na vijiji 32 havina umeme na mpaka sasa hivi vimepatiwa umeme. Kwa kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Rais, Jimbo la Nkasi Kusini sina swali la nyongeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunataka Mheshimiwa Mbunge kama hivi, ukiona maendeleo yapo, unayasema ndani ya Bunge. Maendeleo yakifanywa na Serikali mje kuyasema humu ndani ili wananchi wa mikoa yote yote wasikie. Mtu wa Tabora akisema mtu wa Maswa asikie, mtu wa Maswa akisema mtu wa Shinyanga asikie, mpaka Mtwara. Mheshimiwa Shekilindi. *(Makofi)*

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kumekuwa na changamoto ya kukatikakatika kwa umeme katika Wilaya ya Lushoto. Sasa hivi ni takribani wiki moja sasa jamii haipati huduma hiyo. Je, ni lini changamoto ya kudumu itapatiwa suluhisho katika Wilaya ya Lushoto? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea

kupata umeme wa uhakika kwa ajili ya shughuli zao za kimaendeleo. Tutafuatilia kwa hii wiki moja, tuone ni nini kinatokea Lushoto; lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ni matengenezo au kama kuna hitilafu tutahakikisha zinasimamiwa kwa haraka ili kuweza kutatua changamoto hii. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Tauhida, kwa niaba Mheshimiwa Latifa.

Na. 78

**Ongezeko la Vyombo vya Habari Mtandao**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha ongezeko la vyombo vya Habari Mtandao haliathiri maadili na Utamaduni wa Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya kasi ya teknolojia, hasa kwa maudhui yanayopitia kwa watoa huduma za intaneti Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* imeendelea kuhuisha kanuni zinazosimamia maudhui mtandaoni ili ziweze kuendana na kasi ya mabadiliko na kuhakikisha maadili na utamaduni wetu unalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* imeendelea kutoa leseni za maudhui mtandaoni kwa maombi ambayo yanakidhi vigezo vilivyowekwa sambamba na kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni watengenezaji wa maudhui mtandaoni wanaokiuka sheria na kanuni za utangazaji ikiwemo uvunjifu wa maadili. Vilevile Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi na salama ya mtandao. Aidha, suala la kuzingatia maadili na utamaduni wa Taifa letu ni suala mtambuka na huanzia ngazi ya familia, shuleni na jamii yetu kwa ujumla na hivyo kila mwananchi kwa nafasi yake anapaswa kuwa mlinzi na msimamizi wa maadili na utamaduni wa Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Latifa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; uvunjifu wa maadili katika vyombo vya habari kwa kiasi kikubwa unachangiwa na waandishi wa habari ambao hawana taaluma ya kutosha. Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuweza kuwasaidia waaandishi wa habari hawa ili wasiweze kuipotosha jamii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na watengeneza maudhui wa mtandaoni ambao hawaonekani kuendana na kasi au maudhui ambayo yanaweza kuendana na mila na desturi za wananchi wa Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa maswali mawili mazuri ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Latifa Juwakali kwa niaba ya Mheshimiwa Tauhida Nyimbo. Kujibu swali la kwanza, ni kwamba kwanza miongoni mwa mambo ambayo Serikali inayafanya ni pamoja na kutekeleza matakwa ya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 Sura ya 229; ambapo pamoja na mambo mengine, inaielekeza Serikali kuunda Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeshaunda bodi hii na itakuwa ikiongozwa na mwanahabari nguli na mkongwe ndugu yetu Tido Mhando na itaanza kazi zake hivi karibuni. Tunaamini ya kwamba kuanza kwa bodi hii itakuwa ni mwarobaini wa kuwasaidia waandishi wa habari kuhusiana na kufuata sheria, kanuni, taratibu, weledi na uadilifu kwenye kazi yao. Bodi hii itaanza kazi zake hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunaliona suala la mahitaji ya kuwasaidia waandishi wa habari ili kuifanya kazi yao kwa weledi na tunalifanyia kazi kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili kuhusiana na watengeneza maudhui ya mtandaoni, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kinidhamu kwa watengeneza maudhui wa mtandaoni ambao wamekuwa wakionekana kuvunja maadili na utamaduni wa Kitanzania. Kwa bahati nzuri pia, uvunjifu wa maadili na utamaduni wa Mtanzania unabebwa pia na masuala mengine ambayo ni uvunjifu wa sheria, ni jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria nyingi katika nchi hii ambazo zinaweza kulifanyia kazi jambo hili na hivyo Serikali imekuwa ikichukua hatua za mara kwa mara ikiwemo kuwapeleka Mahakamani watengeneza maudhui hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wajibu wa Taifa lolote lile si tu kulinda mipaka ya nchi au kulinda mali, pia ni kulinda akili ya mwananchi wake, kwa maana kile anachokisikia, anachokiona na kile ambacho anajifunza. Kumekuwa na changamoto ya *media* nyingi kuajiri watu ambao hawana weledi na taaluma ya uandishi wa habari na wamekuwa wakipotosha na kuleta mtafaruku kwenye Serikali. Je Serikali ina kauli gani kwa ajili ya maslahi ya watoto wa Tanzania hii kwenye suala la kulinda maadili ya Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kujibu swali la Mheshimiwa Sanga, kama ambavyo nilijibu kwenye swali la nyongeza lililopita, ni kwamba, Serikali imekuwa ikitekeleza masuala kadhaa kuhakikisha kwamba inalinda masikio ya walaji, watu wa mwisho wanaofikiwa na habari.

Moja ya hatua ambazo tumezichukua ni pamoja na kuunda Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari ili kutekeleza matakwa ya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini baada ya kuundwa kwa bodi hii, miongoni mwa mambo yatakayofanyika ni kuhakikisha kwamba tunasimamia maadili na weledi miongoni mwa waandishi wa habari. Yale matakwa yote ya kisheria yanayotakikana kufikiwa kabla ya mwandishi wa habari kuweza kupata nafasi ya kufanya kazi kwenye chombo cha habari, sasa yataenda kutiliwa mkazo na kuhakikisha yanatekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Subira Mwaifunga.

Na. 79

**Mabadiliko ya Sheria ya Kuasili Watoto**

**MHE HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta mabadiliko ya Sheria ya Kuasili watoto kwani iliyopo imepitwa na wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya mabadiliko ya Sheria ya Mtoto kuhusu masuala ya uasili wa mtoto kwa kuboresha mifumo na kuimarisha taratibu za kuasili nchini kupitia Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya mwaka 2024. Mabadiliko hayo yamepitishwa kupitia kikao cha 16 cha Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Sera na Sheria mbalimbali kadri itakavyohitajika kwa lengo la kuimarisha ulinzi na ustawi wa mtoto, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, familia nyingi zimekumbwa na tatizo la watoto wa kike ama ndugu wa karibu kubakwa na kupata mimba ambazo hawajazitarajia hivyo kupelekea watoto hawa kukosa malezi kwa watoto ama wanawake hao ambao wako hapo. Sheria, masharti na taratibu za Ustawi wa Jamii ili uweze kusaidia malezi kwa mtoto huyo, yamekuwa ni magumu sana. Swali la kwanza; je, Serikali ina kauli gani juu ya wanawake hawa wanaobakwa na hawana uwezo wa kulea watoto hao ili waweze kutengenezewa mazingira ambayo yanaweza kusaidia kulea watoto hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tunatunga sheria ili ziweze kusaidia wananchi na siyo kukomoa wananchi, lakini Sheria za Kuasili zimekuwa ngumu kiasi kwamba watu wengi wanashindwa kuasili watoto na kupelekea watoto hao kuzidi kubaki mitaani. Je, Serikali haioni jambo hili linatakiwa lirahisishwe ili tuweze kuasili watoto hawa walioko mitaani kuliko ilivyo hivi sasa ambapo sheria zimekuwa ngumu kiasi kwamba watu wengi wanashindwa kuasili watoto kwa sababu ya utaratibu unaotakiwa kufuatwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la mwanzo linahusu wanawake ambao wamepata changamoto ya kubakwa, lakini hawawezi kuwalea watoto wao. Sheria hizo zipo; lakini naomba na wanawake hao ambao wamepata changamoto hizo, wafike katika ofisi zetu za ustawi wa Jamii katika halmashauri zote, ambako tuna maafisa hawa; ili kuhakikisha kwamba wanafuata sheria na miongozo

iliyowekwa. Sasa hivi sheria zimerekebishwa na ziko rahisi. Hii ni kwa ajili ya kumhakikishia mwanamke huyu kuweza kujiendesha mwenyewe kwa kupata mikopo ili kuweza kujiendesha kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuhusu watoto ambao wako mitaani, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iko makini na inajali sana watoto katika malezi na makuzi ambayo wamewekewa. Tuna vituo vyetu viwili vya kulelea watoto Kikombo na Kurasini, lakini pia tuna vituo binafsi vya kulelea watoto. Nawaomba tu wale wote ambao wana changamoto na watoto wao, wana changamoto za kulelewa, basi wafike katika ofisi zetu za Ustawi. Sheria na miongozo vipo; watoto hawa watapata haki zao za msingi hadi watakapofika umri wa kujiwezesha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kutokana na ombi hili kuchukua muda mrefu sana, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana na mimi ili akaongee na wananchi wenyewe wa Lunyeta, Utenge na Mtakuja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wizara ya Maliasili na Utalii naishukuru sana kwa sababu iliahidi mashine ya kuchenjua asali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Mheshimiwa…

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je ni lini Serikali…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa…

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, itatimiza ahadi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

Na. 80

**Kutenga Sehemu ya Mto Ugalla Kufunga Mizinga ya Asali**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga eneo la sehemu ya Hifadhi ya Mto Ugalla ili wananchi waweke mizinga ya asali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali kama ifuatavyo. Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282 hairuhusu matumizi ya rasilimali zilizoko ndani ya maeneo ya hifadhi za Taifa badala yake Sheria hiyo inaruhusu uhifadhi wa wanyampori, utalii wa picha na tafiti za kisayansi. Kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi za Taifa, kifungu cha 6(1), mara eneo linapotangazwa kuwa hifadhi ya Taifa, haki, madai, upendeleo wowote uliokuwepo awali kuhusiana na chochote ndani ya eneo hilo lililotangazwa kuwa hifadhi ya Taifa, hukoma mara moja dhidi ya mtu yeyote isipokuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, ufugaji wa nyuki na urinaji wa asali ndani ya eneo la hifadhi ya Taifa ni matumizi ya rasilimali ambayo Sheria ya Hifadhi za Taifa inakataza.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za ufugaji nyuki kwa wakazi wa Urambo na maeneo jirani kwa sasa zinafanyika katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Uyumbu yenye ukubwa wa kilomita za mraba 839 iliyopo Tarafa ya Usoke, Wilaya ya Urambo ambapo wananchi kupitia vikundi mbalimbali vya ufugaji nyuki wameendelea kutumia eneo hilo kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya *Mpanda Line* yenye ukubwa wa hekta 427,363.2, Msitu wa Hifadhi Ulyankulu wenye ukubwa wa hekta 239,841.4 na Msitu wa Hifadhi wa Vijiji vya Kangeme, Itebulanda na Utenge (KIU) wenye ukubwa wa ekari 860.

**NAIBU SPIKA:** Haya Mama Sitta, sasa maswali ya nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali langu namba 80 kupatiwa majibu, lakini nina maswali pia ya nyongeza. Je, Serikali haioni kwamba kulikuwa na umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi kwanza kabla hawajawakataza wananchi kuweka mizinga kwenye mapori hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba suala la utoaji wa elimu ni suala muhimu sana pale inapotokea kwamba eneo limepandishwa hadhi kutoka kwenye mapori ya akiba au kutoka kwenye ardhi zilizokuwa za vijiji kuwa hifadhi za Taifa na wakati wote Serikali imekuwa ikizingatia hilo. Naliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata uelewa mpana wa jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mwambe, kwa niaba, Mheshimiwa Simai.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, naomba swali lake namba 83 lipate majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Aaah! hili swali namba 81, Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Mwambe, watu wa Mtwara, kwa niaba. Mheshimiwa Asenga.

Na. 81

**Ujenzi wa Barabara ya Masasi – Mingoyo – Mtwara**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga upya Barabara ya Masasi, Mingoyo hadi Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi yenye urefu wa kilometa 201 unatekelezwa na Serikali kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Ili kuharakisha utekelezaji wa kazi, mradi umegawanywa katika sehemu mbili ambapo mkataba kwa sehemu ya kwanza ya kutoka Mtwara – Mingoyo (kilomita 82.27) na upanuzi wa barabara kutoka njia mbili hadi njia nne katika Mji wa Mtwara (kilomita 2.82) umesainiwa na sasa mkandarasi yupo kwenye hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi. Sehemu ya pili ya Mingoyo – Nanganga – Masasi (kilomita 108.24) ipo kwenye hatua za mwisho za manunuzi ya kumpata mkandarasi na mkataba unatarajiwa kuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Februari, 2025. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwambe, napenda kuuliza maswali mawili. Swali la kwanza; je, atakuwa tayari kutembelea barabara hiyo itakapoanza ujenzi? Ombi la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mkandarasi wa Barabara ya Ifakara – Mlimba ameshalipwa *advance payment* na sasa ni zaidi ya miezi mitatu hajaanza ujenzi. Nini majibu ya Serikali? Aahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza sikulipata vizuri, lakini swali la pili nimemwelewa. Napenda Mheshimiwa Mbunge nimsikilize vizuri kwenye swali lake la kwanza la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwambe anaomba kwamba barabara hiyo itakapoanza ujenzi, Mheshimiwa Waziri afike, je upo tayari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, hebu uliza vizuri hilo swali.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwambe anaomba, Waziri amesema kwamba barabara hiyo itaanza ujenzi wakati…

**NAIBU SPIKA:** Wewe uliza swali, ushauliza kwa niaba huna haja ya kumtaja Mheshimiwa Mwambe, uliza tu swali.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa Mwambe ni kwamba, Waziri amesema kwamba ujenzi wabarabara hiyo utaanza hivi karibuni. Anaomba na kuuliza, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari wakati ujenzi unaanza kutembelea barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi pamoja na wizara, kwa sababu ya ukubwa wa mradi huo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko tayari kwenda wakati barabara hiyo itakapoanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli kwamba Barabara ya Ifakara – Mlimba mkandarasi ameshalipwa *advance* na tunavyoongea sasa hivi, tayari ameshaanza maandalizi. Wataalam wameshakwenda na yeye sasa hivi anakusanya wafanyakazi wake na vifaa, kwa maana ya mitambo, ili barabara hiyo ianze kujengwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, minaomba kuuliza, je, ni lini vipande vya Barabara ya kuanzia Holili – Arusha

ambavyo havijapata mkandarasi na havijaanza kujengwa vitawekwa kwenye mpango na kujengwa? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara aliyoitaja, tumeshakamilisha taratibu zote na sasa tuko kwenye hatua za manunuzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shangai.

Na. 82

**Ukosefu wa Gari la Zimamoto Ngorongoro**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itanunua gari la Zimamoto Wilaya ya Ngorongoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kujibu swali toka Mheshimiwa Rais imempendeza na kunipa jukumu la kumsaidia kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba... *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kunipa jukumu la kumsaidia kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia, nikushukuru wewe, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano ambao mmendelea kunipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa shukrani hizo, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa ununuzi vifaa mbalimbali vya kuzimamoto na uokoaji pamoja na magari 150 ya kuzima moto na uokoaji. Pindi magari hayo yatakapofika nchini, yatasambazwa nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Ngorongoro. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangai.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa kumetokea matukio mengi sana ya moto Wilayani Ngorongoro bila uokozi. Ni nini mpango wa dharura wa Serikali kwa ajili uokozi majanga ya moto yanapotokea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nini mpango wa Serikali kwa ajili ya kuwapatia mafunzo ya zimamoto na uokoaji kwa Jeshi la Zimamoto na Uokozi Wilayani Ngorongoro? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matukio ya moto kujitokeza mara kwa mara ndani ya Wilaya ya Ngorongoro; nini mkakati wa dharura? Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Shangai pamoja na wananchi wa Jimbo la Ngorongoro kwamba Serikali inapotokea dharura tupo vizuri. Kwa mfano, juzi ilivyotokea wavuvi Mkoa wa Rukwa wamehitaji usaidizi tulipata helkopta ya jeshi tukafika kule na mabaharia kwa kuweza kufanya uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, itakapotokea dharura kule Wilaya ya Ngorongoro, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali tuko tayari kwa ajili ya kujibu kwa mujibu wa dharura zinavyojitokeza na katika hili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hivi sasa ninavyozungumza tayari Mheshimiwa Rais ameshatuwezesha tumenunua magari 12 ya kisasa. Hata juzi Kariakoo ilivyotokea janga la moto mliona aina ya mtambo ambao uliweza kuzima moto kwenye jengo refu, haya ni magari ya kisasa ya zimamoto ambayo tayari tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuko mbioni kununua helkopta maalum kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi tuko vizuri na ninamwagiza Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupeleka mafunzo Wilaya ya Ngorongoro kwenye kikosi cha Zimamoto ambacho kiko pale, lakini mafunzo haya nimwelekeze Kamishna Jenerali wa *Fire* mafunzo haya yawe nchi nzima na liwe ni zoezi endelevu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda Maalum ya Kipolisi ya Tarime Rorya ambayo inahudumia wilaya mbili kwa maana ya Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Rorya na ina gari la Zimamoto lenye uwezo wa *capacity* ya lita 1,000 tu, lakini halina *tank* la kuweza kuzima moto wa mafuta kama ambao umetokea kwenye moto wa ajali ya mafuta, pia, halina *fire hydrant*. Sasa kwa sababu umetamka hapa kwamba Serikali imenunua magari 150 na kwa sababu hii gari moja ya lita 1,000 inahudumia Tarime na Rorya; ni lini sasa Serikali inavyoleta hayo magari haioni kuna haja ya kupeleka magari mawili ya kisasa walau yenye hizo lita 5,000 kuendelea kwa Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Rorya ili kuweza kukabiliana na changamoto ya madhara ya moto? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Esther Matiko kuhusu changamoto

iliyoko Wilaya ya Tarime na Rorya na nimhakikishie magari 150 ni kwa ajili ya kwenda kwenye mikoa yote ambayo haijapata pamoja na wilaya. Kwa hiyo, tutaweka kipaumbele hata kwenye hizi wilaya ambazo zina changamoto hizi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, kwa niaba yake Mheshimiwa Simai.

Na. 83

**_TMA_ Kufanya Kazi na Idara ya Mazingira**

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI K.n.y. MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, lini *TMA* itafanya kazi na Idara ya Mazingira ili kusaidia Sekta nyingine kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya taarifa za hali ya hewa katika uandaaji na uchambuzi yakinifu wa miradi kwa usalama wa Mazingira *(Environmental Impact Assessment)* pamoja na kushiriki katika vikao vya kupitisha miradi hiyo chini ya usimamizi wa *NEMC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TMA* imekuwa na ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira katika masuala mbalimbali yanayohusu mazingira na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo maandalizi na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi. Vilevile, *TMA* imekuwa ikishiriki katika majadiliano ya mikutano inayohusu mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simai.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuiongezea wigo Taasisi ya *TMA* ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi ili kuweza kuwajulisha wananchi kitu gani kinachoendelea kuhusiana na mabadiliko hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; suala la utabiri wa hali ya hewa ni suala la kimazingira, na kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yanategemea zaidi mazingira. Je, Serikali haioni haja ya kuihamisha *TMA* kwenda Ofisi ya Rais inayohusika na masuala ya Muungano na Mazingira kwa ajili ya kuiongezea wigo na uratibu wa ufanisi zaidi kiutendaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama alivyoyauliza na nimshukuru pia kwa kuwa mfuatiliaji mkubwa wa masuala yanayohusu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya mambo mengi na makubwa katika eneo hili na haswa katika utekelezaji wa Ilani ya CCM 2025 Ibara ya 59(j). Katika hayo ninaomba nieleze kwa ufupi. Moja, kwa mara ya kwanza tumenunua rada nyingi na za kutosha kwenye nchi yetu ikiwa ni pamoja na Kigoma na Mbeya. Pili, tumeweza kufanya maboresho makubwa na kuhuisha rada zetu katika Dar es Salaam pamoja na Mwanza. Tatu, katika kujenga uwezo wa watumishi katika eneo hili la *TMA* hivi ninavyozungumza watumishi 96 kati ya watumishi 559 wako masomoni na katika hao watumishi 26 wako nchini China.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi tumenunua vifaa mbalimbali vya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndege zaidi ya 10 katika nchi yetu. Yote haya ni Serikali inaendelea kuyafanya ili kujengea uwezo *TMA*. Kama haitoshi wiki iliyopita habari

njema kwa Taifa letu, nataka kudhihirisha umadhubuti wa jinsi anavyosimamia diplomasia ya uchumi nchi yetu, kupitia Rais tumeweza kupata Mradi wa *SOFF*. Huu ni mradi wa *Systematic Observation Financing Facility* wa shilingi bilioni 13.9 ambao unahusisha Shirika la Hali ya Hewa Duniani, *(UNDP)* pamoja na nchi yetu wenye lengo la kuimarisha miundombinu ya uangazi na uchakataji wa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nchi 26 tu duniani ndizo zime-*qualify* na kupata fedha hii. Pamoja na hayo bado kutokana na kufanya kazi kubwa ya kuijengea uwezo *TMA* ushawishi wa *TMA* katika dunia umekuwa ni mkubwa na hivyo wataalamu wameendelea kuaminika na kuchaguliwa kwenye nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili ambalo amelizungumza kuhamishia kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira. Tunapokea ushauri wake, lakini tutazingatia taratibu za kuhamisha taasisi kutoka ofisi moja kwenda kwenye ofisi nyingine. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kassim Hassan Haji.

Na. 84

**Upatikanaji wa Huduma kwa Watu Wenye Magonjwa ya Damu**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza kasi ya upatikanaji wa huduma kwa watu wenye magonjwa ya damu kama Hemophilia na Seli Mundu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Januari 2025 jumla ya vituo 13 vimewezeshwa kutoa huduma za haemophilia kutoka vituo saba

mwaka 2021; ongezeko hili ni sawa na 49.5%. Aidha, Serikali imeongeza vituo maalum vya Sikoseli kutoka vituo nane mwaka 2021 hadi vituo 45 mwaka 2025 ambavyo vinajumuisha hospitali ya Taifa, hospitali sita za kanda, hospitali 28 za mikoa na hospitali 10 za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewajengea uwezo madaktari bingwa wa watoto 324, Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Madaktari Bobezi wa Magonjwa ya Damu 60 ambao ni sehemu muhimu katika utoaji wa huduma za sikoseli na hemophilia. Aidha, Serikali imeanzisha huduma za upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa sikoseli katika Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa ambapo hadi kufikia Januari, 2025, jumla ya wagonjwa 27 walipatiwa huduma hiyo. Wagonjwa wote hawa wamepatiwa huduma kwa ufadhili kupitia Mfuko wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassim.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa magonjwa haya ni ya urithi, je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya uchunguzi kwa mama wajawazito kama inavyofanya katika magonjwa mengine ili kujua sababu na chanzo cha magonjwa haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa ongezeko limekuwa kubwa la magonjwa haya. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza huduma ya upatikanaji wa dawa kufidia wagonjwa hawa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo linagusa sehemu kubwa ya jamii yetu. Kwanza nimwambie tu ndio maana Serikali imewajengea uwezo madaktari 324 wa akinamama na watoto. Lengo ni hili ambalo Mheshimiwa Mbunge analipendekeza hapa ili kuanzia sasa mwanzo kabisa akinamama wafuatiliwe na mtoto afuatiliwe kuanzia anapozaliwa na kugundua haraka kama

ana hilo tatizo ambalo tatizo hilo linatokana na chembechembe za urithi hivyo waanze kufuatiliwa na kuona jinsi ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuongeza upatikanaji wa dawa. Serikali haiendi tu kuongeza upatikanaji wa dawa; sasa tumekwenda kwenye hospitali zote za Taifa, hospitali zote za kanda, hospitali zote za mikoa na sasa tuko hospitali 10 za wilaya. Tunataka tufike hospitali zote za wilaya pia kuhakikisha dawa zinapatikana kwa wakati kabla hatujafufuka kwenda kwenye vituo vya afya kadri tutakavyoweza kujenga uwezo mapema.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Jesca Jonathan.

Na. 85

**Ajira kwa Wataalam wa Afya ya Akili Nchini**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Wataalam wa Afya ya Akili Nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2024 Serikali imeajiri jumla ya watumishi 56 wapya katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa changamoto za watumishi wa Afya ya Akili, Serikali imewajengea uwezo wataalam 2,980 kutoka vituo 710 vya Afya ya Akili ili kuweza kutoa huduma za Afya ya Akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano, 2020 hadi 2024, jumla ya madaktari 61 wamepatiwa fursa ya masomo ya Udaktari Bingwa wa Afya ya Akili pamoja na Ubingwa Bobezi wa Afya ya Akili. Aidha, Serikali imeongeza idadi ya vyuo vinavyofanya udahili wa Shahada ya Uzamili wa Afya ya Akili kutoka kimoja 2019 hadi viwili mwaka 2025. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ripoti ya *CAG* ilionesha pamoja na changamoto za masuala ya afya ya akili nchini bado tulikuwa hatuna mipango, mbinu, mikakati na utekelezaji wa kutoa uelewa kwa jamii kuhusiana na masuala ya afya ya akili kwa kukosekana kwa Baraza la Afya ya Akili Nchini. Swali la kwanza; mchakato wa uanzishwaji wa Baraza la Afya ya Akili Nchini umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, wapo tayari kushirikiana na wadau kufanya kampeni kwa ajili ya kujenga uelewa kwa jamii kuhusiana na masuala ya afya ya akili kuliko kutegemea siku ya kujinyonga tu duniani ambayo tunategemea kufanya mwezi Mei?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumejipanga vizuri sana kwenye eneo hili kuhakikisha kwamba alichosema *CAG* kinatekelezeka ndio maana unamwona Rais wetu amesaini na Wakuu wa Mikoa suala zima la lishe, maana yake nalo suala la lishe linaathiri pia eneo la afya ya akili na kutoa pia, kampeni kama ulivyosema. Kwa maana ya Baraza la matatizo ya Afya ya Akili nikuombe Mheshimiwa Mbunge kabla ya hiyo siku yako ambayo unafikiria mwezi Mei nitahakikisha kwamba hilo baraza litakuwa limeundwa hiyo siku mnapoenda kufanya tayari mtakuwa na Baraza la Afya ya Akili.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu swali lake la pili, kwamba tunashirikianaje pamoja ili kuhakikisha kwamba siku hiyo inafanyika na inafana na inakuwa na *impact* kwa maana ya kufikisha ujumbe na kuwa chanzo cha hamasa. Leo tukutane mimi na Mheshimiwa Mbunge saa saba na Mkurugenzi anayeshughulika na mambo ya afya ya akili pale Wizarani, tujipange kuanzia leo ili kuhakikisha hiyo siku inaenda kufana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ighondo.

Na. 86

**Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Singida**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, lini serikali itajenga Mahakama ya Wilaya katika Mji wa Ilongero – Singida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA) K. n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Ilongero upo katika Wilaya ya Singida, ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Kwa utaratibu wa kimahakama, Mahakama ya Wilaya ni moja kwenye wilaya, hivyo wananachi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida wanapaswa kuhudumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Singida ambayo ujenzi wake unaendelea sasa Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na ukuaji wa mji wa Ilongero, Mahakama ya mwanzo iliyopo sasa haikidhi mahitaji na hivyo Serikali itazingatia ujenzi wa Mahakama mpya ya mwanzo katika mji wa Ilongero kwenye Mpango ujao wa ujenzi ambao utaanza kutekelezwa 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa. Pamoja na hayo majibu naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni upi mkakati wa Serikali wa kuzikarabati Mahakama zingine za mwanzo katika Jimbo la Singida Kaskazini ambazo kimsingi Mahakama hizi

zimechakaa sana maana ni za tangu ukoloni mathalani ukitazama ile Mahakama ya mwanzo ya Merya, Ngimu, Mgori na Mtinko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ninapenda kujua ni lini Serikali itajenga kituo jumuishi cha utoaji haki katika Mkoa wa Singida? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka msukumo wa kipekee kabisa katika eneo hili la ujenzi wa miondombinu katika Mahakama. Ndiyo maana katika mwaka wa fedha huu tuliokuwa nao kuna ujenzi wa vituo jumuishi vya Mahakama tisa ambavyo vinajengwa lakini kuna Mahakama za Wilaya 18 ambazo na zenyewe zinaguswa na mradi huu wa kipekee kabisa. Pia kuna Mahakama za mwanzo 72 na utekelezaji wa miradi hii unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeona nia na madhumuni ya kimsingi kabisa ya kufanya uendelezaji wa miundombinu hii muhimu katika Mahakama na tayari imeanza kufanya hivyo na itaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, hata katika Jimbo lako la Singida Kaskazini Serikali itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuweza kujenga Mahakama za mwanzo nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kuhusiana na ujenzi wa mradi wa kituo jumuishi cha Mahakama katika Mkoa wa Singida. Ninaomba kumpa taarifa Mheshimiwa Abeid Ramadhan Ighondo kwamba, Serikali imeshaleta jumla ya shilingi bilioni 10.3 kwa ajili ya kujenga kituo hichi jumuishi cha Mahakama katika Mkoa wa Singida, ujenzi unaendelea na unatarajia kukamilika itakapofika mwezi wa 12 mwaka huu wa 2025.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ndulane.

Na. 87

**Ujenzi wa Soko la Samaki – Somanga**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Soko la Samaki katika Mji Mdogo wa Somanga - Kilwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nami ni mara yangu ya kwanza kujibu swali na kusimama mbele yako tangu Mheshimiwa Rais aliponiamini na kunikabidhi kipande hiki cha mifugo na uvuvi. Naomba kwa ruska yako nimshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu na naomba nimhakikishie nitaendelea kutumika kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali namba 87 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Duniani inaendelea na Mpango wa Ujenzi wa Soko la Samaki katika Mji Mdogo wa Somanga. Aidha, Mara baada ya mpango huu kukamilika Soko la Samaki Somanga litakamilishwa. Hata hivyo, naendelea kutoa wito kwa Halmashauri ya Kilwa kutenga sehemu ya mapato yake ya ndani yanayotokana na Sekta ya Uvuvi yaweze kutumika kwa ajili ya maendeleo ya sekta ikiwemo Ujenzi wa Masoko ya Samaki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuweza kujibu vizuri swali langu. Pili, ninashukuru Serikali kwa jitihada kubwa inazofanya katika

kuendeleza Sekta ya Uvuvi na kuwanufaisha wavuvi kiuchumi katika Wilaya ya Kilwa ikiwemo Ujenzi wa Bandari ya Kisasa ya Uvuvi katika Wilaya ya Kilwa, lakini pia utoaji wa boti kwa ajili ya wavuvi wetu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza awamu ya pili ya utoaji wa boti za wavuvi ambazo iliahidi kutekeleza katika mwaka huu wa fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza mradi ambao una manufaa makubwa ya kutoa vifaa kwa wavuvi kama vile vifaa vya kukaushia dagaa pamoja na nyavu kwa wavuvi kupitia mradi unaoitwa *TAS Farm*? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Ndulane kwa kuwa amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kupigania maslahi mapana ya wapiga kura wake wa Kilwa. Nimpongeze pia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake alipotuelekeza sisi kama Wizara kuja na mradi huu wa kugawa boti na vifaa vingine kwa ajili ya uvuvi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umeleta manufaa makubwa kwenye maeneo yote ambapo boti hizi pamoja na vifaa mbalimbali zimegawanywa kwa Watanzania. Baada ya pongezi hizi naomba kumwambia Mheshimiwa Ndulane na Wapiga Kura wake wa Kilwa kwamba mradi huu wa awamu ya pili tupo katika hatua ya mwisho tayari boti 120 zimeishakamilika kuandaliwa na mikataba imeishasainiwa kati ya Benki yetu ya Kilimo pamoja na wananchi wetu wanaokwenda kuzipokea boti hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo katika hatua za mwisho ili malipo yaweze kufanyika na boti hizi pamoja na vifaa vingine alivyouliza Mheshimiwa Mbunge kwenye swali lake la pili la nyongeza vyote

tunakwenda kuvitekeleza kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Venant Daud Protas.

Na. 88

**Kuweka Ukomo wa Bei za Mbegu za Mahindi**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka ukomo wa bei za Mbegu za Mahindi ili kuondoa upandishaji holela wa bei?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania *(TOSCI)* kwa kushirikiana na kampuni za mbegu imekuwa ikifanya mapitio ya bei na kuweka bei elekezi za mbegu za mahindi kila mwaka. Katika msimu wa mwaka 2024/2025, bei elekezi za mbegu za mahindi kwa kilo zilikuwa ni kama zifuatazo:-

(i) Shilingi 4,000 kwa kilo moja au shilingi 8,000 kwa kilo mbili kwa mbegu zinazochavushwa huria *(Open Polinated Varieties – OPV);*

(ii) Shilingi 7,150 kwa kilo moja au shilingi 14,300 kwa kilo mbili kwa mbegu za chotara zinazokomaa kwa muda mfupi;

(iii) Shilingi 8,000 kwa kilo moja au shilingi 16,000 kwa kilo mbili za mbegu chotara zinazokomaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango hivyo vya bei elekezi ya mbegu za mahindi vinaendelea kufanyiwa mapitio ya mara kwa mara kadri ya mahitaji ili kukidhi mahitaji ya wakulima. Aidha, Serikali

itaendelea kusimamia utekelezaji wa bei elekezi ya mbegu za mahindi ili kuwalinda wakulima wa zao la mahindi nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kuunda Taasisi ya Kusimamia Ukomo wa Bei. Hata hivyo, kumekuwa na Mfumuko wa Bei ya Mbegu hata kipindi wakulima wanahitaji mbegu. Mwaka huu mbegu imeuzwa mpaka shilingi 30,000, lakini Serikali nimeona hapo bei elekezi mwisho elfu 16,000 kwa mbegu yenye kilo mbili, bali leo imeuzwa kwa wananchi kilo hadi shilingi 30,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali yetu ni kuwalinda wananchi wetu na nyie mmelinda hiyo Taasisi ya *TOSCI* kulinda ukomo wa bei. Nini hatua stahiki zitachukuliwa kwa wauza mbegu walioenda kuwaibia wananchi na kuwauzia mbegu kwa shilingi 30,000? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nami nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali jema kwa ajili ya faida ya wakulima na wananchi wa Jimbo lake la Igalula. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunatambua kuna changamoto ya mbegu hapa nchini pamoja na bei kama ambavyo ameeleza hapo na ndiyo maana katika moja ya jitihada ambazo sisi Serikali tunazifanya sasa hivi ni pamoja na kuweka ruzuku katika bei ya mbegu za mahindi ambazo tumeanza kutekeleza katika msimu huu wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, tumeielekeza *TOSCI* kupitia Makampuni yote yanayozalisha mbegu pamoja na Mawakala na maduka yote yanayozalisha mbegu ili kuona kama wanafuata maelekezo ya bei elekezi. Kwa hiyo, wataendelea kufanya na moja ya hatua ambazo tumezifanya ni kuwanyang'anya leseni wale wote wanaowauzia wakulima bei zaidi ya ile bei elekezi, lakini vilevile wale wanaouza tu mbegu feki.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, niwaombe wakulima hapa nchini kuhakikisha kwamba wananunua mbegu zote zilizothibitishwa na *TOSCI,* lakini zile ambazo zipo katika maduka na Makampuni ambayo yamethibishwa na yamepata usajili kupitia *TOSCI.* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Dkt. Florence.

Na. 89

**Mdororo wa Bei ya Zao la Mhogo – Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukwamua mdororo wa bei kwa zao la muhogo – Muhambwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha soko la zao la muhogo ndani na nje ya nchi. Utekelezaji huo ni pamoja na Ujenzi wa Miundombinu ya Kukaushia Muhogo na Soko la Muhogo *(market shed)* katika Mkoa wa Kigoma ili kuongeza ubora na kuimarisha bei ya zao hilo; kuendelea kutoa elimu ya kilimo biashara cha muhogo kwa wakulima; na kuendelea kufanya utafiti wa soko la muhogo na bidhaa zake katika nchi mbalimbali ikiwemo mahitaji ya wanga kwa matumizi ya viwanda *(industrial starch)*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipatia nafasi kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; Bei ya Muhogo katika Jimbo la Muhambwe imeporomoka kutoka shilingi 800 mpaka 1,000 mpaka shilingi 300 mpaka 400 kwa kilo ya muhogo mkavu na Jimbo la Muhambwe halijapokea

miundombinu ya kukausha muhogo hata mmoja katika Jimbo. Kwa hivyo muhogo ule uko *grade C* kwa sababu wananchi wanaandaa kwa kumenya wenyewe na kuweka chini na hivyo muhogo unakuwa na mchanga. Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu hiyo aliyoisema Waziri kwamba imejengwa katika Jimbo la Muhambwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; muhogo katika Jimbo la Muhambwe unauzwa katika nchi za jirani ambao wanaununua kwa matakwa yao wenyewe pale wanapotaka na tafiti zinaonesha nchi zilizofanikiwa kuwa na bei nzuri ya muhogo zina sera ya matumizi ya muhogo ndani ya nchi kwa kutengeneza mazao mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye maswali, twende kwenye maswali.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaandaa Sera ya Matumizi ya Muhogo kwenye vyakula vingine kama muhogo na biskuti ili kuongeza matumizi ya muhogo ndani ya nchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba sasa hivi katika Mkoa wa Kigoma tunajenga Soko la Kimkoa pale Kakonko na ujenzi unaendelea. Na lengo la soko hili ni ku-*cover* Mkoa mzima wa Kigoma, tukishamaliza katika *level* ya mkoa katika soko la muhogo maana yake tutakwenda katika *level* za wilaya ambako na Mheshimiwa Mbunge na mwenyewe tutamfikia. Kwa hiyo, nimwondoe shaka jambo hilo lipo ndani ya mipango yetu sisi kama Wizara na Serikali kwa ujumla kwamba tutalitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuandaa Sera ya Muhogo, moja ya mkakati tulioufanya katika mwaka ulipoita mwezi Aprili, 2024, Wizara tuliandaa *forum* ile *Cassava Business Forum* ambayo moja ya mkakati ambayo tulikubaliana ni kuwa na Sera ya Matumizi ya Muhogo ambayo sasa hivi wataalam wapo na wanaichakata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakishamaliza kuichakata maana yake sasa tutaileta kwa ajili ya kupitishwa na ili ianze kutumika

kwa manufaa ya wakulima wote wa zao la muhogo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Moshi Vijijini wananchi wake wanategemea sana Kilimo cha Ndizi na uchumi wake unategemea zao hili, lakini hawana soko la uhakika, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa, kutafuta masoko nje ya nchi ili kuimairisha uchumi wa wananchi hawa, lakini kuiongezea Serikali pato la Taifa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Njau, ni kwamba moja ya kazi nzuri ambayo Serikali tunaifanya sasa hivi ni kujenga masoko hususan katika Mkoa wa Kilimanjaro na tumeanza pale mpakani Rombo tunajenga soko zuri na la kisasa kwa ajili ya wakulima wa ndizi. Vilevile katika moja ya mkataba ambao tulifanya na watu wa China pamoja na Brazil nafikiri na South Africa ni kwamba moja ya watu wanaohitaji ndizi kutoka Tanzania ni pamoja na sisi, kwa hiyo tumeingia makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachohitaji ni kuwa na masoko ambayo yataweza kukidhi ubora wa kuzitunza zile ndizi na kuzisafirisha na ndiyo kazi tunaiyofanya sasa hivi. Kwa hiyo, suala ya masoko nje ya nchi tayari tunayo tunachofanya sasa hivi kuimarisha miundombinu ambayo itasaidia usafirishaji wa zao hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha sasa tupo kwenye kipindi cha wageni. Nilipewa taarifa kwa wale waliolamba asali jana Tabora watakuwepo siwaoni, sasa sijui Mheshimiwa Shangazi mmewaacha au mmesahau? Haya.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 74 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo, Waziri

wa Viwanda na Biashara. Baraza la Vijana CCM, Wilaya ya Kisarawe Mkoani Pwani, karibuni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Angeline Mabula, Mdau wa Maendeleo kutoka Ilemela, Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Cecilia Paresso, mfanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mkurugenzi Chuo cha Afya St. Maximilliancolbe na mfanyabiashara kutoka Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, mpigakura wake kutoka Jimbo la Makete Mkoani Njombe, Watendaji wa Mtaa na Mtendaji Kata kutoka Miyuji Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, ndugu yake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Ally Makoa, Viongozi wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) kutoka Jimbo la Kondoa Mjini, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Zaytun Swai, Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; viongozi 54 wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana *(St. John University)* Tanzania, Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

Samahani kuna tangazo lingine, Mwenyekiti wa Bunge Bonanza Mheshimiwa Festo Sanga, anaomba kutoa taarifa kuhusu Azania Bunge Bonanza. Tamasha la Azania Bunge Bonanza lilifanyika Siku ya

Jumamosi tarehe Mosi Februari, 2025 katika Shule ya Sekondari ya John Merlin Dodoma.

Tunatoa shukrani kwa Benki ya Azania, Wadhamini Wakuu wa Bonanza hili, Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, Washiriki wengine waliotoka Wizara ya Maji, TAMISEMI, Chuo cha Mipango, *DUWASA, TRA, NSSF,* Hospitali ya Benjamini Mkapa, Viongozi wa Klabu ya Simba na Yanga, *Jogging Clubs* za Dodoma na Mashabiki wa Timu ya Simba na Yanga kutoka Dodoma na wadau wote walioshiriki Bonanza hili. *(Makofi)*

Ushindi wa jumla katika Bonanza hilo ni upande wa Mashabiki wa Simba ambao waliwashinda Yanga katika michezo mingi iliyofanyika ikiwemo Mpira wa Miguu, Mpira wa Pete, Wavu, Kuvuta Kamba. Ahsante. *(Makofi)*

Katika Mpira wa Miguu Mashabiki wa Simba walishinda goli nne na Yanga sifuri. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yote

iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa mwaka wa 2024 lengo ni kuliwezesha Bunge kuijadili na hatimaye kuamua kutokana na mapendekezo ya Kamati kwa kuzingatia ufafanuzi unaotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muundo wa Taarifa, naomba kubainisha mpangilio wa taarifa kimuundo, taarifa imegawanyika katika sehemu nne kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza, ni maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, njia na mbinu zilizotumika na orodha ya shughuli zilizotekelezwa; Sehemu ya Pili, shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji; Sehemu ya Tatu, inaonyesha maoni ya jumla na mapendekezo kwa lengo la kuiwezesha Bunge kuamua; na Sehemu ya Nne, ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza shughuli zilizohusu ufuatiliaji wa majukumu yanayotekelezwa na Wizara na inazosimamia. Msingi wa shughuli hizo unapatikana kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Kanuni za Kudumu za Bunge, njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge. Naomba kulijulisha Bunge njia zilizotumika wakati wa utekelezaji njia hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kujadili masuala ya sekta na kuibua *agenda* ya kuwekwa kwenye ratiba;

(ii) Kuwapatia Wajumbe mafunzo ili kuwawezesha kuwa katika muktadha wa majukumu yao;

(iii) Kutoa fursa kwa Mawaziri kufafanua maudhui ya taarifa zilizowasilishwa; na

(iv) Kujumuisha mambo yaliyobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa matokeo, Kamati hii inasimamia Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Usimamizi huo unajikita katika kubaini iwapo shughuli za umma chini ya Wizara hizo zinaongeza tija katika maisha ya watu na kwamba zinakidhi matarajio ya wananchi kulingana na Ilani ya Uchaguzi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji na utekelezaji wa maazimio ya Bunge katika taarifa ya mwaka 2023. Taarifa za Serikali zilizojadiliwa katika Kamati zinaonesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Mwaka 2023. Lengo la shughuli hii ni kulisaidia Bunge kufuatilia hali ilivyo na kuwa katika nafasi ya kusimamia Serikali kwa kuishauri inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maazimio ya Bunge katika Taarifa ya Mwaka 2023 kwenye Sekta ya Ujenzi; Mwenendo usioridhisha wa uwekezaji katika majengo chini ya Wakala wa Majengo *(TBA)*. Kamati imejulishwa kwamba, *TBA* imeendelea kutumia wabunifu wake wa ndani katika utekelezaji wa miradi. Pia, Serikali imehuisha Sheria ya Kuanzishwa kwa *TBA* kupitia Tangazo la Serikali Na. 595 la Agosti 23, 2023 ili kuiwezesha *TBA* kushirikiana na sekta binafsi kuendeleza miliki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malimbikizo ya madeni kutokana na baadhi ya wapangaji wa nyumba za *TBA* kushindwa kulipa pango kwa wakati. Kamati imejulishwa kwamba, jitihada zimefanyika ambapo Serikali iliziandikia barua taasisi zenye madeni jumla ya shilingi bilioni 2.268. Baada ya jitihada hizo, ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.296 sawa na 57% ya lengo. Aidha, jumla ya shilingi milioni 972 bado zinaendelea kufuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ya ulipaji wa madeni ya makandarasi na wahandisi washauri kwa wakati; hadi Desemba 2023, deni la wakandarasi lilikadiriwa kufikia shilingi bilioni 778. Taarifa ya utekelezaji wa azimio hili imefafanua kwamba, hadi tarehe 10 Januari, 2025, kiasi cha shilingi 298,900,000,000 sawa na 38%

tu, kimetolewa kwa ajili ya malipo ya madeni ya wakandarasi. Kamati inaona mwenendo wa ulipaji bado unasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ya ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya ujenzi wa barabara; Kamati imejulishwa kuwa, tathmini imefanyika ambapo Mameneja wa Mikoa *TANROADS* wameainisha maeneo yaliyojengeka sana hasa ya miji na majiji ambayo fidia yake ni kubwa na kushauri kurudisha upana wa eneo la hifadhi ya barabara kuwa meta 45 kwa maana meta 22.5 badala ya meta 60 ya awali. Taarifa ilionesha hadi Desemba, 2023 deni hili lilikadiriwa kufikia shilingi trilioni 5.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Uchukuzi; mapato yatokanayo na *wharfage* kubaki Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Kamati imejulishwa kuwa, Serikali imefanya maboresho ya Sheria ya fedha ya mwaka 2024 ambayo imeipa Mamlaka ya Bandari kukusanya tozo za *wharfage,* ambapo hapo awali ilikuwa inakusanywa na *TRA*. Aidha, Sheria hiyo ilianza utekelezaji wake mwezi Julai, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboresha mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. *TPA* imetekeleza azimio hili kwa kuunganisha mifumo yote na mifumo ya wadau kwa lengo la kubadilishana taarifa za kibiashara, ambapo kwa sasa mifumo inabadilisha taarifa kupitia Mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji Shehena Maeneo ya Forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutungwa kwa Sheria mahsusi inayohusu Uendeshaji, Usimamizi na Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege Nchini. Serikali ilitekeleza agizo hili kwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Bunge lilipitisha Muswada huo tarehe 28 Agosti, 2024 na hatimaye kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano tarehe 2 Oktoba 2024. Sheria hiyo ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kutumika mnamo tarehe 11 Oktoba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kuchelewa kuwalipa wakandarasi katika Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege; katika

kutatua changamoto hii, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliitengea jumla ya shilingi bilioni 88.84 kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)*, ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Desemba, 2024, kiasi cha Shilingi Bilioni 17.12 sawa na 19% tu, zimetolewa kwa ajili ya malipo ya wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Shirika la Posta Tanzania *(TPC)* kulipwa madeni wanayodai Taasisi za Serikali. Azimio hili limetekelezwa ipasavyo kwani *TPC* imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 4.498 kati ya shilingi bilioni 4.498 iliyokuwa inazidai, sawa na ufanisi wa 100% kutoka katika Taasisi za Serikali zilizokuwa zinadaiwa ndani ya kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kufuta deni la shilingi bilioni 26.8 ambalo Shirika la Posta Tanzania *(TPC)* linadaiwa. Kamati imejulishwa kuwa, Serikali inaendelea na taratibu za kufuta deni lisilolipika la Shirika la Posta Tanzania. Kikao baina ya Wizara na Taasisi husika kilifanyika tarehe 19 Desemba, 2024. Mpaka Desemba, 2024 deni hilo limeongezeka na kufikia shilingi bilioni 54.7. Ongezeko hili limetokana na ada ya tozo za Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha shilingi trilioni 1.687 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.141 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 546.084 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2024 ni shilingi bilioni 743.680, sawa na 44.06% ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 639.150 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 104.529 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi trilioni 2.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2.524 ni fedha za ndani, sawa na 96.54% na shilingi bilioni 90.562 ni fedha za nje, sawa na 3.46% ya bajeti ya

maendeleo. Hadi kufikia Desemba, 2024 jumla ya fedha za maendeleo zilizotolewa ni shilingi bilioni 685.151 sawa na 26.20% ya bajeti yote ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 142.019 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 116,469,000,000 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 25.550 ni fedha za nje. Hadi kufikia Desemba, 2024, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 87.990 sawa na 62% kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa shilingi bilioni 56.153 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 31.837 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Ujenzi; miundombinu inayosimamiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. *TANROADS* inakabiliwa na changamoto za kusuasua kwa utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *EPC + F* ambapo Taarifa ya Serikali ilieleza kuwa, eneo linalohusu fedha za *finance* limekuwa na changamoto kama: mtiririko mdogo wa fedha za miradi ya maendeleo; kupanda kwa gharama na utekelezaji wa miradi ya vivuko; ucheleweshaji wa kulipa madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri kwa wakati; na kuchelewa kwa tathmini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi inayosababishwa na Sheria ya Fidia. Hadi Desemba, 2023 madai ya fidia yalifikia shilingi trilioni 5.5 na upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano baina ya *TANROADS* na Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB)* kuhusu miundombinu ya barabara. Wakala unakabiliwa na changamoto kama vile upatikanaji wa fedha za kugharamia matengenezo ya barabara; na ukomo wa bajeti hauendani na uhalisia uliopo. Ukomo wa bajeti unaotolewa, hauendani na makadirio ya matumizi ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Ufundi wa Umeme *(TEMESA)*. *TEMESA* ina changamoto za kasi ndogo ya ulipaji wa miradi ya vivuko, uchache wa wakandarasi wa ndani wenye uwezo wa utekelezaji wa miradi ya vivuko na uhaba wa malighafi za ujenzi na ukarabati wa vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Uchukuzi. Shirika la Reli Tanzania na Zambia *(TAZARA)*. Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zikiwemo: kukosekana kwa mtaji wa uendeshaji wa fedha za uwekezaji; idadi ndogo ya injini tisa na mabehewa 783; changamoto ya madeni makubwa ya nyuma; wateja kupoteza imani kutokana na kuharibika mara kwa mara kwa injini na kusababisha ajali wakati wa uendeshaji; pia, changamoto za utendaji na za kisheria ambazo zinaathiri ufanisi na uendeshaji wa Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)*. Shirika linakabiliwa na changamoto kama vile: matatizo ya kiusanifu wa injini za *Airbus A220* na *A300* ambazo zimekuwa zikipata hitilafu mara kwa mara. Changamoto ya upatikanaji wa vipuri kwa sababu ya kushuka kwa uzalishaji wa vipuri hivyo duniani kutokana na athari za UVIKO; uhaba wa marubani hususan marubani viongozi na wahandisi wenye leseni ya kuruhusu ndege kuruka baada ya matengenezo kukamilika; kuchelewa kupata vibali vya kuanzisha safari kama ilivyojitokeza katika ndege ya mizigo kupata kibali cha China; safari za ratiba maalum; na uwepo wa madeni yanayotokana na mkataba wa ukodishaji ndege kati ya *ATCL* na *TGFA*. Kuna deni la nyuma la *TGFA* shilingi bilioni 429 hadi Juni, 2024 na deni la Taasisi za Serikali shilingi bilioni 64 na madeni ya wazabuni shilingi bilioni18.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. *TRC* inakabiliwa na changamoto zifuatazo: uhaba wa rasilimali fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo; uchakavu wa njia ya reli *(MGR)* na uhaba wa vitendeakazi; kuwepo kwa hati za madai zilizowasilishwa na wakandarasi; madeni ya wananchi yanayotokana na ardhi iliyotwaliwa ili kupisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha *SGR;* na wakandarasi kutokamilisha kazi kwa wakati kwenye Mradi wa *SGR* mfano, kipande cha Makutopora – Tabora na Tabora – Isaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF);* Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unakabiliwa na changamoto za kukosekana kwa miundombinu wezeshi ya ujenzi wa minara ikiwemo umeme na barabara kutokana na mvua kubwa zinazoikabili nchi

yetu; kutokupatikana fedha kwa wakati; na utekelezaji usioridhisha wa ujenzi wa minara kwa baadhi ya watoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*. Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo: uharibifu wa miundombinu ya mawasiliano; utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa bado; usalama wa mitandao na uhalifu wa mitandao; na kukosekana kwa udhibiti wa maudhui ya mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaoendeshwa chini ya Shirika la Mawasiliano *(TTCL)*. Shirika linakabiliwa na changamoto zifuatazo: ukosefu wa mtaji; sheria na kanuni zisizo rafiki kibiashara kama vile manunuzi ya umma; upungufu wa watumishi; na kasi ndogo ya kuunganisha wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati; mtazamo na maoni ya jumla. Kwa kuzingatia ufafanuzi huo Kamati ina mtazamo na maoni ya jumla kama ifuatavyo: -

(i) Suala la *LATRA* na Jeshi la Polisi kuwa na mgongano wa kimajukumu linalostahili kupatiwa ufumbuzi;

(ii) Upungufu wa Watumishi katika Wizara zote tatu unahitaji kupatiwa ufumbuzi;

(iii) Manufaa ya ujenzi na ukarabati wa barabara ni mambo yanayohitaji kutiliwa mkazo kutatua tatizo la ufinyu wa Bajeti ya *TANROADS* na *Road Fund;*

(iv) Changamoto kwenye eneo la fedha katika Miradi ya *EPC+ F* ni jambo linaloitaka Serikali kutafuta njia mbadala na ya haraka kutatua;

(v) Kutokutatua changamoto za *TBA* kuhusu upungufu wa mtaji; na tatizo la wapangaji wengi wa *TBA* kutokulipa pango ni jambo linalochangia kasi ndogo ya uwekezaji wa *TBA* kwenye majengo;

(vi) Suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao linastahili hatua madhubuti za kudhibiti; na

(vii) Suala la mzigo wa madeni kwa Shirika la Posta; na kasi ndogo ya ujenzi wa minara ya mawasiliano kwa *TTCL* kushindwa kujiendesha kibiashara yanastahili kauli madhubuti ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapendekezo ya Kamati. Sasa, ninaliomba Bunge lako Tukufu lizingatie ufafanuzi nilioutoa na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa msingi huo, ninaomba kutoa hoja katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto za utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha *TAZARA* na uendeshaji wa Shirika:-

Kwa kuwa, changamoto za utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha *TAZARA*, unachangia Shirika hilo kutokufanya majukumu yake kwa ufanisi. Pia, kukosekana kwa mtaji wa uendeshaji na fedha za uwekezaji, uwepo wa madeni, kuharibika kwa injini na ajali za mara kwa mara wakati wa uendeshaji pia kusababisha kero kwa wananchi;

Na kwa kuwa, changamoto hizo zinaathiri ufanisi katika usimamizi wa sekta ya uchukuzi na wateja kupoteza imani na zinasababisha kero katika shughuli za umma kwenye Sekta ya Uchukuzi.

Hivyo Basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ilete Bungeni maboresho ya Sheria iliyoanzisha *TAZARA* ili kuruhusu marekebisho yatakayowezesha Shirika kujiendesha kibiashara na kwa ufanisi zaidi; na

(ii) Serikali za pande zote mbili zifanye mazungumzo ya dhati na kuona namna bora ya kuiendesha reli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni yanayotokana na mkataba wa ukodishaji ndege kati ya *ATCL* na *TGFA* na uboreshaji wa utendaji wa *ATCL*.

KWA KUWA changamoto ya uwepo wa madeni ya nyuma yaliyolimbikizwa kabla ya ufufuaji wa *ATCL* yanaathiri mizania ya vitabu vya hesabu za Kampuni; kutopatikana kwa baadhi ya vipuri duniani kama vile injini za ndege; uhaba wa marubani viongozi na wahandisi; pia kutopata kibali cha kusafirisha mizigo nje ya nchi kwa wakati vinasababisha athari kubwa kwa Shirika na kurudisha nyuma jitihada za kuboresha sekta ya usafiri wa anga;

NA KWA KUWA changamoto hizo za madeni na ubovu huo zinarudisha nyuma Taifa katika azma ya kuwa na shirika kubwa la ndege lenye kutoa huduma kwa ufanisi.

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iendelee na mchakato wa kuhamisha ndege kutoka *TGFA* kwenda *ATCL* na isimamie kuboreshwa kwa sheria ya uanzishwaji wa *ATCL,* ili itambulike kama kampuni na siyo shirika la umma;

(ii) Serikali ihakikishe upatikanaji wa injini mbadala wa ndege aina ya *A220-300* na pia itafute namna bora ya kuhakikisha kwamba ndege hizo zinaleta faida kwa nchi;*(Makofi)*

(iii) Serikali ifute deni la *TGFA* la shilingi bilioni 429, isimamie Taasisi nyingine za Serikali kulipa shilingi bilioni 64 kwa *ATCL* na kulipa madeni ya wazabuni shilingi bilioni 18, ili kuondoa changamoto ya madeni ya nyuma yanayokabili shirika; na

(iv) Serikali ihakikishe inaboresha maslahi ya Marubani na Wahandisi wa *ATCL;* kuwahamasisha marubani Watanzania walioko nje ya nchi kurudi kufanya kazi katika Shirika letu na kuajiri marubani kutoka nje ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni ya wakandarasi na wazabuni pamoja na fidia kwa wananchi kwa ardhi iliyotwaliwa;

KWA KUWA kukosekana kwa fedha za kuwalipa wakandarasi na wazabuni kwa wakati; madeni ya fidia kwa wananchi yanayotokana na kutwaliwa kwa ardhi katika kupisha miradi; uchakavu wa njia ya reli *(MGR);* na uhaba wa vitendea kazi ni changamoto zinazosababisha Shirika la Reli kushindwa kutekeleza majukumu yake;

NA KWA KUWA changamoto hizo zinaweza kuathiri ufanisi na huduma muhimu ya usafiri inayotarajiwa kutolewa na wananchi;

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ilipe madeni ya Wakandarasi na Wazabuni kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosababishwa na riba;

(ii) Serikali ilipe fidia kwa wananchi. Tathmini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi zifanyike kwa haraka, pia, maeneo ambayo yanaonekana hayahitajiki kwa sasa yaachwe kwa wananchi ili yaendelezwe; na

(iii) Serikali itoe fedha kwa wakati ili ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli ya *MGR* ifanyike kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mahitaji ya fedha za kugharamia ujenzi na matengenezo ya miradi ya barabara na madaraja nchini.

KWA KUWA usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja nchini unakabiliwa na: ufinyu wa bajeti ya ujenzi na matengenezo; uvamizi wa maeneo ya barabara nchini; na upungufu wa watumishi wa kutosha kuwezesha tija iliyokusudiwa na kuanzishwa kwa *TANROADS;*

NA KWA KUWA hali hiyo inakwamisha dhamira ya kuanzishwa *TANROADS* na kutofikia malengo;

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iongeze fedha za ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja;

(ii) Serikali ilipe madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosababishwa na riba;

(iii) Serikali itekeleze miradi kwa uangalifu, uhalisia na ukomo wa bajeti uendane na makadirio ya makusanyo; na

(iv) Serikali iharakishe kufanya tathmini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi. Pia, maeneo ambayo yanaonekana hayahitajiki kwa sasa yaachwe kwa wananchi ili yaendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa wakandarasi wa ndani wenye uwezo wa utekelezaji wa miradi ya vivuko:

KWA KUWA uchache wa wakandarasi wa ndani wenye uwezo wa utekelezaji wa miradi ya vivuko; kuwepo kwa mtiririko mdogo wa fedha za miradi ya maendeleo; kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi; na malighafi za ujenzi na ukarabati wa vivuko kuagizwa nje ya nchi ni kati ya changamoto zinazosababisha *TEMESA* kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

NA KWA KUWA hali hiyo inasababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hasa miradi inapotumia muda mrefu kukamilika.

KWA HIYO, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwawezeshe wakandarasi wa ndani kwa kuwapa kazi na kuwalipa kwa wakati, ili waweze kutekeleza miradi kwa ufanisi. Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa mtiririko mzuri, ili miradi ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kasi Ndogo ya Uwekezaji Chini ya Wakala wa Majengo *(TBA)*:

KWA KUWA Wakala wa Majengo Tanzania umebainika kuwa na kasi ndogo ya uwekezaji kutokana na moja; upungufu wa mtaji wa upangaji na kutokulipa pango kwa wakati na mbili; changamoto za kimuundo na kisheria na upungufu wa watumishi.

NA KWA KUWA hali hiyo inaweza kuathiri uwezo wa *TBA* katika kutekeleza agizo la ujenzi wa nyumba 10,000, jambo linalokwamisha manufaa ya nyumba hizo na uwekezaji mwingine wa kimkakati.

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali itenge fedha za kutosha kuiwezesha *TBA* kufanikisha azma ya ujenzi wa majengo ya makazi na ofisi. Mbili, iliendelee kuweka msukumo unaoisaidia *TBA* kulipa madeni ya pango, zinazodaiwa taasisi za Serikali. Tatu; iwasilishe mapendekezo ya kuwepo kwa sheria, ili *TBA* iwe na mamlaka kamili ambayo itawezesha wakala kuwa na mamlaka ya kisheria na kimuundo, ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utapeli na Uhalifu Mwingine wa Kimtandao:

KWA KUWA suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao linapaswa kupatiwa ufumbuzi na *TCRA*.

Na Kwa kuwa, suala hili linatokana na maendeleo ya TEHAMA, linaloathiri uchumi, jamii, ustawi na maadili.

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali iimarishe udhibiti wa uhuru wa mtandao kwa kuzingatia umuhimu wa demokrasia yenye mipaka. Ihakikishe kwamba, *TCRA* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inaweka mikakati madhubuti inayohusisha kampuni za simu kukabiliana na uhalifu wa kimtandao. Tatu, ihakikishe kwamba, kampuni za simu zinawajibika ipasavyo katika kutoa nafuu za kisheria kwa waathirika wa uhalifu wa kimtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* Kujiendesha Kibiashara. Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inapaswa kujiendesha kibiashara, lakini inashindwa kutokana na moja; taratibu za ajira za watumishi wake kufungwa na taratibu za Sekta ya

Umma inayoongozwa na misingi ya kibiashara. Mbili, upungufu wa fedha, kwa ajili ya uwekezaji katika biashara ya ndani ya sekta;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa, Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inawezeshwa kifedha, ili iweze kuwa na mtaji wa kujiendesha kibiashara. Iangalie upya muundo wa kibiashara wa *TTCL*, ili shirika liwe na eneo mahsusi la uwekezaji kimiundombinu, ambalo litaifanya *TTCL* iwe na nguvu kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, iongeze uwezo wa kutekeleza ujenzi wa minara kwa wakati, kwa ufanisi, na kwa kasi ya kutosha kuunganisha wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzigo wa Madeni na Mtaji Mdogo wa Shirika la Posta Tanzania:

KWA KUWA Shirika la Posta Tanzania limebainika kuwa na mzigo mkubwa wa madeni na mtaji mdogo wa kuweza kujiendesha.

NA KWA KUWA bado changamoto hizo zinakwamisha nia ya Serikali katika kufufua mashirika na kurudisha nyuma maendeleo ya shirika katika kujiendesha kibiashara.

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali ibebe deni linalodaiwa na Shirika la Posta Tanzania la shilingi bilioni 54, ili kusafisha mizania ya shirika na kuliwezesha kukopesheka. Mbili, ihakikishe kwamba, Serikali inabuni vyanzo vipya vya mapato, ili kujiendesha kibiashara. Tatu, iongeze mtaji wa Shirika la Posta na kuhakikisha linapata kamisheni kwa kila mzigo kutoka kwa kampuni binafsi za usafirishaji mizigo inayofanana na wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kasi Ndogo ya Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano:

KWA KUWA ujenzi wa minara ya mawasiliano umebainika kuwa na kasi ndogo kutokana na mchakato mrefu wa kiutaratibu na baadhi ya wakandarasi kutokamilisha ujenzi kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

NA KWA KUWA hali hiyo inakwamisha lengo la Serikali kufikisha mawasiliano nchini kinyume na matarajio ya wananchi.

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kasi ya kutekeleza ujenzi wa minara na mawasiliano, hasa maeneo yaliyoainishwa kuwa na mahitaji maalum. Serikali isimamie kwa ukaribu baadhi ya kampuni zinazooneshwa, hususan katika utekelezaji wa minara. Ifanye mapitio na taratibu za mchakato wa zoezi la ujenzi wa minara ili kuboresha taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho; ninaamini kwa maelezo haya na ufafanuzi nilioutoa utaliwezesha Bunge kujadili inavyostahili, kutoa ushauri kwa Serikali, kuboresha shughuli na kuongeza tija katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kushukuru tena kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuwasilisha taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee kabisa, ninawashukuru Wajumbe wa kamati hii kwa kujituma, wakilenga kutoa ushauri unaofaa kwa Bunge. Kutokana na muda sitoweza kuwataja majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, ninaomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wa Ujenzi, kwa kushirikiana na Naibu Waziri, *Eng.* Msongwe Godfrey Kasekenya. Pia, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi, akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Mheshimiwa Jerry Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akishirikiana na Naibu Waziri, Maryprisca Winifred Mahundi, kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa kamati katika kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninawashukuru Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kuwezesha Mawaziri na Naibu Mawaziri kutoa ushirikiano kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge kwa niaba ya Sekretarieti ya Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha kamati kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ili hatimaye kupitisha mapendekezo yake, ili yawe Ushauri wa Bunge kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA MIUNDOMBINU KWA MWAKA 2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 136 (15**) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Mwaka 2024. Lengo ni kuliwezesha Bunge kuijadili na hatimaye kuamua kutokana na Mapendekezo ya Kamati kwa kuzingatia ufafanuzi unaotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** mjadala wa Taarifa hii utaliwezesha Bunge kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za umma katika sekta zinazosimamiwa na Kamati. Aidha, maudhui ya Taarifa hii yanaweza kulifaa Bunge katika uhakiki wa hatua zinazofikiwa na Serikali ili kukidhi matarajio ya wananchi katika Sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kubainisha mtiririko wa maudhui, naomba kubainisha mpangilio wa Taarifa. Kimuundo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne kama ifuatavyo: -

a) Sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla, ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, njia na mbinu zilizotumika na orodha ya shughuli zilizotekelezwa;

b) Sehemu ya pili inayoeleza shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Aidha, sehemu hii inabainisha mafanikio yaliyobainika na changamoto zinazojitokeza;
c)
d) Sehemu ya tatu inayoonesha maoni ya jumla na mapendekezo kwa lengo la kuliwezesha Bunge kuamua; na

e) Sehemu ya nne inayohitimisha ili Bunge liijadili na hatimaye kupitisha mapendekezo kama yalivyo au kwa kuyarekebisha kwa kadiri itakavyofaa.

## 1.3 Msingi wa Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza Shughuli zilizohusu ufuatiliaji wa majukumu yanayotekelezwa na Wizara inazozisimamia. Msingi wa shughuli hizo unapatikana kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 Ibara ya ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaitambua Serikali kuwa chombo chenye Mamlaka ya Utendaji na Bunge ni chombo chenye Mamlaka ya Kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Aidha, Ibara ya 8 (1) (b) inatambulisha lengo kuu la Serikali la kuwezesha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 96 ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa

madaraka yake. Vilevile, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. Katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimebainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za kisekta, ikiwemo Kamati hii. Majukumu hayo ni: -

a) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara inazozisimamia; na

d) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia msingi huo, Kamati imetekeleza shughuli zifuatazo:-

a) Kupata mafunzo kuhusu muundo na majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo ni kujiandaa kwa pamoja kulingana na wigo wa majukumu ya Kamati;

b) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2024. Lengo ni kufuatilia utekelezaji wa bajeti;

c) Kutembelea na Kukagua miradi ya maendeleo chini ya Wizara inazozisimamia iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Lengo ni kuoanisha na mwenendo wa jumla wa utekelezaji wa bajeti; na

d) Kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023/2024 na makadirio ya Bajeti ya mwaka 2024/2025 za Wizara inazozisimamia.

## 1.4 Njia Zilizotumika Kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, naomba kulijulisha Bunge njia zilizotumika wakati wa utekelezaji. Njia hizo ni kama ifuatavyo: -

a) Kujadili masuala ya sekta na kuibua ajenda ya kuwekwa kwenye ratiba;

b) Kuwapatia wajumbe mafunzo ili kuwawezesha kuwa katika muktadha wa majukumu yao;

c) Kutoa fursa kwa Mawaziri kufafanua maudhui ya Taarifa zilizowasilishwa;

d) Kuhoji na kujadiliana kuhusu mambo yaliyojitokeza kwenye taarifa zilizowasilishwa na pia kwenye ufafanuzi wa Serikali;

e) Kutumia matokeo ya ziara za Kamati na kuyaoanisha na mawasilisho kwenye Kamati; na

f) Kujumuisha mambo yanayobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano na mahojiano ili kuorodhesha mambo makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulihakikishia Bunge kuwa, njia hizo zimefanikisha matokeo ya kuaminika na kujenga uthabiti wa mapendekezo. Bila shaka Bunge litakapojadili Taarifa hii na kupitisha mapendekezo yaliyomo, Serikali itaboresha shughuli za umma kwenye sekta zinazosimamiwa na Kamati. Matokeo yake yatakuwa ni kufanikisha lengo la Serikali la ustawi wa watu kama lilivyofafanuliwa kwenye Katiba.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MATOKEO

### 2.1 Ufafanuzi wa Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii inasimamia Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Usimamizi huo unajikita katika kubaini iwapo shughuli za umma chini ya Wizara hizo zinaongeza tija katika maisha ya watu na kwamba, zinakidhi matarajio ya wananchi kulingana na Ilani ya uchaguzi inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, ufafanuzi wa shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

a) **Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Taarifa ya Mwaka 2023**

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hii ilihusisha hali halisi ya sekta zinazosimamiwa na Kamati. Taarifa za Serikali zilizojadiliwa katika Kamati zinaonyesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya shughuli za Kamati wa Mwaka 2023. Lengo la shughuli hii ni kulisaidia Bunge kufuatilia hali ilivyo na kuwa katika nafasi ya kusimamia Serikali kwa kushaishauri inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika**, ufuatiliaji uliofanywa na Kamati uligusa sekta ya Uchukuzi, sekta ya Ujenzi, sekta Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Taarifa za sekta hizo zilibainisha hali ya utekelezaji ambapo udadisi ulitumika wakati wa majadiliano. Matokeo ya shughuli hiyo yalidhihirisha hatua iliyofikiwa dhidi ya matarajio.

b) **Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 19 - 28 Machi, 2024, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti wa Mwaka 2023/2024 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Shughuli hiyo ilifanyika baada ya kutembelea na kukagua miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka

2023/2024 na kufanya ulinganisho na makadirio ya matumizi katika sekta zinazohusika. Maoni ya Kamati yalitolewa wakati wa mkutano wa bajeti Mwezi Aprili hadi Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa bajeti za sekta hizo kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 zinaendelea kutekelezwa, basi, Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji huo na Matokeo ya ufuatiliaji yataripotiwa utakapofika wakati kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge. Kwa sasa Kamati inasisitiza kuwa Serikali iendelee kutekeleza bajeti kama ilvyokasimiwa na kupitishwa na Bunge.

c) **Kushughulikia Taarifa za Utendaji na Kufuatilia Utekelezaji wa Mipango ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia umuhimu wa Taarifa za utendaji, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za sekta inazozisimamia. Taarifa hizo zilihusu shughuli za umma katika sekta ya Uchukuzi, sekta ya Ujenzi na sekta ya Mawasiliano. Uchambuzi wa taarifa hizo uliiwezesha Kamati kupata picha halisi ya hali ya sekta na uendeshaji wa taasisi za umma kwenye sekta hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ulihusisha mambo yafuatayo: -

(i) Kubaini mambo yanayougusa umma ambayo yanafaa kupata ufafanuzi wa Serikali na kuyaweka kwenye ajenda;

(ii) Kuiomba Serikali iwasilishe Taarifa maalumu ya ufafanuzi kuhusu mambo yaliyobainishwa na Kamati; na

(iii) Kurejea Ilani ya CCM ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Sera zinazoongoza sekta hizo na miongozo mingine ya utekelezaji wa shughuli za umma. Lengo lilikuwa ni kulionesha Bunge msingi wa mapendekezo ya Kamati kwa kila sekta.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kufanya hivyo, Kamati italisaidia Bunge kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kushauri Serikali ipasavyo. Bila shaka mapendekezo kutokana na shughuli hizo yatakuwa nyenzo muhimu kwa Bunge kutekeleza madaraka yake katika sekta ya Uchukuzi, Ujenzi pamoja na sekta ya habari na mawasiliano

## 2.2 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Taarifa ya Mwaka 2023

### 2.2.1 Sekta ya Ujenzi

a) **Mwenendo Usioridhisha wa Uwekezaji katika Majengo chini ya Wakala wa majengo (TBA)**

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulia changamoto hii, Kamati imejulishwa kwamba, TBA imeendelea kutumia wabunifu wake wa ndani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Umma Masaki, Temeke Kota, Magomeni Kota jijini Dar es Salaam na Ghana Kota jijini Mwanza. Katika hatua nyingine, Serikali imehuisha Sheria ya kuanzishwa kwa TBA kupitia Tangazo la Serikali Na. 595 la Agosti 25, 2023 ili kuiwezesha TBA kushirikiana na sekta binafsi kuendeleza miliki nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hayo, TBA imeainisha maeneo yake yaliyoiva kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na inatarajia kuyatangaza maeneo hayo ili kupata wabia watakaoshirikiana nayo kwa ajili ya kuyaendeleza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa jitihada hizo, ambazo zinakidhi maelekezo ya Bunge lako kuitaka TBA kuongeza kasi ya mwenendo wa uwekezaji katika majengo nchini

b) **Malimbikizo ya Madeni Kutokana na Baadhi ya Wapangaji wa Nyumba za TBA Kushindwa kulipa pango kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kwamba, jitihada zimefanyika ambapo Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi iliziandikia barua Taasisi zinazodaiwa na TBA, ili kukumbushia ulipaji wa pango zinazodaiwa Taasisi za Serikali na Sekta binafsi. Madeni hayo yalikuwa na jumla ya **Shilingi 2,268,554,983.82**. Baada ya jitihada hizo TBA kwa kushirikiana na Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,296,135,202.61** sawa na **asilimia 57** ya lengo. Aidha, jumla ya **Shilingi 972,419,781.21** bado zinaendelea kufuatiliwa. **Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza kuwa, Serikali iendelee kufuatilia ulipaji wa madeni hayo ili shirika liweze kujiendesha kibiashara.

c) **Kuhusu changamoto ya ulipaji wa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri kwa wakati**

**Mheshimiwa Spika**, hadi Disemba 2023, deni la Wakandarasi lilikuwa ni **shilingi bilioni 778**. Taarifa ya utekelezaji wa azimio hili imefafanua kwamba, hadi tarehe 10 Januari, 2025 kiasi cha **Shilingi 298,900,295,651.40** sawa na **asilimia 38** tu kimetolewa kwa ajili ya malipo ya madeni ya Wakandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kwamba, kasi ya ulipaji madeni ya Wakandarasi bado ni ndogo ukilinganisha na uhalisia wa madai, hali hii inaathiri utekelezji wa miradi. Hivyo basi, juhudi zaidi zinahitajika katika kulipa deni hilo.

d) **Changamoto ya Ulipaji wa Fidia kwa Wananchi wanaopisha Miradi ya Ujenzi wa Bararbara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa, tathimini imefanyika ambapo Mameneja wa Mikoa TANROADS wameainisha maeneo yaliyojengeka sana hasa ya Miji na Majiji ambayo fidia yake ni kubwa, na kushauri kurudisha upana wa eneo la Hifadhi ya Barabara kuwa mita Arobaini na Tano (45) badala ya mita 60 ya awali. na iwepo kwa

bypass ili kukwepa maeneo hayo. Taarifa ilionyesha hadi Disemba 2023 deni hili lilikadiriwa kufikia **Shilingi 5,588,658,067,710.69**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa, Serikali iangalie mchakato mzuri wa kuendesha zoezi hilo bila kuwaathiri wananchi wa maeneo hayo, pia kwa maeneo yasiyohitajika yaachwe kwa wananchi ili waweze kuyaendeleza.

### 2.2.2 Sekta ya Uchukuzi

#### a) Mapato Yatokanayo na *Wharfage* Kubaki Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa azimio hili, Kamati imejulishwa kuwa, Serikali imefanya maboresho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 ambayo imeipa Mamlaka ya Bandari kukusanya tozo za Wharfage, ambapo hapo awali ilikuwa inakusanywa na TRA. Aidha, Sheria hiyo ilianza utekelezaji wake mwezi Julai, 2024 na imeendelea kukusanya tozo hizo ambazo zinachangia uboreshaji wa miundombinu katika Bandari zote nchini. Kwa wastani TPA inakusanya jumla ya shilingi bilioni **60** kwa mwezi kutokana na makusanyo ya *wharfage*.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali na inaisisitiza kuendelea kutoa fedha kwa ukamilifu, na kuhakikisha kwamba TPA inatumia ipasavyo fedha hizo katika kuboresha miundombinu ya bandari nchini.

#### b) Kuboresha Mifumo ya TEHAMA katika Uendeshaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

**Mheshimiwa Spika**, TPA imetekeleza azimio hili kwa kuunganisha mifumo yake na mifumo ya wadau kwa lengo la kubadilishana taarifa za kibiashara, ambapo kwa sasa mifumo inabadilisha taarifa kupitia mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji Shehena Maeneo ya Forodha yaani "*Tanzania electronic Single Window System - TeSWS*".

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati ilitaarifiwa kwamba, taarifa za ujio wa meli na shehena iliyobebwa kwenye meli husika *(Manifest)*

zinapatikana kupitia mfumo huu. Vilevile, TPA imeunganisha mfumo wake na mfumo wa Forodha (TANCIS) ili kupokea taarifa mbalimbali kutoka kwa wadau kwa ajili ya uondoshaji shehena bandarini na kupata taarifa sahihi.

**c) Kuhusu Kutungwa kwa Sheria Mahsusi inayohusu Uendeshaji, Usimamizi na Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitekeleza agizo hili kwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Bunge lilipitisha Muswada huo tarehe 28 Agosti 2024 na hatimaye kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano tarehe 02 Oktoba 2024. Sheria hiyo ilitangazwa kwenye gazeti la Serikali na kuanza kutumika mnamo tarehe 11 Oktoba 2024.

**d) Serikali Kuchelewa Kuwalipa Wakandarasi Katika Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, katika utatua changamoto hii, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ilitengea jumla ya **shilingi bilioni 88.84** kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Desemba 2024, kiasi cha **shilingi bilioni 17.12** sawa na **asilimia 19** tu zimetolewa kwa ajili ya malipo ya wakandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa agizo hili na inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati ili miradi iweze kuanza na kukamilika kwa wakati.

### 2.2.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

a) **Shirika la Posta Tanzania (TPC) Kulipwa Madeni Wanayodai Taasisi za Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kupitia taarifa walizojadili kuwa, azimio hili limetekelezwa ipasavyo kwani TPC imefanikiwa kukusanya Shilingi **4,498,934,931** kati ya Shilingi **4,498,934,931** sawa na

ufanisi wa asilimia **100** kutoka katika taasisi za Serikali zilizokuwa zinadaiwa ndani ya kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa ufuatiliaji na kuwezesha ulipaji wa deni hilo.

b) **Serikali Kufuta Deni la Shilingi Bilioni 26.8 Ambalo Shirika la Posta Tanzania (TPC) Linadaiwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa azimio hili, Kamati imejulishwa kuwa, Shirika linaendelea na taratibu za kufuta deni lisilolipika la Shirika la Posta Tanzania. Kikao baina ya Serikali na Taasisi husika kilifanyika tarehe 19 Desemba, 2024. Mpaka Disemba 2024 deni hilo limeongezeka na kufikia shilingi bilioni **54.7.** Ongezeko hili limetokana na ada na tozo za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa, kasi ya kutatua changamoto hiyo ni ndogo hivyo basi, mikakati inahitajika ili kukabiliana na deni hilo.

### 2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

#### 2.3.1 Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi **1,687,888,714,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,141,803,989,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **546,084,725,000.00** ni fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha Shilingi **599,756,467,800.00** za Mfuko wa Barabara na Shilingi **542,047,521,200.00** ni fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2024 ni Shilingi **743, 680, 055 081.841** sawa na asilimia **44.06** ya Lengo. Kati ya Fedha hizo Shilingi **639,150,729,669.281** ni fedha za ndani zinazojumuisha Shilingi **309,982,814,471.83** za Mfuko wa Barabara na Shilingi **329,167,915,197.451** ni fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali *(Consolidated Fund)*; na Shilingi **104,529,325,412.56** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha hizo ni pungufu ukilinganisha na fedha zilizopokelewa Mwaka wa fedha 2023/24 katika kipindi kama hiki ambapo asilimia **64** zilikuwa zimepokelewa.

**Mheshimiwa Spika,** hali hiyo hairidhishi katika utekelezaji kwa kuwa kipindi cha utekelezaji kilichobaki haina uhakika kama asilimia iliyobaki inaweza kutumika kukamilisha upatikanaji wa fedha iliyosalia.

### 2.3.2 Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi **2,614,931,941,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **2,524,369,202,000** ni fedha za ndani, sawa na asilimia **96.54** na Shilingi **90,562,739,000** ni fedha za nje, sawa na asilimia **3.46** ya bajeti ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Desemba, 2024 jumla ya Fedha za Maendeleo zilizotolewa ni Shilingi **685,151,667,276.53** sawa na asilimia **26.20** ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, Shilingi **676,067,567,351.32** ni fedha za ndani sawa na asilimia **26.78** ya fedha za ndani zilizotolewa na Shilingi **9,084,099,925.21** ni fedha za nje sawa na asilimia **10.03** ya fedha za nje zilizotolewa. Taarifa imeeleza kuwa, Fedha zilizopokelewa zililipwa kulingana na kuwasilishwa kwa hati za madai.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizopokelewa ni kidogo ukilinganisha fedha zilizopokelewa katika kipindi kama hiki katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambapo, asilimia **73** zilikuwa zimepokelewa. Hali hiyo haionyeshi matumaini makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwa kuwa, kipindi kilichobaki hakuna uhakika kama kinaweza kukamilisha upatikanaji wa fedha iliyosalia.

### 2.3.3 Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi **142,019,894,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo

Shilingi **116,469,894,000** ni fedha za ndani na Shilingi **25,550,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba, 2024, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi **87,990,650,996.17** sawa na asilimia **62** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa Shilingi **56,153,235,096.17** ni fedha za ndani na Shilingi **31,837,415,900.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa fedha zilizopokelewa unaridhisha ukilinganisha na kipindi kama hiki kwa Mwaka wa fedha uliopita ambapo asilimia **56** ya fedha zilizotengwa zilikuwa zimepokelewa. Kamati inaona hali hii inaweza ikaleta matokeo chanya katika utekelezaji wa miradi.

### 2.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji

#### 2.4.1 Sekta ya Ujenzi

##### a) Miundombinu Inayosimamiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi kufikia Desemba, 2024 jumla ya kilometa 100.54 sawa na asilimia **44.37** ya mpango wa nusu Mwaka zimejengwa kwa kiwango cha lami ambazo ni sawa na asilimia **26.11** ya mpango wa Mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza) lenye urefu wa km 3.2 na ujenzi wa barabara unganishi kwa kiwango cha lami (km 1.66) lenye gharama za mradi Shilingi Bilioni **592.6**. Utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia **94.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo kwa mafanikio ambayo baadhi yameainishwa hapo juu, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i) Kumekuwa na kusuasua kwa utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa EPC + F ambapo Taarifa ya Serikali ilieleza kuwa, eneo linalohusu fedha (F) limekuwa na changamoto ambapo Serikali inaendelea na uchambuzi wa mapendekezo ya *financiers* yaliyowasilishwa na mkandarasi ili kupata gharama nafuu za miradi hiyo.

ii) Mtiririko mdogo wa fedha za miradi ya maendeleo ambapo, kasi ya ulipaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni ndogo ikilinganishwa na hati za madai zinazozalishwa na wakandarasi wanaotekeleza miradi;

iii) Kupanda kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya vivuko Malighafi za ujenzi na ukarabati wa vivuko zinaagizwa nje ya nchi ambapo malipo yake hufanyika kwa fedha za kigeni. Hali hii inasababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hasa miradi inapotumia muda mrefu kukamilika;

iv) Kupungua kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo;

v) Ucheleweshaji wa kulipa madeni ya Wakandarasi na Waandisi Washauri kwa wakati kwenye miradi, na kusababisha kuongezeka kwa gharama;

vi) Kuchelewa kwa tathimini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi inayosababishwa na Sheria ya Fidia. Kwani imebainika kuwa, hadi Disemba 2023, fidia inayohitajika kwenye maeneo yote nchini kwa barabara za kuu na za mikoa inakadiriwa kufikia **Shilingi 5,588,658,067,710.69**; na

vii) Upungufu wa Watumishi.

### b) Ushirikiano Baina ya TANROADS na Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) Kuhusu Miundombinu ya Barabara

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa zilizowasilishwa, Kamati ilibaini kwamba TANROADS kwa kushirikiana na RFB imeainisha maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile maeneo yanayofaa kwa

biashara pamoja na michoro inayoonyesha maeneo ya maegesho ya magari madogo, malori, bajaji na pikipiki, maeneo ya kupumzika, huduma ya vyoo vya umma na Mabango ya kisasa. Vilevile, Pamoja na kutekeleza ujenzi wa barabara za mwendo kasi (BRT) TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam imeanza pia kutekeleza miradi ya kupendezesha Jiji kama vile kupanda miti, maua, uwekaji wa mabango ya kisasa na uwekaji wa mabango ya kisasa kwenye mipaka (Kiluvya, Airport & Bunju B).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu, mashirikiano baina ya taasisi hizo mbili, Wakala unakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa fedha za kugharamia matengenezo ya barabara ambapo yamekuwa yanaongezeka na ukomo wa bajeti hauendani na uhalisia uliopo. Pia ukomo wa bajeti unaotolewa hauendani na makadirio ya matumizi ya mafuta ambayo ndiyo msingi mkubwa wa kukadiria mapato ya Mfuko.

**Mheshimiwa Spika**, inakadiriwa kwamba matengenezo ya barabara nchi nzima yanahitaji takribani shilingi trilioni **2,** ili ziweze kutengamaa, lakini fedha za matengenezo zilizopokelewa hadi Disemba 2024 ni shilingi **522,712,735,425** kwa matengenezo. Aidha, Barabara nyingi zinahitaji kufanyiwa matengenezo maalum *(periodic maintenance)* au ukarabati mkubwa. Hata hivyo, matengenezo na ukarabati huo haufanyiki kikamilifu kutokana na uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara.

### c) Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)

**Mheshimiwa Spika,** Wakala umepata mafanikio mbalimbali katika katika kutekeleza majukumu yanayohusiana na vivuko: -

i) Wakala umekamilisha ukarabati mkubwa wa vivuko 13;

ii) Jumla ya Watumishi 45 wa Vivuko wamepatiwa mafunzo katika Chuo cha DMI. Aidha, Wakala unatarajia kuwapeleka Jumla ya Watumishi 42 wakiwemo Wahandisi, Manahodha, Mabaharia na Mafundi wa Vivuko kwenye mafunzo ya muda mfupi katika chuo cha DMI; na

iii) Wizara kupitia TEMESA ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba wa Joint Venture na kampuni ya Azam Marine ili kuwezesha utoaji wa huduma katika kivuko cha Kigamboni.

**Mheshimiwa Spika** Changamoto za TEMESA ni kama zifuatazo: -

i) Kasi ya ulipaji wa miradi ya maendeleo ni ndogo ikilinganishwa na hati za madai zinazozalishwa na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maendeleo ya ujenzi wa vivuko vipya na ukarabati mkubwa wa vivuko;

i) Uchache wa wakandarasi wa ndani wenye uwezo wa utekelezaji wa miradi ya vivuko; na

ii) Malighafi za ujenzi na ukarabati wa vivuko zinaagizwa nje ya nchi ambapo malipo yake hufanyika kwa fedha za kigeni. Hali hii inasababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hasa miradi inapotumia muda mrefu kukamilika.

### 2.4.2 Sekta ya Uchukuzi

#### a) Shirika la Rela la Tanzania na Zambia (TAZARA)

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 11 Novemba, 2024 ilipokea taarifa ya utendaji wa TAZARA. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kwamba uendeshaji bora wa TAZARA unaweza kuwa na mchango mkubwa sana katika maendeleo ya uchumi kwa nchi za Ukanda wa Kusini Mashariki zinazopakana na Tanzania. Mathalani, inatarajiwa kwamba, ifikapo mwaka 2030, uzalishaji wa madini ya shaba katika nchi ya Zambia unatarajiwa kuongezeka hadi tani milioni 3 na kwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kufikia tani milioni 7.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba TAZARA ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu, na nchi za jirani, Kamati ilibaini kwamba uendeshaji wa Shirika hilo umeendelea kuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: -

i) Kukosekana kwa mtaji wa uendeshaji na fedha za uwekezaji kumesababisha kutofanyika kwa matengenezo muhimu;

ii) Idadi ndogo ya injini na (injini 9, mabehewa 783). Mahitaji ni injini 26 na mabehewa 1000 ili kufikia kiwango cha kutopata hasara Idadi ndogo na ya kuaminika ya mabehewa ya abiria;

iii) Changamoto ya madeni makubwa ya nyuma, **USD165 (181.2)** millioni yakiwemo madeni ya kisheria *(statutory debts)* na watoa huduma *(supplier debts)*;

iv) Wateja kupoteza imani kutokana na kuharibika mara kwa mara kwa injini na kusababisha ajali wakati wa uendeshaji;

v) Kuwepo kwa changamoto za utendaji na za kisheria ambazo zinaathiri ufanisi wa uendeshaji wa Shirika la Reli ya TAZARA.

**b) Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)**

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa iliyowasilishwa kuhusu utendajii wa Shirika la Ndege, Kamati ilitaarifiwa kwamba mtandao wa safari za ndege umepanuka kutoka vituo 4 mwaka 2016 hadi vituo 28 kufikia Novemba, 2024. Vituo vinavyofanya kazi ni 25 kati ya hivyo13 ni vya ndani ya nchi, 9 ni kikanda na 3 ni kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, ATCL imefaulu ukaguzi wa usalama katika uendeshaji wa shughuli za usafiri wa anga mara nne (4) mfululizo na kutunukiwa cheti kiitwacho "*IOSA Certificate*". Pia, ATCL imekidhi taratibu za ubora na usalama katika nchi kumi inazofanya safari ikiwa ni pamoja na Uingereza inapotarajia kuanza safari, ambapo tayari ATCL imepewa kibali.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Shirika limeendelea kufanya mashirikiano na mashirika mengine ya ndege kama Air India, APG Airline, Emirate Airlines, Ethiopian Airline, Hahn Air, Oman Air, Precision Air, Qatar

Airways, Rwanda Air, Egypt Air, Proflight Zambia, LAM - Mozambique Airlines, na Fly Dubai. Vilevile, ATCL iko katika hatua mbalimbali za kuingia makubaliano ya ushirikiano na KLM Royal Dutch Airlines, Turkish Airlines, Uganda Airlines, na Saudi Arabia Airline.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mapato ya Shirika, Kamati ilitaarifiwa kwamba mapato ya fedha za kigeni yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 79.22 Mwaka 2022/23 hadi Dola za Marekani milioni 83.93 Mwaka 2023/24. Aidha, kodi, Ada na Tozo za Kisheria umeongezeka kutoka shilingi bilioni 28.6 Mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 50.3 kwa Mwaka wa fedha 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 76. Jumla ya mapato hayo katika kipindi cha miaka mitatu 2021/22 – 2023/24 ni shilingi bilioni 156.5.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ya ATCL yaliyoainishwa hapo juu, Shirika limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na: -

i) Matatizo ya kiusanifu wa injini za Airbus A220 – 300 ambazo zimekuwa zikipata hitilafu mara kwa mara na kuathiri shughuli za kampuni za kila siku na kusababisha kukosa mapato wastani wa **TZS bilioni 127.3** kwa mwaka;

ii) Changamoto ya upatikanaji wa vipuri kwa sababu ya kushuka kwa uzalishaji wa vipuri hivyo duniani kutokana na athari za UVIKO-19;

iii) ATCL inakabiliwa na uhaba wa marubani hususan marubani viongozi (captains), na wahandisi wenye leseni ya kuruhusu ndege kuruka baada ya matengenezo kukamilika *(certifying engineers)*;

iv) Kuchelewa kupata vibali vya kuanzisha safari kama ilivyojitokeza katika ndege ya mizigo kupata kibali cha China kwa safari za ratiba maalum; na

v) Uwepo wa madeni yanayotokana na mkataba wa ukodishaji ndege kati ya ATCL na TGFA. kuna deni ya

nyuma la TGFA **Sh bil 429** hadi Juni, 2024 na deni la taasisi za Serikali **Sh. bil 64** na madeni ya wazabuni **Sh bil 18.**

### c) Shirika la Reli Tanzania (TRC)

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa zilizowasilishwa kuhusu TRC, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Shirika limeanza uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo huduma zilianza tarehe 14 Juni, 2024 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na tarehe 25 Julai kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma. Aidha, TRC imeendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa vipande vilivyobaki vya Makutupora – Tabora (Km 368), Tabora – Isaka (Km 165), Isaka – Mwanza (Km 341) na Tabora – Kigoma (Km 506). Vilevile, TRC imeanza mchakato wa ununuzi na kupata Mkandarasi na Msimamizi wa mradi kwa kipande cha Uvinza – Musongati – Gitega (Km 282).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, TRC inaendelea na ukarabati wa njia ya reli ya Kati iliyopo kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Isaka umbali wa kilometa 970 kwa kuongeza uwezo wa madaraja kutoka uwezo wa ekseli 13.5 hadi 18.5.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa hatua ambazo imefikia katika kuboresha miundombinu ya reli inayosimamiwa na Shirika la Reli Tanzania. Hata hivyo, pamoja na mafanikio ambayo yameainishwa hapo juu, Kamati imebaini kwamba TRC inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i) Uhaba wa rasilimali fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo katika kuwezesha utekelezaji wa miradi;

ii) Uchakavu wa njia ya reli (MGR) na uhaba wa vitendea kazi;

iii) Kuwepo kwa hati za madai zilizowasilishwa na wakandarasi ambalo hadi kufikia Agosti, 2024 ni Dola za Marekani (USD) **550,993,095.18;**

iv) Madeni ya wananchi yanayotokana na ardhi iliyotwaliwa ili kupisha ujenzi wa reli ya kiwango cha SGR yenye thamani ya shilingi bilioni **46.55**;

v) Wakandarasi kutokamilisha kazi kwa wakati kwenye mradi wa SGR, mfano ni Kipande cha Makutopola - Tabora na Tabora -Isaka.

### 2.4.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

#### a) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali ilitenga fedha Jumla ya takribani shilingi bilioni 126 ambazo zitatumika kama ruzuku katika kutekeleza mradi wa kupeleka huduma za mawasiliano. Utekelezaji wa mradi huu ni miaka kwa miwili na utakamilika ifikapo mwezi Mei, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, kupitia fedha za mradi wa Tanzania ya Kidigitali pamoja na fedha za ndani zitolewazo na Serikali kupitia UCSAF, malipo ya awali yamekwisha lipwa ambayo ni jumla ya **shilingi bilioni 71.54** sawa na **asilimia 56.7** ya lengo. Malipo haya yamelipwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Serikali imepanga kujenga minara 758 katika kata 713 Tanzania Kupitia Mradi huu Kampuni ya TTCL itajenga minara 104 katika kata 104, Airtel itajenga Minara 168 katika kata 161, Honora (Tigo) itajenga minara 262 katika kata 224, Vodacom itajenga Minara 190 katika kata 190 na kampuni ya Halotel itajenga minara 34 katika kata 34.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 31 Julai 2024 jumla ya minara 193 kwenye kata 183 imekwisha washwa sawa na asilimia **25.46** ya Lengo. Airtel amewasha minara 84, Vodacom amewasha minara 37, Honora amewasha minara 57 na Halotel amewasha minara 15.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ambayo yameainishwa hapo juu, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i) Kukosekana kwa miundombinu wezeshi ya ujenzi wa minara ikiwemo umeme na barabara ambapo Mvua kubwa zilizoikabili nchi yetu, zilipelekea kuharibu miundombinu mbalimbali ikwemo miundombinu ya Barabara madaraja;

ii) Changamoto ya kupatikana fedha kwa wakati; na

iii) Utekelezaji usioridhisha wa ujenzi wa minara kwa baadhi ya watoa huduma/washitiri Mfano Kampuni ya TTCL.

## b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa zilizowasilishwa, Kamati imebaini kwamba TCRA imefanikiwa kutoa Elimu kwa Umma, ambapo pia imeendeleza ushirikiano na wadau wa Sekta ya Mawasiliano kuhusu usajili wa laini za simu, usalama mtandaoni, matumizi sahihi na salama ya huduma za mawasiliano na maombi ya leseni za mawasiliano kupitia mfumo ya mtandao *(Tanzanite Portal)*.

**Mheshimiwa Spika,** TCRA imekuwa ikiandaa Makala za Televisheni ambapo Jumla ya vipindi vya kila wiki vya elimu kwa umma mia mbili na nane (208) vilirushwa katika televisheni, kati ya hivyo 102 ni vipindi vya Bambo la Mtaa vilivyotangazwa kupitia Clouds TV na 106 vipindi vya Mawasiliano kwa Maendeleo kupitia TBC1 kufikia Agosti, 2024

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuenea kwa mtandao wa simu *(coverage)*, Kamati ilitaarifwa kwamba, mtandao wa 4G sasa umefikia asilimia 83 ya watu, na pia kumeongeza kasi na upatikanaji wa uhakika wa huduma ya Intaneti. Wakati huo huo, 5G imeenea kwa asilimia **15** ya watu huku ikiongeza kasi ya Intaneti ambayo ni muhimu kwa mahitaji ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kuwa, jumla ya makala na habari mia moja thelathini na tatu (133) ziliandaliwa na kuchapishwa

kwenye magazeti ya kila wiki, zikilenga masuala mbalimbali yaliyofanywa na TCRA na sekta ya mawasiliano kwa ujumla. Aidha, Elimu kupita mitandao ya kijamii *(Facebook, Instagram, LinkedIn, YouTube, threads, Podcast na TikTok)* ambapo wafuatiliaji takiribani (73,416,753) wamefikiwa kwa kipindi cha Julai - Desemba 2023 na Januari – Juni. Kwa upande mwingine, maudhui yenye Elimu kwa Umma yamewekwa kama (Video, Makala, Bango n.k. yaliyopakiwa kwenye tovuti ya https://tcra.go.tz) ambayo yamefikia watumiaji 471,638.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ambayo yameinishwa hapo juu, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo: -

i) Uharibifu wa mara kwa mara wa Miundombinu ya Mawasiliano;

ii) Utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa bado;

iii) Usalama wa Mtandaoni na Uhalifu wa Mtandaoni (Cyber security and Cybercrime); na

iv) Kukosekana kwa udhibiti wa Maudhui ya mitandao.

**c) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaoendeshwa chini ya Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, shughuli za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Taifa cha kutunza Data kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH) zimehamishiwa rasmi kwa TTCL. Aidha, umiliki wake bado unasubiri waraka wa Baraza la Mawaziri (BLM). Aidha, Shirika limefanikiwa kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati mpya wa mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027 wenye mwelekeo wa uchumi wa kidijitali na kuongeza mauzo ya data na intaneti ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Shirika limefanikiwa kufikisha mawasiliano ya intaneti ya kasi (faiba) katika vijiji vipya vya Msomera na Kwala juu na kilele cha Mlima Kilimanjaro inayotarajiwa kuhudumia watalii wote wanaopanda mlima kwa mwaka pia kufikisha Mawasiliano kwenye vijiji vipya vya Msomera na Kwala.

**Mheshimiwa Spika**, TTCL imefanikiwa pia kuboresha mfumo wa masijala (*e-Office*), mfumo wa utendaji na wa fedha kwa kuanza kutumia Enterprise Resources Management System (ERMS). Zaidi ya hayo, Shirika limefanikiwa kupanua wigo wa intaneti kupitia mkongo wa baharini wa EASSY na SEACOM kwa asilimia **286** kutoka 17.5 Gbps hadi 67.5 Gbps Upanuzi huu inatoa hakikisho la upatikanaji wa intaneti).

**Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu, Shirika** linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i) Ukosefu wa mtaji umelifanya Shirika kutofikia malengo ya Mpango mkakati wake uliopita, Shirika lilko kwenye hatari kubwa ya kunyang'anywa soko kutokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na kampuni nyingine za simu hapa nchini hasa Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel;

ii) Sheria na kanuni zisizo rafiki kibiashara kama vile za manunuzi ya umma na ajira kwa watumishi ambapo kwa sasa Shirika halina maamuzi ya mwisho na uwezo wa kuajiri wafanyakazi wapya; na

iii) Kasi ndogo ya kuunganisha wateja.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inabainisha mtazamo na maoni ya jumla kutokana na matokeo ya Shughuli zisizotekelezwa na Kamati.

Lengo lake ni kujulisha masuala mbalimbali yaliyobainika kwa kipindi cha mwaka mzima na kuonesha maoni ya jumla. Aidha maoni hayo yanajenga msingi wa hoja ya Kamati kuhusu mambo ya kufanyiwa kazi iwapo Bunge litaridhia.

### 3.2 Mtazamo na Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi uliofanyika, mambo mbalimbali yaliyobainika yamefafanuliwa ndani ya Taarifa hii. Kwa kuzingatia ufafanuzi huo Kamati ina mtazamo na maoni ya jumla kama ifuatavyo: -

a) Upungufu wa Watumishi kwa LATRA, TAA, MSCL, TANROADS, TTCL na TBA unahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuepuka athari zake kwenye ufanisi na tija ya taasisi hizo.

b) Suala la LATRA na Jeshi la Polisi kuwa na mgongano wa kimajukumu linalostahili kupatiwa ufumbuzi, pia mkakati wa kuwathibiti waendesha bodaboda kwa kuwapa elimu ni jambo muhimu na kuondoa msongamano wa maroli uliopo mpakani mwa Tanzania na nchi jirani linahitaji kupatiwa ufumbuzi;

c) Dhamira ya kuanzishwa kwa TANROADS na manufaa ya ujenzi na ukarabati wa barabara ni mambo yanayohitaji kutiliwa mkazo kwa kutatua tatizo la ufinyu wa bajeti ya TANROADS na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya barabara nchini.

d) Changamoto ya eneo la fedha katika miradi ya EPC+ F ni jambo linaloitaka Serikali kutafuta njia mbadala na ya haraka ili barabara zinazoguswa na miradi hiyo zianze kutekelezwa.

e) Kutokutatua changamoto za TBA kuhusu upungufu wa mtaji na tatizo la wapangaji wengi wa TBA kutokulipa pango ni jambo linalochangia kasi ndogo ya uwekezaji wa TBA kwenye majengo.

f) Suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao linastahili hatua madhubuti za kudhibiti. Kutokudhibiti uhalifu huo ni jambo linalosabisha madhara kwa jamii, ustawi na maadili.

g) Ujenzi wa bandari kavu ni suala linalotakiwa kupewa umuhimu ili kuondoa mlundikano wa mizigo bandarini na kupunguza foleni ya makontena barabarani

h) Suala la mzigo wa madeni kwa shirika la Posta, kasi ndogo ya ujenzi wa minara ya mawasiliano na TTCL kushindwa kujiendesha kibiashara yanastahili kauli madhubuti ya Bunge kwa lengo la kuboresha sekta ya mawasiliano.

### 3.3 Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo niliyoyatoa, sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie ufafanuzi nilioutoa, na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Hoja hii inaliwezesha Bunge kusimamia shughuli za umma kwenye sekta ya Uchukuzi, Sekta ya Ujenzi pamoja na Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwa msingi huo naomba kutoa hoja katika maeneo yafuatayo: -

#### A. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA SHERIA ILIYOANZISHA TAZARA NA UENDESHAJI WA SHIRIKA

**KWA KUWA**, changamoto za utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha TAZARA, unachangia Shirika hilo kutofanya majukumu yake kwa ufanisi, pia kukosekana kwa mtaji wa uendeshaji na fedha za uwekezaji, uwepo wa madeni na kutofanyika kwa matengenezo muhimu, kumesababisha kuharibika kwa injini na ajali za mara kwa mara wakati wa uendeshaji pia kusababisha kero kwa wananchi wa pande zote mbili,

**NA KWA KUWA**, changamoto hizo: -

i) zinaathiri ufanisi katika usimamizi wa Sekta ya uchukuzi na wateja kupoteza imani; na

ii) zinasababisha kero katika shughuli za umma kwenye Sekta ya Uchukuzi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,**

i) Serikali ilete bungeni maboresho ya Sheria iliyoanzisha TAZARA ili kuruhusu marekebisho yatakayowezesha Shirika kujiendesha kibiashara; na

ii) Serikali za pande zote mbili zifanye mazungumzo ya dhati na kuona namna bora ya kuiendesha Reli hiyo.

**B. MADENI YANAYOTOKANA NA MKATABA WA UKODISHAJI NDEGE KATI YA ATCL NA TGFA NA UBORESHAJI WA UTENDAJI WA ATCL**

**KWA KUWA,** changamoto ya uwepo wa madeni ya nyuma yaliyolimbikizwa kabla ya ufufuaji wa ATCL, yanayoathiri mizania ya vitabu vya hesabu za Kampuni, kutopatikana kwa baadhi ya vipuri duniani kama vile injini za ndege, uhaba wa marubani viongozi, na wahandisi, pia kutopata kibali cha kusafirisha mizigo nje ya nchi kwa wakati vimesababisha athari kubwa kwa Shirika na kurudisha nyuma jitihada za kuboresha sekta ya usafiri wa anga;

**NA KWA KUWA**, changamoto hizo za madeni na ubovu huo; -

i) unaathiri ufanisi katika uendeshaji wa shirika la Ndege ATCL;

ii) zinarudisha nyuma Taifa katika azma ya kuwa na shirika kubwa la ndege lenye kutoa huduma kwa ufanisi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,**

i) Serikali iendelee na mchakato wa kuhamisha ndege kutoka TGFA kwenda ATCL na isimamie kuboreshwa kwa sheria ya uanzishwaji wa ATCL ili itambulike kama kampuni na sio shirika la umma;

ii) Serikali iharakishe upatikanaji wa injini mbadala wa ndege aina ya A220-300 na pia itafute namna bora ya kuhakikisha kwamba ndege hizo zinaleta faida kwa nchi;

iii) Serikali ifute deni la TGFA la Sh. bil.**429**, isimamie Taasisi nyingine za Serikali kulipa **Sh. bil 64** kwa ATCL na kulipa madeni ya wazabuni **Sh. bil 18** ili kuondoa changamoto ya madeni ya nyuma yanayokabili shirika;

iv) Serikali iharakishe ujenzi wa chuo cha Mamlaka ya anga Tanzania;

v) Serikali ihakikishe inaboresha maslahi ya Marubani na Wahandisi wa ATCL, kuwahamasisha marubani watanzania walioko nje ya nchi kurudi kufanya kazi katika shirika letu na kuajiri marubani kutoka nje ili kuongeza ufanisi; na

vi) Serikali iendelee kufuatilia vibali vya kusafirisha mizigo China na nchi nyingine duniani.

**C. MADENI YA WAKANDARASI NA WAZABUNI PAMOJA NA FIDIA KWA WANANCHI KWA ARDHI ILIYOTWALIWA**

**KWA KUWA,** kukosekana kwa fedha za kuwalipa Wakandarasi, Wazabuni kwa wakati, wadeni ya fidia kwa wananchi yanayotokana na kutwaliwa kwa ardhi katika kupisha miradi, uchakavu wa njia ya reli (MGR) na uhaba wa vitendea kazi ni changamoto zinazosababisha shirika la reli kushindwa kutekeleza majukumu yake;

**NA KWA KUWA**, changamoto hizo zinaweza; -

i) kusababisha kutofikia malengo ya utekelezaji wa miradi kwa wakati; na

ii) kuathiri ufanisi wa huduma muhimu ya usafiri inayotarajiwa kutolewa kwa wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,**

i) Serikali ilipe madeni ya Wakandarasi na Wazabuni kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosababishwa na riba;

ii) Serikali ilipe fidia kwa wananchi, tathimini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi ifanyike kwa haraka, pia maeneo ambayo yanaonekana hayahitajiki kwa sasa yaachwe kwa wananchi ili yaendelezwe; na

iii) Serikali itoe fedha kwa wakati ili ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli (MGR) ifanyike kwa ufanisi.

**D. MAHITAJI YA FEDHA ZA KUGHARAMIA UJENZI NA MATENGENEZO YA MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA NCHINI**

**KWA KUWA**, usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja nchini unakabiliwa na ufinyu wa bajeti ya ujenzi na matengenezo, uvamizi wa maeneo ya barabara nchini na upungufu wa watumishi wa kutosha kuwezesha tija iliyokusudiwa kwa kuanzisha TANROADS.

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inakwamisha dhamira ya kuanzishwa TANROADS na kutofikia malengo yalivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020-2025 Ibara ya 55 (c),

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

i) Serikali iongeze fedha za ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja, pia itekeleze miradi kwa kuangalia uhalisia na ukomo wa Bajeti uendane na makadirio ya makusanyo;

ii) Serikali ilipe madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosababishwa na riba;

iii) Serikali iharakishe kufanya tathimini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi, pia maeneo ambayo yanaonekana hayahitajiki kwa sasa yaachwe kwa wananchi ili yaendelezwe;

iv) Serikali ijenge barabara kwa kutumia mfumo wa kuwashirikisha wawekezaji binafsi (PPP) na itafute njia mbadala ya kutekeleza ujenzi wa Barabara zilizosainiwa kwa mfumo wa EPC+F;

v) Serikali iwasimamie TANROAD na TAMISEMI ili waweze kushirikiana kutatua changamoto zilizopo kwenye Miradi ya Barabara ziendazo kasi; na

**E. UCHACHE WA WAKANDARASI WA NDANI WENYE UWEZO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA VIVUKO**

**KWA KUWA**, uchache wa Wakandarasi wa ndani wenye uwezo wa utekelezaji wa miradi ya Vivuko, kuwepo kwa mtiririko mdogo wa fedha za miradi ya maendeleo, kuchelewa kwa malipo ya Wakandarasi na malighafi za ujenzi na ukarabati wa vivuko kuagizwa nje ya nchi ni kati ya changamoto zinazosababisha TEMESA kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inasababisha; -

i) kupanda kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya vivuko nchini

ii) kuongezeka kwa gharama za miradi hasa miradi inapotumia muda mrefu kukamilika.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

i) Serikali iwawezeshe wakandarasi wa ndani kwa kuwapa kazi, na kuwalipa kwa wakati ili waweze kutekeleza miradi kwa ufanisi; na

ii) Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa mtiririko mzuri ili miradi ikamilike kwa wakati.

**F. KASI NDOGO YA UWEKEZAJI CHINI YA WAKALA WA MAJENGO (TBA)**

**KWA KUWA**, Wakala wa Majengo Tanzania imebainika kuwa na kasi ndogo ya uwekezaji kutokana na:

i) Upungufu wa mtaji;

ii) Changamoto za kimuundo na kisheria;

iii) Wapangaji kutokulipa pango kwa wakati; na

iv) Upungufu wa watumishi.

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inaweza kuathiri uwezo wa TBA katika kutekeleza agizo la ujenzi wa nyumba 10,000 jambo linalokwamisha manufaa ya nyumba hizo, na uwekezaji mwingine wa kimkakati

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,** Serikali; -

i) itenge fedha za kutosha kuiwezesha TBA kufanikisha azma ya ujenzi wa majengo ya makazi na ofisi;

ii) iendelee kuweka msukumo unaoisaidia TBA kulipwa madeni ya pango zinazodaiwa Taasisi za Serikali;

iii) iwasilishe mapendekezo ya kuwepo kwa Sheria ili TBA iwe na mamlaka kamili, ambayo itawezesha Wakala kuwa na mamlaka ya kisheria na kimuundo kuongeza ufanisi;

iv) iruhusu TBA kuajiri watumishi wanaohitajika ili kufanikisha majukumu yao; na

v) iwezeshe na kuisimamia TBA ili iendelee kutumia ubunifu zaidi wa kujenga majengo na kuingia mikataba yenye tija na Sekta binafsi katika uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo na kuuza.

## G. UTAPELI NA UHALIFU MWINGINE WA KIMTANDAO

**KWA KUWA**, suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao umeendelea kuwepo nchini, jambo hili linapaswa kupatiwa ufumbuzi wa kina,

**NA KWA KUWA**, suala hili linalotokana na maendeleo ya TEHAMA linaathiri uchumi, jamii, ustawi na maadili,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali,

i) iimarishe udhibiti wa uhuru wa mitandao kwa kuzingatia umuhimu wa demokrasia yenye mipaka;

ii) ihakikishe kwamba, TCRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inaweka mikakati madhubuti inayozihusisha kampuni za simu kukabiliana na uhalifu wa kimtandao;

iii) Serikali ihakikishe Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi ya eGA wanashirikiana kwa pamoja kutatua matatizo ya TEHAMA nchini;

iv) Serikali iwekeze katika kukuza teknolojia ya TEHAMA kwa vijana na kuifundisha kwa lugha ya Kiswahili; na

v) Katika kudhibiti uhalifu wa mitandao ya mawasiliano, Serikali ihakikishe kwamba, makampuni ya simu yanawajibika ipasavyo katika kutoa nafuu za kisheria kwa waathirika wa uhalifu wa kimtandao.

**H. KAMPUNI YA MAWASILIANO TANZANIA (TTCL) KUJIENDESHA KIBIASHARA**

**KWA KUWA**, Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inayopaswa kujiendesha kibiashara lakini inashindwa kutokana na: -

i) Taratibu za ajira ya watumishi wake kufungwa na taratibu za Sekta ya umma isiyoongozwa na misingi ya kibiashara;

ii) Upungufu wa fedha kwa ajili ya uwekezaji katika biashara ndani ya Sekta; na

iii) Uwezo mdogo wa kampuni kuunganisha wateja

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali,

i) ihakikishe kuwa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inawezeshwa kifedha ili iweze kuwa na mtaji wa kujiendesha kibiashara;

ii) iangalie upya muundo wa kibiashara TTCL ili Shirika liwe na eneo mahsusi la kuwekeza [kimiundombinu] ambalo litaifanya TTCL iwe na nguvu kibiashara;

iii) iweke mfumo wa utoaji wa vibali vya ajira Serikalini uangaliwe ili kuruhusu kampuni zinazojiendesha kibiashara kuwa na taratibu za ajira zinazoruhusu kuunda ushindani; na

iv) iongeze uwezo wa kutekeleza ujenzi wa minara kwa wakati na kwa ufanisi na kuwa na kasi ya kutosha kuunganisha wateja.

## I. MZIGO WA MADENI NA MTAJI MDOGO WA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

**KWA KUWA**, Shirika la Posta Tanzania limebainika kuwa na mzigo mkubwa wa madeni na mtaji mdogo wa kuweza kujiendesha,

**NA KWA KUWA**, bado changamoto hizo zinakwamisha nia ya Serikali katika kufufua mashirika na kurudisha nyuma maendeleo ya Shirika katika kujiendesha kibiashara,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia Kwamba Serikali,

i) ibebe deni inalodaiwa Shirika la Posta Tanzania la Shilingi **bilioni 54** ili kusafisha mizania ya Shirika na kuliwezesha kukopesheka;

ii) ihakikishe kwamba Shirika linabuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiendesha kibiashara; na

iii) iongeze mtaji kwa Shirika la Posta na kuhakikisha linapata kamisheni kwa kila mzigo kutoka kwa makampuni binafsi ya usafirishaji mizigo.

## J. KASI NDOGO YA UJENZI WA MINARA YA MAWASILIANO

**KWA KUWA**, ujenzi wa minara ya Mawasiliano umebainika kuwa na kasi ndogo kutokana na mchakato mrefu wa kiutaratibu na baadhi ya Wakandarasi kutokamilisha ujenzi kwa wakati kama ilivyokusudiwa,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inakwamisha lengo la Serikali kufikisha mawasiliano nchini kinyume na matarajio ya wananchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali –

i) iongeze kasi ya kutekeleza ujenzi wa minara ya mawasiliano hasa maeneo yaliyoanishwa kuwa na mahitaji maalum mfano, katika barabara kuu, mbuga za wanyama, mipakani na mapori tengefu ili kukuza shughuli za utalii na kuboresha usalama;

ii) isimamie kwa ukaribu baadhi ya makampuni yanayoonyesha kusuasua katika kutekeleza ujenzi wa minara; na

iii) ifanye mapitio ya taratibu za mchakato wa zoezi la ujenzi wa minara ili kuboresha taratibu hizo kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO NA HOJA

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuhitimisha Taarifa hii kwa kutambua utaratibu uliowekwa na Bunge wa kuzitaka Kamati za Kudumu za Bunge kuripoti shughuli zake kwa kipindi cha mwaka. Utaratibu huu unalitaka Bunge kuwa katika nafasi ya kutambua hali ilivyo katika sekta mbalimbali. Ushauri huu wa Bunge kwa Serikali unaweza kufanyiwa kazi kwa Mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika**, naamini kwa maelezo haya na ufafanuzi nilioutoa, utaliwezesha Bunge kujadili inavyostahili na kutoa ushauri kwa Serikali ili kuboresha shughuli na kuongeza tija katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kujituma wakilenga kutoa ushauri unaofaa kwa Bunge. Kufanya hivyo kutaiwezesha Serikali kuboresha maeneo mbalimbali na kuendelea kukidhi matarajio ya wananchi kwa Serikali yao. Kwa

kutambua mchango wao, naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **M/Kiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati, naomba kumshukuru kwa dhati Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb), Waziri wa Ujenzi akishirikiana na Naibu Waziri Mhe. Eng. Msongwe Geofrey Kasekenya (Mb), pia Mhe Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akishirikiana na Naibu Waziri Mhe David Mwakiposa Kihenzile. Vile vile Mhe. Jerry Slaa Mb) Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akishirikiana na Naibu Waziri Mhe. Maryprisca Winfred Makundi (Mb) kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati katika kutimiza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya

Uchukuzi, na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuwawezesha Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kutoa ushirikiano kwenye Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge kwa niaba ya Sekretarieti na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada yakusema hayo, naliomba Bunge lako tukufu lipokee na kuijadili Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ili hatimaye kupitisha mapendekezo yake ili yawe ushauri wa Bunge kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante.

Sasa ninamwita Mwenyekiti, Kamati ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, niwasilishe Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Shughuli za Kamati, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 – Januari, 2025. Ninaomba taarifa hii yote iingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 141 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 na imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza inahusu Utangulizi, ambao unatoa maelezo ya jumla ya utangulizi, ikijumuisha mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Sehemu ya Pili inatoa maelezo kamili kuhusu namna kamati ilivyotekeleza majukumu yake na masuala yaliyobainika kutokana na utekelezaji wa kazi hizo. Sehemu ya Tatu inaeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Maelezo zaidi ni kama yanavyoonekana katika ukurasa wa 1 – 3 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Februari 2024 – Januari 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imetekeleza shughuli zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati, iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari 2024; ziara ya ukaguzi wa miradi, iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024; uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2024/2025; uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba 2024); uchambuzi wa taarifa za utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo; ziara za ukaguzi na mafunzo mbalimbali katika Sekta ya Nishati na Madini; uchambuzi wa utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati, iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya mapendekezo 26 yalitolewa na Kamati na kuazimiwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa 14, ili yatekelezwe na Serikali. Katika Vikao vya Kamati vya Mwezi wa Januari 2025, kamati ilichambua utekelezaji wa maazimio hayo kutoka Wizara zote mbili inazozisimamia. Uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio manne, sawa na 15% yametekelezwa kikamilifu. Maazimio 20, sawa na 77% yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Maazimio mawili, sawa na asilimia nane hayakutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maazimio ya Bunge yaliyotekelezwa kikamilifu ni pamoja na yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuboresha ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara zote mbili, ambapo ukusanyaji umevuka lengo. Kukamilisha kiasi kilichobakia cha Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere na kuanza uzalishaji wa umeme. Kwa sasa mitambo mitano kati ya tisa inazalisha umeme jumla ya Megawati 1,175.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Ujenzi wa kituo cha kushindilia na kujaza gesi asilia *(CNG)* kwenye magari, katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio mawili ambayo hayakutekelezwa kikamilifu ni haya yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuchukua hatua ya kupunguza gharama za kufunga mfumo wa kutumia gesi kwenye magari. Bado gharama ya kufunga mfumo ni wastani wa shilingi milioni mbili kwa gari dogo, tangu mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbil, upatikanaji wa fedha za nje, ambapo Mwaka wa Fedha 2023/2024 fedha za nje kutoka *IMF* kupitia *ECF*, shilingi bilioni 53.2, kwa ajili ya miradi ya *TANESCO*, yaani Gridi Imara na *REA, (Hamlet Electrification Project)* hazikupatikana kabisa. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanapatikana katika ukurasa wa 4 – 6 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha mwaka 2023/2024, uchambuzi wa bajeti na utekelezaji wa bajeti wa Julai – Disemba 2024, unapatikana kuanzia ukurasa wa 6 – 11 wa Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge; kamati inawajibika kufuatilia utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Katika Vikao vya Kamati vya Mwezi Agosti, Oktoba, 2024 na Januari, 2025, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara ya Nishati, jumla ya taarifa 21 zilichambuliwa na kwa Wizara ya Madini taarifa 18 zilichambuliwa. Uchambuzi wa baadhi ya taarifa hizo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme Nchini. Taarifa zilizowasilishwa kwenye kamati zinaonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Disemba 2024, uwezo wa mitambo ya kufua umeme kutoka vyanzo mbalimbali vilivyounganishwa katika Gridi ya Taifa, ulifikia Megawati 3,091.71. Kiasi hiki ni ongezeko la uwezo wa Megawati 1,201.87, sawa na 63.59% katika kipindi cha mwaka mmoja, ikilinganishwa na uwezo wa megawati 1,889.84, mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitambo hiyo ilikuwa na uzalishaji halisi wa umeme *(available capacity)* wa megawati 2,626.82, mwezi Disemba, 2024, kutoka megawati 1,200 zilizokuwa zikizalishwa katika Mwaka 2023. Kiasi hicho ni ongezeko la megawati 1,426.82, sawa na 118.9%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa ongezeko la uzalishaji huo linatokana na mitambo mitano ya Mradi wa Julius Nyerere kuanza kuzalisha umeme. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, kutokana na kuwa na ziada ni muhimu Serikali kutumia fursa hiyo kwa kufikisha umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini; hadi mwezi Januari 2025, takribani vitongoji vyote 12,318 vya Tanzania Bara vilikuwa vimefikiwa na huduma ya umeme. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa jitihada hizi ambazo zimeakisi utekelezaji wa

Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, iliyoelekeza vijiji vyote kufikiwa na huduma ya umeme mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini; hadi Disemba 2024, vitongoji 33,659, sawa na 52.3% ya vitongoji 64,359 vya Tanzania Bara vilikuwa vimefikiwa na umeme. Kuanzia Septemba 24 – 26, Wizara imepanga kufikisha umeme kwenye vitongoji 3,060 kati ya majimbo 204 ya uchaguzi kwa wastani wa vitongoji 15 kwa kila jimbo. Gharama za mradi huo ni shilingi bilioni 350.889. Hadi Disemba 2024, mradi ulifikia 12.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara; upatikanaji wa umeme nchini unategemea masuala ya uzalishaji wa umeme na uwepo wa miundombinu imara ya kusafirisha, kupoza na kusambaza umeme kwa walaji. Kwa sasa hali ya uzalishaji ni ya kuridhisha, lakini changamoto ni kwenye miundombinu ya kusafirisha na kupoza, pamoja na kusambaza umeme, jambo ambalo linaathiri wananchi kwa kukosa umeme kwa viwango vinavyostahili na kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua changamoto hizo, mwaka 2022/2023 Wizara ilianzisha Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (Gridi Imara), kwa gharama ya shilingi trilioni 4.2 na utekelezwaji utatekelezwa kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ina miradi 27 kuanzia Mwaka 2022 hadi Aprili, 2026 kwa gharama ya shilingi trilioni 1.97.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa faida ya mradi huu ni Mkoa wa Kigoma kuunganishwa kwenye umeme wa Gridi ya Taifa, hivyo kuokoa gharama za shilingi bilioni 58.4 kwa mwaka, zilizokuwa zinatumika kwenye mafuta na mitambo ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi wa Nishati Safi ya Kupikia; Serikali kupitia Wizara ya Nishati imepanga kuwa, ifikapo mwaka 2034 matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia *(Clean Cooking)* yafikie 80%. Katika kufikia azma hiyo, Wizara ya Nishati inaendeleza programu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia

tangu Mwaka wa Fedha 2024 hadi sasa. Utekelezaji wake umefanyika kwa namna zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa mitungi ya gesi ya kupikia *(LPG)* kwa bei ya ruzuku, ambapo mwaka 2023/2024 mitungi ya gesi *(LPG)* 83,500 imetolewa kwa wananchi kupitia Waheshimiwa Wabunge. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inatekeleza Mradi wa Kusambaza Mitungi 452,445 kwa Bei ya Ruzuku, kwa gharama ya shilingi bilioni 8.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, tangu kuanza kwa programu hii jumla ya mitungi 123,500 imetolewa kwa wananchi hadi kufikia Disemba, 2024. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, baadhi ya wananchi waliouziwa na kupewa mitungi wamekuwa wakishindwa kujaza gesi kwenye mitungi yao kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo vituo au maduka ya kuuza gesi kuwa mbali, gharama kubwa za kujaza gesi na jiko kwenye mitungi ya gesi kutokukidhi mahitaji ya baadhi ya jamii ikiwa ni pamoja na mtazamo halisi kwamba, chakula kilichopikwa kwenye gesi hakina ladha nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Biashara ya Mafuta Nchini. Mafuta yote yanayotumika nchini na mengine ya kwenda nchi jirani huagizwa nje kwa kupitia mfumo wa uagizwaji wa mafuta kwa pamoja *(BPS)*. Faida ya mfumo huu wa nchi ni kuwa na uhakika wa usalama wa mafuta na kudhibiti upotevu na ubora wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati mwezi wa Januari, 2025 zimeonesha kuwa, mwaka 2024 mwenendo wa biashara ya mafuta uliimarika, ikilinganishwa na mwaka 2023. Kwa mfano, kati ya mwezi Septemba – Disemba, 2024, jumla ya tani 2.51 za mafuta zilingizwa nchini. Kiasi ambacho ni ongezeko la tani 429,100, sawa na 20.59%, ikilinganishwa na tani milioni 2.08 zilizoagizwa nchini kwa kipindi kama hicho mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mafuta kwa pipa katika soko la dunia imeendelea kupungua kuanzia mwezi Agosti hadi Desemba mwaka 2024 kwa wastani wa asilimia tatu nukta tano kwa mwezi, matokeo yake kushuka kwa bei katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ni

maoni ya Kamati kwamba, ili nchi iweze kunufaika na kushuka kwa bei ya mafuta inahitaji kuwa na maghala ya kutosha ya kuhifadhia mafuta kwa kuagiza mafuta mengi pindi yanaposhuka bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya uwajibikaji kwa jamii yaani, *corporate Social Responsibility (CSR)* kutokana na shughuli za uchakataji wa gesi asilia Lindi na Mtwara. Kamati ilitembelea mradi wa uchakataji wa gesi asilia katika kitalu kilichopo kwenye ghuba ya *Mnazi Bay* pamoja na mitambo ya kuchakata gesi inayozalishwa katika Kijiji cha Madimba na Msimbati katika Mkoa wa Mtwara, kupitia mradi huo kumekuwepo na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015 hadi 2023/2024 *TPDC* na wabia wake mbalimbali katika miradi ya gesi asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ilichangia kiasi cha shilingi bilioni 9.3 kama *CSR* katika sekta ya afya, maji, elimu, michezo na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mwaka 2023/2024 pekee kiasi kilichotolewa kilikuwa ni shilingi bilioni 5.4 sawa na 58.06% ya kiasi chote kilichotolewa kwa miaka tisa. Kamati inatambua kuwa ongezeko hili kubwa, kutolewa kwa fedha za *CSR* katika mwaka mmoja tu ni juhudi za makusudi za Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, baada ya kupewa dhamana ya Uwaziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, Kamati inampongeza sana kwa jitihada anazozifanya katika eneo hili ili jamii inufaike kutokana na rasilimali zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kuinua wachimbaji wadogo ili wachangie kikamilifu katika pato la Taifa. Uchimbaji mdogo wa madini umeelezwa na Sheria ya Madini, Sura 123 kuwa ule unaofanywa na Watanzania, yaani wazawa kupitia leseni ya uchimbaji mdogo *(Primary Mining Licences)*. Uchimbaji huo unaratibiwa na Shirika la Madini la Taifa *STAMICO* ambalo limeanzishwa mwaka 1972 ili kushiriki na kuendeleza rasilimali madini nchini kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, *STAMICO* imechukua hatua kadhaa ili kuboresha uchimbaji mdogo

ikiwa ni pamoja na kutoa leseni za uchimbaji mdogo *(Primary Mining Licences – PMLs),* kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchini, wachimbaji wadogo kushirikishwa kwenye sekta ya madini kwa kupata uwakilishi kwenye Tume ya Madini, na kuanzishwa kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo imeleta manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa leseni za uchimbaji mdogo wa madini kutoka 2,456 hadi 6,511 kama inavyoonekana katika kielelezo namba nne cha taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mchakato wa wachimbaji wadogo katika mapato yanayotokana na sekta ya madini nchini umekuwa ukiendelea kukua hadi kufikia asilimia 40 katika mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na asilimia 21 mwaka 2018/2019 kielelezo namba tano cha taarifa kinafafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni mkakati wa Benki Kuu wa ununuzi wa dhahabu. Madini ya dhahabu hutumika kwa nchi nyingi duniani kama akiba na hutunzwa ndani ya Benki Kuu au nje ya nchi baada ya kukidhi viwango vya Kimataifa vya 999.9 *purity* yaani *purity* ya dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hiyo ni kutumia dhahabu kama dhamana ya kupata mikopo katika ulipaji wa madeni na kuilinda thamani ya fedha za nchi. Aidha, hifadhi za dhahabu inaweza kutumika wakati wa misukosuko ya kiuchumi inapoathiri nchi husika. Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)* ilipitisha mpango wa ununuzi wa dhahabu Septemba, 2022 kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa fedha za kigeni hususan dola za Marekani kuboresha akiba ya fedha za kigeni na kulinda thamani ya Shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo ulilenga kununua kiasi cha tani sita za madini ya dhahabu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Utekelezaji wa mpango huu umepata mafanikio ambapo katika kipindi cha miezi mitatu pekee, Oktoba hadi Desemba mwaka 2024 kiasi cha kilogramu 2,323.34 sawa na tani 2.3 za dhahabu kilinunuliwa kutoka kwa wachimbaji wadogo,

wachimbaji wakati na wafanyabiashara wa dhahabu nchini. Kiasi hicho kina thamani ya shilingi bilioni 472.94 kwa mujibu wa bei ya dhahabu ya soko la dunia la tarehe 06/01/2025 iliyotolewa na Tume ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu uchambuzi, utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na ziara za mafunzo yanapatikana ukurasa wa 11 hadi wa 52 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo. Kwa kuwa fedha za *IMF* kupitia *ECF* shilingi bilioni 53.2...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya kwanza imeshapigwa.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa Kuwa, fedha za *IMF* kupitia *ECF* shilingi bilioni 53.2 kwa ajili ya miradi dhidi ya gridi imara ya umeme vitongojini na matumizi mengineyo *OC* ya Wizara na Taasisi zake hazikutolewa mwaka wa fedha 2023/2024 na nusu ya kwanza ya mwaka 2024;

Na Kwa Kuwa, kutopatikana kwa fedha hizo kumeathiri utekelezaji wa miradi ya Gridi Imara na umeme vitongojini na hivyo kukwamisha umeme kufikishwa katika baadhi ya maeneo, jambo ambalo limezua malalamiko mara kwa mara miongoni mwa wananchi;

Hivyo Basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe inapata uhakika *(commitment)* ya upatikanaji wa fedha za *ECF* zinazotelewa na *MF* kabla ya kuzitenga katika bajeti husika. Aidha, ifanye ufuatiliaji wa upatikanaji wa fedha hizo zinazotengwa na kuidhinishwa na bajeti.

Kwa Kuwa, katika jitihada za kutatua changamoto ya umeme wa gridi ya Taifa kukatika mara kwa mara, Serikali ilianzisha mradi wa gridi imara ya mwaka 2022 na kutenga shilingi trilioni 1.97 ili kutekeleza

miradi 27 ya awamu ya kwanza katika kipindi cha mwaka 2022/2024 hadi 2026;

Na Kwa Kuwa, tangu kuanza utekelezaji wa miradi mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa hauridhishi na hivyo kusababisha miradi mitano tu kati ya 27 kukamilika;

Na Kwa Kuwa, kutotolewa kwa fedha hizo kumekwamisha malipo ya jumla ya shilingi bilioni 570.53 kwa wakandarasi pamoja na fidia za maeneo ya wananchi waliopitisha utekelezaji wa miradi hiyo;

Hivyo Basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itoe fedha zote za mradi wa Gridi Imara zilizobakia shilingi bilioni 340 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama ilivyoahidi wakati wa vikao vya bajeti mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikamilishe malipo ya wakandarasi na wananchi wote wanaodai mapema kwa ukamilifu ili kuzuia ongezeko la riba na ucheleweshaji wa malipo na Serikali itekeleze na kumaliza ujenzi wa miradi 22 ya Gridi Imara iliyobakia katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba taarifa yangu rasmi ambayo imeshatolewa, basi iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuwasilisha, lakini pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, pamoja na Waziri wa Madini, Mheshimiwa Antony Mavunde.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Makamu Mwenyekiti wangu, napenda kushukuru Kamati kwa ujumla kwa kufanya kazi nzuri. Napenda kuwashukuru Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuandaa ripoti hii. Pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge na wafanyakazi wake kwa kutusaidia na kutupa ushirikiano wakati wa kazi zetu na uandaji wa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani hizo, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**[*Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023*]**

**SURA YA KWANZA**

**1.0** UTANGULIZI

**1.1** Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini niwasilishe Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

**1.2** Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** muundo wa taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi ambao unatoa maelezo ya jumla ya Utangulizi ikijumuisha mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati;

(b) Sehemu ya Pili inatoa maelezo kamili kuhusu namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake na masuala yaliyobainika kutokana na utekelezaji wa kazi hizo; na

(c) Sehemu ya Tatu inaeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

**1.3** Madhumuni ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, uwasilishaji wa taarifa hii unalenga kueleza majukumu ambayo Kamati imeyatekeleza kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Taarifa inaonesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali. Aidha, taarifa inabainisha maeneo yenye mafanikio pamoja na yale yenye changamoto. Lengo ni kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustawi wa wananchi.

**1.4** Njia na Mbinu zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilitumia njia na mbinu zifuatazo: -

a) Kufanya vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kutathmini utendaji, mafanikio na changamoto zinazowakabili;

b) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali iliyotengewa fedha kwa lengo la kutathmini hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake; na

c) Kupata mafunzo ya ndani kwa lengo la kujenga uelewa wa masuala ambayo Kamati iliona yana umuhimu.

**1.5** Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge unatokana na Ibara ya 96(1) ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977[1]. Kwa kuzingatia muktadha huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeundwa kupitia Kanuni ya 137[2] ikisomwa pamoja na Kifungu cha 5(k) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 6(11) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo, Kamati ya Nishati na Madini imepewa jukumu la kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Vilevile, kifungu cha 7 (1) (a-d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeainisha majukumu yafuatayo kwa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Nishati na Madini: -

a) Kushughulikia bajeti ya Wizara au Taasisi inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 136 (14)[3] ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023;

c) Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu katika Wizara hizo.

## SURA YA PILI

**2.0** SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

**2.1** Maelezo ya Jumla

---

[1] 96.-(1) Bunge laweza kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.
[2] 137.-(1) Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizi.
[3] Kamati yoyote ambayo Spika atapeleka kwake kwanza Muswada au jambo lingine lolote, itahesabiwa kuwa ndiyo Kamati inayohusika kushughulikia Muswada au jambo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(a) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari, 2024;

(b) Ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(c) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(d) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha Nusu mwaka (Julai hadi Disemba, 2024);

(e) Uchambuzi wa taarifa za utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo; na

(f) Ziara za ukaguzi na mafunzo mbalimbali katika sekta za nishati na madini.

**2.1.1** Uchambuzi wa utekelezaji wa Maazimio yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya mapendekezo ishirini na sita (26) yalitolewa na Kamati na kuazimiwa na Bunge lako Tukufu katika mkutano wa kumi na nne. Maazimio hayo yalikuwa na lengo la kuhakikisha Serikali inatekeleza kikamilifu majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Januari, 2025, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio

hayo kutoka Wizara zote mbili inazozisimamia. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo: -

a) Maazimio manne (4) sawa na asilimia kumi na tano (15%) yametekelezwa kimamilifu.

b) Maazimio ishirini (20) sawa na asilimia sabini na saba (77%) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

c) Maazimio mawili (2) sawa na asilimia nane (8%) hayajatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya maazimio ya Bunge yaliyotekelezwa kikamilifu ni pamoja na: -

(a) Kuboresha ukusanyaji wa maduhuli kwa wizara zote mbili, ambapo ukusanyaji ulivuka lengo.

(b) Kukamilisha kiasi kilichobakia cha mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (**JNHPP)** na kuanza uzalishaji wa umeme. Kwa sasa mitambo mitano (5) kati ya tisa (9) inazalisha umeme jumla ya **MW 1,175**.

(c) Ujenzi wa kituo cha kushindilia na kujaza gesi asilia (CNG) kwenye magari katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio katika utekezaji wa maazimio hayo, kamati imebaini kwamba maazimio mawili hayakutekelezwa kikamilifu. Maazimio hayo ni:-

(a) Serikali kuchukua hatua ili kupunguza gharama za kufunga mfumo wa kutumia gesi kwenye magari halijatekelezwa kikamilifu. Hadi sasa, gharama za kufunga mfumo huo bado zipo juu kwa wastani wa **shilingi milioni 2** kwa gari dogo, hali iliyokuwepo tangu mwaka 2023/2024.

(b) Kuboresha mfumo wa upatikanaji wa fedha za nje. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, fedha za nje kutoka IMF kupitia ECF **shilingi Bilioni 53.2** kwa ajili ya miradi ya TANESCO (gridi imara) na REA

(Hamlet Electrification Project) hazikupatikana kabisa. Vilevile katika bajeti ya mwaka 2024/2025, hadi mwezi Januari, 2025 hakukuwa na kiasi kilichopatikana au kutolewa licha ya kutengwa katika bajeti.

**2.1.2** Ziara za Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaweka masharti kwa Kamati za kisekta ikiwemo Kamati ya Nishati na Madini kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Ili kuzingatia masharti hayo, Kamati ilifanya ziara katika mikoa minne ambayo ni Arusha, Dodoma, Pwani na Dar es Salaam na kukagua miradi sita (6). Masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo yaliwasilishwa Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa bajeti za Wizara mwezi Aprili, 2024.

**2.1.3** Uchambuzi wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Bajeti za Wizara inazozisimamia ikiwa ni utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Taarifa hizo zilibainisha masuala mbalimbali kama vile hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024, na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa upande wa Wizara ya Nishati (Fungu 58) bajeti ilipungua kwa kiasi cha **shilingi 1,164,873,084,000.00** ikiwa ni kutoka **shilingi 3,048,632,519,000.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **shilingi 1,883,759,455,000.00** mwaka 2024/2025. Punguzo hilo lilikuwa ni sawa na **asilimia 38.21**. Kupungua huko kulitokana na kupunguzwa kwa ukomo wa bajeti (budget ceiling) iliyotolewa na Serikali kwa Wizara ya Nishati na kukamilika kwa kiasi kikubwa mradi wa JNHPP ambao ulichukua **asilimia 51.72** ya bajeti katika mwaka 2023/2024.

Kwa upande wa Wizara ya Madini (Fungu 100), bajeti iliongezeka kutoka **shilingi 163,008,241,000.00** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **shilingi 231,983,614,000.00** mwaka 2024/2025, na hivyo kufanya ongezeko la **shilingi 68,975,373,000.00** sawa na **asilimia 41.7**.

**2.1.4** Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2024)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2024) kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Lengo lilikuwa ni kutathmini mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha ili kuweza kuishauri Serikali ipasavyo hasa ikizingatiwa kuwa katika kipindi hicho, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha unatakiwa kufikia angalau asilimia hamsini (50%).

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

**a) Wizara ya Nishati**

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 8,000,000.00**. Hadi kufikia mwezi Disemba 2024, kiasi cha **Shilingi 4,426,278.00** kilikuwa kimekusanywa sawa na **asilimia 55.3**. Kwa upande wa bajeti, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 802,329,890,339.29** ambayo ni sawa na **asilimia 42.6** ya kiasi cha **Shilingi 1,883,759,455,000.00** kilichoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 01.**

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) siyo wa kuridhisha kwani kiasi kilichopokelewa ni **Shilingi 8,212,100,498.97** sawa na asilimia kumi na mbili (12%) ya kiasi kilichoidhinishwa cha shilingi **69,524,201,000.00**. Kutokupokelewa kwa fedha hizi kulitokana na Wizara kutokupokea fedha za IMF **shilingi 53,200,000,000** kupitia *ECF* kwa ajili ya kutekeleza miradi ya TANESCO (Gridi imara), umeme vitongojini mradi unaotelezwa na REA (HEP) na OC ya Wizara na taasisi zake za PURA na TPDC.

Kwa upande wa fedha za mishahara, hadi mwezi Disemba, 2024 upatikanaji wake ulikuwa kiasi cha **shilingi 3,965,466,727.16** sawa na

asilimia ishirini (20%) ya kiasi chote kilichoidhinishwa cha **shilingi 19,368,422,000.00.**

Kamati ilifahamishwa kuwa, kupokelewa kiasi kidogo cha fedha za mishahara kunatokana na kutokupokelewa kwa mishahara ya TPDC iliyoidhinishwa kwenye bajeti kwa kuwa tangu mwezi Julai, 2024, TPDC inalipa mishahara kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani. **Kamati inapongeza hatua hii, na hili ni jambo ambalo lingefaa kuigwa na mashirika mengine hususani ya kibiashara**, **na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa mishahara.**

**Kielelezo Na: 1: Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2024**

| AINA | KILICHOIDHINISHWA | KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **OC** | 69,524,201,000 | 8,212,100,498.97 | 12 |
| **MISHAHARA** | 19,368,422,000 | 3,965,466,727.16 | 20 |
| **MAENDELEO NDANI** | 1,536,020,274,000 | 702,957,171,412.36 | 45.8 |
| **MAENDELEO NJE** | 258,846,558,000 | 87,195,151,700.80 | 33.7 |
| **JUMLA** | 1,883,759,455,000 | 802,329,890,339.29 | 42.6 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara ya Nishati ya Januari, 2025 na usanifu wa Sekretarieti ya Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kwa ujumla upatikanaji wa fedha uko chini ya lengo kwa wastani wa asilimia saba (7%), ikilinganishwa na kiasi kilichotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Ni mtazamo wa Kamati kuwa, endapo fedha za *IMF* kupitia *ECF* zingepatikana, kiasi cha fedha zilizopokelewa kingefikia asilimia 50.

**b) Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 1,052,480,027,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 887,630,000,000.00**

zilikusudiwa kukusanywa kupitia idara, vitengo vya Wizara na tume ya madini na kuwasilishwa Hazina**.** Aidha, **Shilingi 164,850,027,300.00** zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo.

Hadi kufikia Disemba 2024, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **562,376,624,707.42** sawa na **asilimia 53.43** ya lengo. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kufikia lengo lililokusudiwa kwenye ukusanyaji wa maduhuli katika kipindi cha miezi sita**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa bajeti, hadi kufikia mwezi Disemba, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 240,271,877,594.15 sawa na asilimia 103.57** ya kiasi cha **shilingi 231,983,614,000.00** kilichoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 02.**

**Kielelezo Na: 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Madini kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2024**

| AINA | KILICHOIDHINISHWA | KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **OC** | 66,449,539,000 | 31,465,316,425.23 | 47.35 |
| **MISHAHARA** | 24,872,875,000 | 9,953,788,903.34 | 40.02 |
| **MAENDELEO NDANI** | 140,661,200,000 | 198,852,772,265.58 | 141.37 |
| **JUMLA** | 231,983,614,000 | 240,271,877,594.15 | 103.57 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara ya Madini ya Januari, 2025 na usanifu wa Sekretarieti ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kupokelewa kwa kiasi kikubwa cha fedha kunatokana na kupokelewa kwa fedha za maendeleo kwa kiasi kikubwa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa. Katika bajeti husika, Bunge liliidhinisha **shilingi Bilioni 140.66** kwa ajili ya fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, Wizara ilipokea **shilingi Bilioni 198.85** sawa na **asilimia 141.37** ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa, kiasi cha **shilingi Bilioni 193.47** sawa na **asilimia 97.3** ya fedha zote zilizopokelewa kilikuwa ni kulipa fedha kwa ajili ya kutekeleza hati za maridhiano (*deed of settlements*) zilizotokana na mashauri manne yaliyofunguliwa na wawekezaji kwenye sekta ya madini dhidi ya Serikali ya Tanzania. Aidha, kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kilikuwa **shilingi Bilioni 5.38** sawa na **asilimia 2.7** ya kiasi chote cha fedha kilichopokelewa.

Kamati inasisitiza kuwa Serikali iongeze kasi ya kupeleka fedha katika kipindi kilichobaki ili kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

**2.1.5** Uchambuzi wa utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina wajibu wa kufuatilia utendaji wa Wizara inazozisimamia ikiwa ni utekezaji wa Masharti ya Kifungu cha 7(1)(d)[4] cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika vikao vilivyofanyika mwezi Agosti na Oktoba, 2024 na Januari, 2025, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara inazozisimamia kama ifuatavyo: -

**(a) Wizara ya Nishati**

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya taarifa ishirini na moja (21) zinazohusu utendaji wa Wizara ya Nishati na taasisi zake zilichambuliwa na Kamati katika kipindi cha mwezi Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Uchambuzi wa baadhi ya taarifa hizo ni kama ifuatavyo: -

**i) Hali ya uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, uwezo wa mitambo ya kufua umeme (*installed capacity*) kutoka vyanzo mbalimbali vilivyounganishwa katika Gridi ya Taifa ulifikia **MW 3,091.71.** Kiasi hiki ni ongezeko la uwezo wa **MW 1,201.87** sawa na **asilimia 63.59** katika

[4] Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

kipindi cha mwaka mmoja ikilinganishwa na uwezo wa **MW 1889.84**[5] mwaka 2023.

Mitambo hiyo ilikuwa na uzalishaji halisia wa umeme (*available capacity*) wa **MW 2626.82** mwezi Disemba, 2024 kutoka **MW 1,200** zilizokuwa zikizalishwa mwaka 2023. Kiasi hicho ni ongezeko la **MW 1,426.82** sawa na **asilimia 118.9**. Kwa sehemu kubwa, ongezeko la uzalishaji huo lilitokana na mitambo mitano ya mradi wa JNHPP kuanza uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, mahitaji ya juu ya umeme nchini yalifikia **MW 1,890.00**, kutoka **MW 1,482.8** zilizofikiwa mwaka 2023. Mahitaji haya yako chini ya kiwango cha umeme unaozalishwa ambao ni **MW 2,626.82**, na hivyo kuwa na ziada ya **MW 736.82**. Aidha, ziada hiyo inatarajiwa kuongezeka baada ya kuwashwa kwa mitambo minne iliyobakia katika mradi wa JNHPP itakayozalisha **MW 940**. **Ni mtazamo wa Kamati kwamba,** k**utokana na kuwa na ziada hiyo**, **ni muhimu Serikali kutumia fursa hiyo kwa kufikisha umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa.**

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwa na ziada ya umeme nchini, uimara katika upatikanaji wa umeme katika baadhi ya maeneo ulikuwa wa kusuasua. Umeme ulkatika mara kwa mara na wakati mwingine umeme kukosa nguvu. Kamati ilielezwa kuwa, hali hiyo imetokana na uchakavu wa miundombinu na kukosekana kwa mashine umba na vituo vya kupoza umeme vya kutosha. **Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ichukue hatua stahiki na za haraka katika kukabiliana na uchakavu na kukosekana kwa uimara wa miundombinu ya umeme na hivyo kuondoa malalamiko kutoka miongoni mwa wananchi.**

### ii) Miradi ya Nishati Vijijini

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali iliyolenga kufikisha umeme maeneo ya vitongoji, vijiji miji na maeneo mengine yenye uhitaji maalum ikiwemo migodi midogo, viwanda

[5] Taarifa ya Kamati ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, ukurasa wa 11 hadi 12 pamoja na Taarifa ya Wizara ya Nishati kwenye Kamati ya tarehe 16 Mwezi Januari, 2025.

vidogo na maeneo ya kilimo. Uchambuzi kuhusu utekelezaji huo ni kama ifuatavyo: -

**(a) Miradi ya kusambaza umeme vijijini**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Januari, 2025, takribani vijiji vyote **12,318** vya Tanzania Bara vilikuwa vimefikiwa na huduma ya umeme. **Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa jitihada hizi ambazo zimeakisi utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala (CCM) ya Mwaka 2020 iliyoelekeza vijiji vyote kufikiwa na huduma ya umeme mwaka 2025.**

**(b) Mradi wa kupeleka umeme vitongojini**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania Bara ina jumla ya vitongoji **64,359**, ambapo hadi mwezi Disemba, 2024 vitongoji **33,657** sawa na **asilimia 52.3** vilikuwa vimefikiwa na umeme. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Septemba, 2024 hadi Septemba, 2026, pamoja na hatua nyingine, Wizara imepanga kutekeleza mradi wa kufikisha umeme kwenye vitongoji **3,060** katika **majimbo 204** ya uchaguzi kwa wastani wa vitongoji 15 kwa jimbo. Gharama za mradi huo ni **shilingi Bilioni 350.889** zinazofadhiliwa na Serikali ya Tanzania. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, utekelezaji wa mradi huu ulifikia **asilimia 12.3**.

Aidha, mwaka 2024/2025 hadi 2026/2027, Serikali imepanga kutekeleza mradi (HEP IIB) kwa kupeleka umeme kwenye **vitongoji 10,000** kwa gharama ya **shilingi Trilioni 1.5** kwa kuanza na vitongoji **4000** mwaka 2024/2025. Ni imani ya Kamati kuwa **Serikali itaongeza kasi na kutoa kipaumbele kwa kukamilisha miradi hiyo mapema ili wananchi waanze kufaidi umeme huo**.

**(c) Mradi wa kusambaza umeme kwenye vijiji miji (Peri-Urban) awamu ya pili na awamu ya tatu**

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza miradi hii, Wizara kupitia REA imekuwa ikitekeleza kwa kuchagua mikoa. Mathalani, mradi wa vijiji miji awamu ya kwanza ulioanza Julai, 2022 hadi Disemba, 2024, ulifikisha umeme kwenye mikoa mitatu ambayo ni Mwanza, Dodoma na Arusha. Hadi mwezi Disemba, 2024, mradi ulikamilika kwa kufikisha

umeme kwenye **vijiji miji 165** vya mikoa hiyo kwa gharama ya **shilingi bilioni 31.4** zilizotolewa na Serikali ya Tanzania. Mradi kama huo awamu ya tatu ulianza mwezi Februari, 2023 na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2025 kwa kufikisha umeme kwenye vijiji miji, mitaa na vitongoji **416** katika mikoa nane ya Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida, Tabora na Tanga. Hadi Disemba, 2024, mradi ulikuwa umefikia **asilimia 87**.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa bado kuna idadi kubwa ya vijiji miji vilivyoko katika mikoa iliyosalia nchini havijafikishiwa na umeme. **Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iongeze wigo wa mradi huo kwa kuingiza mikoa yote yenye changamoto hiyo na kufikisha umeme katika maeneo hayo.**

**iii) Utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara**

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa umeme nchini unategemea masuala makuu mawili ambayo ni uzalishaji wa umeme wenyewe na uwepo wa miundombinu imara ya kusafirisha umeme, kuupoza na kuusambaza kwa walaji.

Kwa sasa, hali ya uzalishaji wa umeme ni ya kuridhisha. Changamoto kubwa imebakia kwenye suala la miundombinu ya kusafirisha, kupoza na kusambaza umeme, na hivyo kuathiri wananchi kwa kutokupata umeme wa viwango stahiki na wenye uhakika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hizo, pamoja na hatua nyingine, mwaka 2022/2023 Wizara ilianzisha mradi wa kuimarisha Gridi ya Taifa (Gridi Imara), wenye gharama ya **shilingi Trilioni 4.2**. Mradi huo umepangwa kutekelezwa katika awamu tatu (3). Awamu ya kwanza ina **miradi 27** na inatekelezwa kuanzia mwaka 2022 hadi mwezi Aprili, 2026, kwa gharama ya **shilingi Trilioni 1.97**. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, utekelezaji wa miradi yote 27 ulikuwa kama ifuatavyo: -

(a) Miradi mitano (5) imekamilika kwa asilimia 100;
(b) Miradi mitano (5) imefikia kati ya asilimia 60 hadi 99;
(c) Miradi sita (6) imefikia kati ya asilimia 30 hadi 59;

(d) Miradi saba (7) imefikia kati ya asilimia 10 hadi 29; na
(e) Miradi minne (4) imefikia kati ya asilimia 0 hadi 9.

**Mheshimiwa Spika,** mojawapo ya faida iliyopatikana kwa kukamilika kwa miradi mitano ni mkoa wa Kigoma kuunganishwa kwenye umeme wa gridi ya Taifa, jambo lililosababisha kuzimwa kwa mitambo iliyokuwa inatumia mafuta kuzalisha umeme na hivyo kuokoa kiasi cha shilingi **Bilioni 58.4** kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu miradi 22 iliyosalia, uchambuzi ulionesha kuwa asilimia kubwa ya miradi hiyo muda wa utekelezaji wake umekwisha kwa mujibu wa mikataba. Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2024, wakandarasi wa miradi na wananchi waliopisha maeneo yao ili miradi hiyo itekelezwa, wanaidai Serikali jumla ya **shilingi Bilioni 570.53.** Madai haya yana uwezekano wa kuendelea kuongezeka kutokana na riba inayotokana na malipo kucheleweshwa, kutokana na Serikali kutokupeleka fedha kikamilifu. Kielelezo Na.03 kinafafanua zaidi.

**Kielelezo Na: 3: Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Miradi ya Grid Imara, Madai ya Wakandarasi katika kuktekeleza miradi hiyo na kiasi kinachotolewa na Serikali katika mwaka husika.**

| Mwaka | Kiasi cha fedha kilichopangwa | | |
|---|---|---|---|
| | Fedha iliyotengwa kwenye Bajeti | Fedha iliyoombwa na Wizara | Fedha iliyotolewa na Serikali |
| 2022/23 | 500,000,000,000 | 331,200,000,000 | 90,900,000,000 |
| 2023/24 | 473,000,000,000 | 388,560,000,000 | 133,000,000,000 |
| 2024/25 | 200,000,000,000 | 345,500,000,000 | 88,130,000,000 |
| **JUMLA** | **1,173,000,000,000** | **1,074,260,000,000** | **312,030,000,000** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Wizara ya Nishati ya Januari, 2025 na usanifu wa Sekretarieti ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondokana na hali hii, ni rai ya Kamati kuwa, **Serikali iliangalie suala hili kwa ukaribu unaostahiki ili miradi yote ya**

**gridi imara ya awamu ya kwanza ikamilishwe katika muda uliopangwa.**

### iv) Utekelezaji wa Mradi wa Nishati Safi ya Kupikia

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imepanga kuwa ifikapo mwaka 2034, matumizi ya nishati safi ya kupikia (clean cooking) yafikie asilimia themanini (80%). Katika kufikia azma hiyo, Wizara ya nishati inaendeleza progamu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia tangu mwaka wa fedha 2023/2024 hadi sasa. Utekelezaji wake unafanyika kwa namna zifuatazo: -

#### *(a) Usambazaji wa mitungi ya gesi ya kupikia (LPG) kwa bei ya ruzuku*

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2023/2024, Wizara iligawa mitungi ya gesi (LPG) **83,500** kwa wananchi kupitia Waheshimiwa Wabunge. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara inatekeleza mradi wa kusambaza **mitungi 452,445** kwa bei ya ruzuku kwa gharama ya shilingi **Bilioni 8.6**. Kwa ujumla, tangu kuanza kwa programu hii, jumla ya **mitungi 123,500** imetolewa kwa wananchi hadi kufikia Disemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, baadhi ya wananchi waliouziwa na kupewa mitungi wamekuwa wakishindwa kujaza gesi kwenye mitungi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

1. Vituo au maduka ya kununua gesi kuwa mbali na hivyo kuhitajika gharama kubwa ya nauli kujaza mtungi gesi hizo;

2. Gharama kubwa kujaza gesi ikilinganishwa na mkaa na kuni;

3. Jiko lililopo kwenye mtungi wa gesi kutokukidhi mahitaji kwenye baadhi ya jamii ambazo zina utamaduni wa kupika chakula kingi kwa wakati mmoja; na

4. Mtazamo hasi kwamba chakula kinachopikwa kwenye gesi hakina ladha ikilinganishwa na kinachopikwa kwenye mkaa na kuni.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, kutokana na sababu hizo, baadhi ya familia zilizopewa mitungi hiyo zimekuwa zikiiuza kama chuma chakavu na familia nyingine zinaitumia kwa ajili ya kuendeshea mitambo na kangavuke (jenereta) badala ya kupikia.

***(b) Usambazaji wa gesi Asilia (LNG) majumbani kwa ajili ya kupikia katika mikoa ya Lindi na Pwani***

**Mheshimiwa Spika**, mradi huo ulianza kutekelezwa katika mwaka 2023/2024 na kuendelea mwaka 2024/2025 kwa gharama ya shilingi **Bilioni 6.82** kupitia TPDC, kwa ufadhili wa REA.

Kamati ilielezwa kuwa, matumizi ya gesi asilia kupikia majumbani yana gharama ndogo zaidi ikilinganishwa na nishati ya mkaa, gesi ya mitungi (LPG) na umeme. Aidha, ilionekana pia kuwa, matumizi ya gesi asilia ni salama zaidi pindi kunapotokea kuvuja kwa gesi ikilinganishwa na gesi ya mitungi (LPG).

***(c) Miradi mingine ya nishati safi ya kupikia***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mingine ikiwemo usambazaji wa majiko banifu, ufungaji wa mifumo ya kupikia kwenye taasisi zenye zaidi ya watu 300, uzalishaji wa mkaa mbadala kwa kutumia makaa ya mawe (coal briquete) unaotekelezwa na STAMICO. **Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itekeleze miradi hiyo kwa kuzingatia mradi unaokidhi mazingira ya jamii husika.**

**v) Taarifa kuhusu utendaji kazi wa kampuni tanzu za TANESCO**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua taarifa kuhusu utendaji kazi wa kampuni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme (ETDCO) na kampuni ya uzalishaji wa nguzo za zege Tanzania (TCPM) ili kupata taarifa kuhusu uanzishwaji na utekelezaji wa majukumu ya kampuni hizo. Uchambuzi wake ni kama ifuatavyo:-

**(a) Kampuni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme (ETDCO)**

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ilianzishwa mwaka 2016 kwa lengo la kujenga na kukarabati miundombinu ya umeme ndani na nje ya nchi kwa gharama nafuu, viwango vya hali ya juu na katika muda mfupi ili kuisaidia Serikali kutekeleza miradi ya umeme kwa tija na unafuu ikilinganishwa na wakandarasi wengine. Aidha, kampuni hiyo inatekeleza miradi hiyo kwa fedha za kitanzania ikilinganishwa na Kampuni za nje ambazo zinatekeleza miradi kwa fedha za kigeni hususani Dola za Kimarekani.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Septemba, 2024 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 Kampuni ilipata jumla ya kandarasi **hamsini na nne (54)** za ndani ya nchi kutoka TANESCO na REA. Kati ya hizo, ilikuwa imekamilisha kandarasi thelathini na tano (35), na kandarasi kumi na tisa (19) ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kutokana na kazi hizo, Kampuni ilianza kupata faida ambayo imeongezeka hadi, **shilingi Bilioni Bilioni 7.3** mwaka 2024 na hivyo kuiwezesha kampuni kulipa mishahara na stahiki nyingine za wafanyakazi wake wote.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kampuni hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mtaji mdogo na hivyo kushindwa kununua mitambo inayohitajika, uchache wa watalaam hususani wahandisi na kukosekana kwa kitengo cha biashara. Hali hii imesababisha kusuasua kwa utekelezaji wa miradi iliyoipata, kushindwa kupata kazi za kutosha za ndani ya nchi, na kutokupata kandarasi nje ya nchi.

**(b) Kampuni ya uzalishaji wa nguzo za zege Tanzania (TCPM).**

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ilianzishwa mwaka 2014 ili kufanya biashara ya kutengeneza na kuuza nguzo za zege na kutoa ushauri katika masuala mbalimbali ikiwemo uhandisi, mazingira, ujenzi na tathmini ya kiteknolojia.

Kamati ilielezwa kuwa, nguzo za zege ni nafuu na salama ikilinganishwa na nguzo za miti. Unafuu huo unatokana na nguzo hizo kuwa imara, kutokuathiriwaa na matukio ya kuchoma moto misitu, zinadumu kwa muda mrefu takribani miaka sabini na tano (75) hadi miamoja (100). Aidha, zinatumia gharama ndogo kutengenezwa na katika muda mfupi (takribani siku 21) ikilinganishwa na nguzo za miti ambazo zinatumia miaka 15 hadi 30 tangu mti kupandwa hadi kukomaa na kuwa tayari kutumika kwa ajili ya nguzo za umeme.

Licha ya uhumimu wa nguzo hizo, Kampuni haikuweza kufikia malengo ya kuzalisha nguzo toshelezi kutokana na kukabiliwa na changamoto ya kukosa mtaji. Ilielezwa kuwa, wakati wa uanzishwaji wake, mtaji wa kuanzia ulitegemewa kuwa kiasi cha **shilingi Bilioni 8.** Hata hivyo, Serikali haikuweza kutoa mtaji huo kwa mara moja kadiri ilivyokuwa imepangwa.

Katika kukabiliana na hali hiyo, mwaka 2016 iliamua kuanza kutekeleza kazi mbalimbali kupitia ubia (joint venture agreements) na wawekezaji wa ndani (wazawa). Makubaliano hayo yamewezesha kuanzisha viwanda vya kuzalisha nguzo za zege katika mikoa minne ya Tanga, Arusha, Morogoro, Shinyanga na Tabora.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana katika biashara hiyo ni pamoja na kutengeneza faida kwa mara ya kwanza ya **shilingi Bilioni 2.028** mwaka 2023/2024, kununua magari, ardhi na vitendea kazi vyenye thamani ya shilingi **milioni 538.15** na kusambaza nguzo za zege **36,064** zilizouzwa kwa TANESCO na ETDCO. Kupitia biashara hiyo, Kampuni inadai jumla ya deni la **shilingi Bilioni 19.84**, ambapo TANESCO inadaiwa shilingi **Bilioni 18.08** na ETDCO shilingi **Bilioni 1.77**.

### vi) Mwenendo wa Biashara ya Mafuta Nchini

#### (a) Uagizaji wa mafuta

**Mheshimiwa Spika,** mafuta yote yanayotumika nchini na mengine kwenda nchi jirani huagizwa nje ya nchi kupitia mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (BPS). Kamati ilielezwa mafanikio ya kutumia mfumo wa BPS kuagiza mafuta kuwa ni pamoja na:-

(a) Nchi kuwa na uhakika wa usalama katika upatikanaji wa mafuta;

(b) Udhibiti wa upotevu wa mafuta kutoka asilimia 0.35 hadi asilimia 0.10. Aidha, mwezi Novemba, 2023 PBPA ilifunga mfumo wa SCADA kwa ajili ya kufuatilia mtiririko wakati wote wa kushusha mafuta. Mfumo huo umesaidia kupunguza upotevu wa mafuta kwa **tani 1,250** yenye thamani ya **shilingi Bilioni 4.53** mwezi; na

(c) Udhibiti wa ubora wa mafuta. Kutokana na mafuta kuagizwa kwa Pamoja, TBS imeweza kufanya uhakiki wa ubora wa mafuta kwa urahisi na kwa haraka kabla ya kushushwa.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zilizowasilishwa kwenye Kamati mwezi Januari, 2025 zinaonesha kuwa mwaka 2024 mwenendo wa biashara ya mafuta uliimarika ikilinganishwa na mwaka 2023. Kwa mfano; kati ya mwezi Septemba hadi Disemba, 2024, jumla ya **Tani za mafuta 2,512,895** ziliingizwa nchini.

Kiasi hicho ni ongezeko la **Tani 429,100** sawa na **asilimia 20.59** ikilinganishwa na **tani 2,083,795** zilizoingizwa nchini kwa kipindi kama hicho mwaka 2023. Katika **tani hizo 2,512,895** zilizoingizwa nchini kwa Septemba hadi Disemba, 2024, **Tani 1,164,531 (asilimia 46.3)** za mafuta hayo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi, na **tani 1,348,364 (asilimia 53.7)** kwa ajili ya nchi jirani *(transit)***.**

**Mheshimiwa Spika,** tani hizo ziliingizwa nchini kupitia zabuni arobaini na tatu **(43)** zilizoratibiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa pamoja (PBPA). Kati ya zabuni hizo, TPDC lilishinda zabuni moja **(1)** tu ya kuagiza mafuta ya dizeli na zabuni 42 zikienda kwenye kampuni nane (8) za binafsi. Hali kama hii ilijitokeza pia mwaka 2023, ambapo TPDC ilishinda zabuni moja tu kati ya zabuni 42 zilizoshindanishwa.

**(b) Bei ya mafuta kupungua**

**Mheshimiwa Spika,** bei ya mafuta kwa pipa katika soko la dunia imeendelea kupungua kuanzia mwezi Agosti kuelekea mwezi Disemba, 2024 kwa wastani wa **asilimia 3.5** kwa mwezi. Matokeo ya kupungua kwa bei yameendelea kuonekana ndani ya nchi, ambapo

mafuta yameendelea kushuka bei kwa mkoa wa Dar es Salaam. Mbali na kushuka kwa bei kwenye soko la dunia, kupungua huko kulisababishwa na kuimarika kwa shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani. Ufafanuzi kuhusu kupungua kwa aina zote za mafuta ni kama ifuatavyo: -

a) Petroli – ilipungua na kufikia **Shilingi 2,898** kwa lita mwezi Disemba, 2024 ikiwa ni upungufu wa **asilimia 10.3** kutoka **Shilingi 3,231** kwa lita mwezi Agosti, 2024;

b) Dizeli – ilipungua na kufikia **Shilingi 2,779** kwa lita mwezi Disemba, 2024 ikiwa ni upungufu wa **asilimia 11.2** kutoka **Shilingi 3,131** kwa lita mwezi Agosti, 2024; na

c) Mafuta ya Taa – yalipungua na kufikia **Shilingi 2,831** kwa lita mwezi Disemba, 2024 ikiwa ni upungufu wa **asilimia 13.1** kutoka **Shilingi 3,257** kwa lita mwezi Agosti, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kwamba, ili nchi iweze kunufaika na kushuka kwa bei ya mafuta, inahitaji kuwa na maghala ya kutosha ya kuhifadhia mafuta kwa kuagiza mafuta mengi pindi yanaposhuka bei. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umeendelea kubaini kuwa uagizaji wa mafuta kwa mwezi umeongezeka kutoka wastani wa **tani 300,000** kwa mwezi mwaka 2012 hadi kufikia **tani 600,000** kwa mwezi mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 100**, wakati hakujawa na ongezeko kwa upande wa maghala ya kuhifadhi mafuta katika kipindi hicho.

**i) Ziara ya mafunzo katika sekta ya nishati**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024, Kamati ilifanya ziara mbalimbali za mafunzo nchini. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Kagera, Lindi na Mtwara, ili kujifunza na kukagua utekelezaji wa miradi chini ya Wizara ya Nishati. Maelezo kuhusu baadhi ya ziara hizo ni kama ifuatavyo: -

**a. Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere-JNHPP (MW 2115) Rufiji-Pwani**

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa bwawa ulianza mwaka 2018 ukitazamiwa kukamilika mwezi Juni, 2024, kwa gharama ya **shilingi Trilioni 6.558**. Kamati ilipotembelea na kukagua mradi huu mwezi Julai, 2024, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 98.9**. Aidha, kiasi cha malipo ya **shilingi Trilioni 6.167** sawa na **asilimia 94.03** kilikuwa kimeshalipwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Katika kipindi hicho mitambo minne ilikuwa inazalisha umeme **MW 940**. Hata hivyo, taarifa za kutokana na taarifa ya Wizara kwenye Kamati ya Januari, 2025 zinaonesha kwamba, hadi Disemba, 2024, mradi ulifikia **asilimia 99.55** na jumla ya mitambo mitano (5) ilikuwa imeshawashwa na kuzalisha umeme wa **MW 1,175** kwenye gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wa mradi huo, Kamati ilifahamishwa kuwa katika baadhi ya nyakati, mitambo imekuwa ikiruhusiwa kuzalisha umeme chini ya uwezo wake au kupumzishwa kwa baadhi ya mitambo kutokana na matumizi ya umeme kuwa chini. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa umeme wote unaozalishwa ungeweza kutumika kwa kuwa mahitaji ya umeme bado ni makubwa, isipokuwa tu kuna ukosefu wa miundombinu wezeshi ya kufikisha umeme katika maeneo yote nchini. Mfano dhahiri ni mikoa ya Lindi, Mtwara, Rukwa, Kagera na Katavi kutokuunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa ambao unajumuisha umeme wa bwawa la Julius Nyerere (JNHPP).

**b. Mradi wa kufua umeme wa bwawa la Rusumo (MW 80)-Ngara, Kagera**

**Mheshimiwa Spika,** mradi umetekelezwa, kusimamiwa na kumilikiwa na Kampuni ya *Rusumo Power Company Limited (RPCL)* iliyoundwa mwaka 2013. Kampuni hiyo (RPCL) inamilikiwa kwa usawa na wanahisa watatu ambao ni nchi ya Tanzania, Rwanda na Burundi. Utekelezaji wa mradi ulianza mwaka 2016 ukitegemewa kukamilika mwezi Oktoba, 2019 kwa jumla ya Dola za Kimarekani **Milioni 421**. Hata hivyo, kufuatia changamoto mbalimbali, mradi ulikamilika mwezi

Juni, 2024 na kuanza kuzalisha **MW 80** zinazogawanywa katika **MW 26.6** kwa kila nchi.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulienda sambamba na utolewaji wa fedha za uwajibikaji kwenye jamii **(CSR)** wenye jumla ya Dola za Marekani **Milioni 10 (Shilingi Bilioni 25)** kwa kila nchi. Kwa upande wa Tanzania, fedha hizo zilitolewa kwa Wilaya ya Ngara ili zitekeleze miradi ishirini na tano (25) inayohusu elimu, afya, masoko na gari la zimamoto.

Kamati ilipofanya ziara mwezi Novemba, 2024 ilielezwa kuwa miradi kumi na tano (15) ilikamilika na kuanza kutoa huduma, na miradi mingine kumi (10) ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya miradi iliyokaguliwa ni: -

(i) Ujenzi wa kituo cha afya Rusumo. Hadi muda wa ukaguzi, kituo kilikuwa kimekamilika na kuanza kutoa huduma. Kamati ilielezwa kuwa, ujenzi wa majengo ulitumia gharama ya shilingi **Bilioni 1.42**, na ununuzi wa vifaa tiba uligharimu **shilingi Milioni 268**. Hata hivyo, Kamati ilibaini kutokuwepo kwa vifaa muhimu kama vile *x-ray* na jokofu kwa ajili ya mochwari, licha ya vyumba vya huduma hiyo kujengwa. Kamati ilipohoji ilifahamishwa kuwa vifaa hivyo havikuwa sehemu ya mradi wa **CSR**.

(ii) Mradi wa kuzalisha maji katika kijiji cha Rusumo. Kamati ilielezwa kuwa mradi huo ulitumia **shilingi Bilioni 3** na kuanza kutoa huduma kwenye **kaya 322**. Kamati ilibaini kuwa, ujenzi wa mradi haukuangalia mahitaji ya mbeleni ili kukidhi mahitaji kwa muda mrefu kutokana na ongezeko la watu katika eneo hilo.

(iii) Mradi wa soko la Kimkakati la Kahaza kwa ajili ya mazao ya kwenda nje ya nchi. Mradi huo unagharimu shilingi **Bilioni 2.51**. Hadi wakati wa ukaguzi tarehe 10 Novemba, 2024, kiasi cha **shilingi Bilioni 1.45** kilikuwa kimetumika, na matarajio ilikuwa ni kukamilisha ujenzi ifikapo tarehe 27 Novemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** katika miradi iliyokaguliwa na taarifa ya miradi ambayo haikukaguliwa, Kamati ilipata wasiwasi kutokana na

gharama za utekelezaji wake kuonekana kuwa juu, ikilinganishwa na ujenzi wa miradi inayotekelezwa na Serikali. Kamati ilifahamishwa kuwa, ujenzi wa miradi katika mradi wa **RPCL** ulitumia taratibu za manunuzi za **WB** ambazo zinachukua muda mrefu na gharama kubwa.

**c. Miradi ya Uwajibikaji kwa Jamii (Corporate Social Responsibility-CSR) kutokana na shughuli za uchakati wa ges asilia Lindi na Mtwara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea mradi wa uchakataji wa gesi asilia katika kitalu kilichopo kwenye ghuba ya Mnazi (Mnazi bay) pamoja na mitambo ya kuchakata gesi inayozalishwa katika kijiji cha Madimba na Msimbati katika mkoa wa Mtwara. Kupitia mradi huo, kumekuwepo na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya CSR.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015 hadi 2023/2024, TPDC na wabia wake mbalimbali katika miradi ya gesi asilia katika mkoa wa Lindi na Mtwara ilichangia kiasi cha **shilingi Bilioni 9.3** kama CSR katika sekta ya afya, maji, elimu, michezo na utawala bora.

Aidha, kwa mwaka 2023/2024 pekee, kiasi kilichotolewa kilikuwa **shilingi Bilioni 5.4**, sawa na **asilimia 58.06** ya kiasi chote kilichotolewa kwa miaka tisa. Kamati inatambua kuwa, ongezeko hili kubwa la kutolewa kwa fedha za CSR katika mwaka mmoja tu, ni juhudi za makusudi za **Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mb Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, baada ya kupewa dhamana ya Uwaziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu. Kamati inampongeza sana kwa jitihada anazozifanya katika eneo hili ili jamii inufaike kutokana na raslimali zake**.

**Mheshimiwa Spika,** kiasi kilichotolewa mwaka 2023/2024 cha **shilingi Bilioni 5.4** kililenga kutekeleza jumla ya miradi kumi na tisa (19) katika Mkoa wa Lindi na Mtwara. Kamati katika ziara yake iliyofanyika mwezi Septemba, 2024, iliweza kukagua miradi miwili ambayo ni ujenzi wa wa kituo cha afya na ujenzi wa kituo cha polisi inayotekelezwa katika Kijiji cha Msimbati, Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu ujenzi wa kituo cha afya Msimbati, fedha za ujenzi zilitolewa na TPDC ni **shilingi milioni 759.87**, ambapo Halmashauri ya Mtwara inajenga kituo hicho kupitia mfumo wa *force account* kwa lengo la kuhudumia wakazi wa kata ya Msimbati. Katika ukaguzi wake, Kamati ilibaini kuwa kituo kina majengo ya kutosha kuhudumia wakazi wa kata ya msimbati na kata Jirani. Kamati Ilielezwa kuwa ujenzi wa kituo hicho ulikuwa umefikia **asilimia 95**, na kwamba kiasi cha **shilingi milioni 600** kilikuwa kimetumika.

Kuhusu ujenzi wa kituo cha Polisi Msimbati, Kamati ilipofanya ukaguzi katika mradi huo mwezi Septemba, 2024, ujenzi ulikuwa umekamilika kwa asilimia mia moja (100). Ilielezwa kuwa, gharama za ujenzi wa kituo hicho zilikuwa **shilingi Milioni 186.17** zilizotolewa na TPDC kama CSR, na ujenzi wake ulisimamiwa na Jeshi la Polisi Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa Kamati ilibaini kuwa licha ya mradi huo kukamilika, huduma zilizokusudiwa zilikuwa bado hazijaanza kutolewa kutokana na ukosefu wa nyumba za kuishi askari na mkuu wa kituo hicho, samani za kituo na miundombinu ya maji. **Kamati ilishauri kuwa changamoto zilizoelezwa zipatiwe ufumbuzi wa muda mfupi ili kuwezesha wananchi kuanza kufaidi matunda ya rasilimai zao za asili**.

**d. Ujenzi wa kituo cha kushindilia na kujaza gesi asilia (CNG) kwenye Magari, Sam Nujoma-Dar es Salaam (UDSM)**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko kubwa la wanachi hususani katika mkoa wa Dar es Salaam kufunga mfumo kwenye magari wa kutumia gesi asilia, ambapo magari takribani 4500 yameshafungwa mfumo huo. Ongezeko hilo limesababisha uwepo wa foleni kiasi cha madereva bajaji na magari kutumia saa **tatu hadi tano** kusubiri huduma. Kamati ilishuhudia foleni hizo mwezi Machi, 2024 wakati wa ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha, na kuishauri Serikali kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuongeza pampu za kujaza gesi na kujenga vituo vingine.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza maelekezo ya Kamati na maazimio ya Bunge lako, Wizara inatekeleza mradi wa ujenzi wa kituo mama cha kushindilia na kujaza gesi kwenye magari (**mother station**)

pamoja na kuweka mfumo kwenye magari ili yaweze kutumia gesi asilia (**CNG**) katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), na vituo vidogo (daughter stations) viwili Muhimbili na Kibaha. Gharama za mradi wa vituo vyote ni **shilingi Bilioni 18.9**, ambapo kituo mama kinagharimu **shilingi Bilioni 14.9**, na vituo vidogo **shilingi Bilioni 2** kwa kila kituo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea na kukagua ujenzi wa kituo mama mwezi Januari, 2025, utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia **tisini (90),** na umepangwa kukamilika mwezi Februari, 2025. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kujaza gesi asilia kwenye **magari 1200** kwa siku, na kushindilia gesi takribani futi za ujazo **Milioni 3.1** kwa siku ambayo itatumika na vituo vidogo (*daughter stations*), kutumika kwenye magari na na kuuzwa kwa wawekezaji binafsi wenye vituo hivyo. Kamati ilielezwa kuwa, tayari magari tisa (9) yameshanunuliwa ikiwa ni sehemu ya mradi kwa ajili ya kusafirisha gesi hiyo.

### (b) Wizara ya Madini

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wizara ya Madini, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili jumla ya taarifa kumi na nane (18) za utendaji wa Wizara na taasisi zake. Ufuatao ni uchambuzi wa baadhi ya taarifa hizo:-


### (i) Mikakati ya kuinua wachimbaji wadogo ili wachangie kikamilifu katika pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** uchimbaji mdogo wa madini umeelezwa na Sheria ya Madini Sura 123 kuwa ni ule unaofanywa na watanzania (wazawa) kupitia leseni za uchimbaji mdogo (Primary Mining License - PML). Uchimbaji huo unaratibiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ambalo lilianzishwa Mwaka 1972 ili kushiriki na kuendeleza rasilimali madini nchini kwa niaba ya Serikali.

Katika kutekeleza majukumu yake STAMICO imechukua hatua kadhaa ili kuboresha uchimbaji mdogo ikiwa ni pamoja na:- kutoa leseni za uchimbaji mdogo (PML); kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchini; wachimbaji wadogo kushirikishwa kwenye sekta ya madini kwa kupata uwakilishi kwenye Tume ya Madini na kuanzishwa kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hizo zimeleta manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kuongeza leseni za uchimbaji mdogo ambapo katika kipindi cha miaka mitano leseni zilizotolewa na tume ya madini ziliongezeka kutoka 2456 hadi 6511 kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.04.**


**Kielelezo Na: 4: Leseni za uchimbaji mdogo zilizotolewa na Tume ya Madini kuanzia mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2022/2023**




**Chanzo:** Taarifa za Wizara na Usanifu wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kutokana na mikakati ya Serikali na ushiriki madhubuti wa wachimbaji wadogo kwenye mnyororo wa thamani wa madini, mchango wa kundi hilo katika mapato yatokanayo na Sekta ya Madini nchini umekuwa ukiendelea kukua hadi kufikia **asilimia 40** katika mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na asilimia 21 mwaka 2018/19.

**Kielelezo Na: 5: Mchango wa Wachimbaji Wadogo katika Mpato yatokanayo ya Sekta ya Madini**




**Chanzo:** Taarifa za Wizara ya Madini na Usanifu wa Sekretarieti.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo wachimbaji wadogo wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo kuhusu sheria zinazosimamia Sekta ya Madini; ukosefu wa taarifa sahihi za uwepo wa mashapo katika maeneo ya uchimbaji, matumizi ya teknolojia duni katika shughuli za uchimbaji na kukosa mitaji ya kuwawezesha kuendesha shughuli zao kwa ufanisi. Serikali kupitia STAMICO imekuwa ikichukua hatua kadha wa kadha ili kutatua changamoto zinazokabili wachimbaji wadogo, jambo ambalo limeanza kuzaa matunda na kuona mchango kundi hilo ukikua katika sekta ya madini na pato la taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, ni mtazamo wa Kamati kwamba, juhudi ziongezwe katika hatua zinazochukuliwa ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za mafunzo kwa wachimbaji wadogo, kuokoa mitaji ya wachimbaji wadogo kwa kuwasaidia kupata taarifa sahihi kuhusu mashapo, na kuwapatia teknolojia ya kisasa na mitaji.

**(i) Utekelezaji wa kanuni za usimamizi wa masoko, minada ya ndani na minada ya kimataifa ya vito**

**Mheshimiwa Spika,** minada ya madini ni masoko yanayowakutanisha wamiliki wa madini (wachimbaji na wafanyabiashara) na wanunuzi kutoka maeneo mbalimbali ndani au nje ya nchi kwa lengo la kupata bei bora kwa njia ya ushindani. Maonesho ya madini na bidhaa za usonara ni soko linalowakutanisha wachimbaji, waongezaji thamani

madini, wafanyabiashara, wanunuzi, watoa huduma na wadau wengine kwa lengo la kutangaza na kufanya biashara ya madini pamoja na bidhaa za usonara. Utaratibu wa aina hii umekuwa ukitumika katika nchi za Asia hususan India na Thailand na kuingizia Serikali za nchi hizo mapato mengi yatokanayo na madini ya vito. Mathalan, nchini Thailand biashara ya madini ya vito pekee ni ya tatu katika kuchangia Pato la Taifa la nchi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** urejeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito hapa nchini unatokana na maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Wizara ya Madini kutatua changamoto zinazofanya madini ya tanzanite yasinufaishe nchi.

Madini ya Tanzanite yamekuwa hayanufaishi nchi kutokana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uwepo wa wafanyabiashara wachache, kuzuiwa biashara huria ya tanzanite, kusitishwa shughuli za uongezaji thamani, minada na maonesho ya kimataifa ya madini ya vito kama ilivyokuwa ikifanyika miaka ya 2010.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza azma ya uanzishwaji wa minada ya madini ya vito nchini changamoto kubwa ilibainika kwenye sheria na kanuni, hivyo Wizara imefanya marekebisho katika Sheria ya Madini Sura 123, Kanuni za Eneo Tengefu la Mirerani za Mwaka 2019, Kanuni za Makinikia na Biashara ya Madini za Mwaka 2018, Kanuni za Masoko ya Madini za Mwaka 2019 na Kanuni za Uongezaji Thamani Madini za Mwaka 2020 na kuanza kutumika.

**a) Kanuni za masoko ya madini za mwaka 2019**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za masoko ya Madini za mwaka 2019 zilifanyiwa marekebisho ili miongoni mwa mambo mengine, kuondoa vikwazo vya uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito nchini; kuruhusu tume ya madini ambayo ina jukumu la kuendesha minada, itafute mwendeshaji kutoka nje ya nchi mwenye uzoefu ambaye ataweza kuyafikia masoko ya kimataifa na kusimamia na kuendesha minada ya kimataifa. Waendeshaji wa nje wana uwezo wa kuendesha minada ya Kimataifa kwa tija kwa sababu ya mifumo

ya kisasa ya uendeshaji na kanzidata ya wanunuzi wakubwa duniani ambao hualikwa na hivyo kuleta ushindani na bei nzuri. Aidha, kanuni zinaelekeza wauzaji wa madini kulipa ada ya ushiriki wa minada na kulipa kamisheni kwa madini watakayouza.

Kamati inapongeza marekebisho ya kanuni yaliyoondoa zuio la wanunuzi wenye uwezo mkubwa wa kifedha kununua madini kwenye mnada endapo zabuni zao zitashinda kwa asilimia 100 na kuruhusiwa kununua asilimia 75 pekee. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, ilikuwa ni vigumu kufanya maamuzi ya utengaji wa asilimia 75 hususan kwa madini ya vito ambayo huwa na viwango vinavyotofautiana kwenye ubora.

**b) Kanuni za eneo tengefu la Mirerani za mwaka 2019**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Kanuni za Eneo tengefu la Mirerani za mwaka 2019 *maboresho yameondoa zuio* la kufanya shughuli za uongezaji thamani ya madini ya vito nje ya Eneo Tengefu la Mirerani, hivyo kuwanyima fursa wafanyabiashara wanaoongeza thamani ndani ya nchi kunufaika moja kwa moja na biashara ya madini hayo. Marekebisho ya kanuni yanaruhusu tanzanite kuuzwa nje ya Mirerani kupitia Kituo cha Uuzaji wa Pamoja (TEC), na kueongeza uwanda wa wamiliki wa leseni kubwa za uoongezaji thamani pamoja na madini ya tanzanite yanayokatwa na kusanifiwa.

Aidha, ili kuwezesha nchi yetu kuwa na akiba ya dhahabu, Kanuni ya 3 ya Makinikia na Biashara ya Madini za Mwaka 2018 imeboreshwa kwa kuongeza Kanuni ndogo ya 6 hadi ya 10 kwa kuweka utaratibu wa namna ya madini yaliyotengwa na mmiliki wa leseni ya uchimbaji au biashara ya madini kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania, kwa kiwango kisichopungua asilimia 20 ya dhahabu kwa lengo la kuwa na akiba ya dhahabu ya nchi. Utekelezaji wa kanuni hii umeanza na tayari nchi imeanza kuhifadhi dhahabu ambapo hadi Disemba 2024, kilogramu 2000 na zaidi zilikuwa zimenunuliwa na Benki Kuu.

c) **Minada ya ndani na minada ya kimataifa ya vito**

**Mheshimiwa Spika,** minada ya ndani ya madini ya vito itafanyika katika maeneo ya uzalishaji hususan Mirerani, Mahenge, Tunduru, Dar es Salaam, Arusha na Tanga na itaendeshwa na Tume ya Madini kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange – TMX) kupitia mfumo wa mauzo wa kielektroniki.

Aidha, Serikali imepanga kuanzisha minada ya kimataifa katika miji ya Zanzibar, Arusha na Dar es Salaam itakayofanyika kila robo kutokana na vivutio vingi vya utalii na miundombinu wezeshi kama hoteli na migahawa ya viwango vya juu. Vilevile, Wizara ya Madini itafanya minada ya kimataifa kati ya miji ya Bangkok – Thailand na Jaipur – India kwa lengo la kutangaza uwepo wa minada ya kimataifa nchini. Katika mwaka huu wa fedha (2024/2025), Wizara ya madini imetengewa kiasi cha Shilingi 820,000,000 katika bajeti ya maendeleo ili kugharamia shughuli zitakazowezesha utekelezaji wa minada hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** *urejeshwaji wa minada* na maonesho ya kimataifa, unatarajia kuleta manufaa mbalimbali ambayo ni pamoja na kutangaza madini ya vito yanayozalishwa nchini hususan, tanzanite kwenye masoko ya kimataifa; kuwafikishia Watanzania masoko ya kimataifa ambayo yatawahakikishia masoko ya uhakika na upatikanaji wa bei nzuri na stahiki za madini wanayozalisha na kuifungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za kiuchumi hasa ya utalii na biashara na hivyo kuingiza pato kubwa nchini.

Sambamba na mafanikio hayo, zipo changamoto kadhaa katika uendeshaji wa minada ambao ni pamoja na uhaba wa fedha za kuendesha shughuli za minada na upungufu wa miundombinu inayokidhi sifa katika majengo ya masoko ya minada. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali iendelee kutenga fedha katika bajeti ili kuwezesha uanzishwaji wa minada ya madini ya vito, sambamba na kuboresha miundombinu katika majengo ya masoko hayo ili yafikie viwango vya ubora vinavyotakiwa na hivyo kuwavutia wawekezaji jambo litakalokuwa na faida nyingi kwa nchi.

**(ii) Ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Tume ya Madini, Dodoma**

***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa jengo la Tume ya Madini ulianza kutekelezwa Januari 2021 na unahusisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) kwa ajili ya Ofisi za Tume ya Madini Makao Makuu, Dodoma. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha Watumishi wote wa Tume ya Madini Makao Makuu kuwa pamoja na hivyo kuboresha mazingira ya kazi, kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi na wadau wengine.

Mradi unatekelezwa na Mkandarasi M/s Mohammedi Builders Ltd kwa thamani ya **shilingi 6,505,035,057.97** kuanzia Februari, 2023 baada ya kuhitimisha mkataba na Mkandarasi wa awali (M/s MCB Company Ltd) na ulitarajiwa kukamilika Oktoba, 2024 baada ya mkandarasi kuomba mkataba wa nyongeza ya muda.

**Mheshimiwa Spika**, mradi haukuweza kukamilika kama ulivyopangwa kutokana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa mkandarasi amelipwa **shilingi 2,718,522,484.39** sawa na **asilimia 41.79** tu ya gharama zote, ingawa hati Na. 05 ya malipo imewasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya hatua za malipo. Kwa upande wa mkataba wa mshauri elekezi (TBA) wenye gharama ya **shilingi 141,146,880.00** hadi sasa amelipwa kiasi cha **shilingi 70,573,440.00**. sawa na asilimia 50 ya gharama yote.

**Mheshimiwa Spika,** ni mtazamo wa Kamati kwamba, mradi huu ambao utekelezaji wake umechukua muda mrefu na kugharimu pesa nyingi unapaswa kukamilika ili usiendelee kuigharimu Wizara fedha ambazo zingeweza kuelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi mingine, na pia kutoendelea kuwanyima Watumishi wa Tume fursa ya kupata mazingira mazuri ya kufanyia kazi**.**

**(iii) Ujenzi wa majengo ya ofisi za afisa madini wakazi (RMOs)**
**Mheshimiwa Spika,** ofisi ni muhimu ili kuwezesha watumishi wa Tume ya Madini kutekeleza majukumu yake katika mazingira bora, na hivyo kutoa huduma nzuri kwa wananchi na wadau wengine wa madini.

Tume ya Madini imejikita katika kuhakikisha ujenzi wa majengo ya ofisi yakiwemo ya Afisa Madini Wakazi yanapewa kipaumbele.

Hadi sasa kuna jumla ya Ofisi za Afisa Madini Wakazi 30 maeneo mbalimbali nchini na maabara moja (1). Kati ya ofisi hizo ni 18 tu ndiyo ziko kwenye majengo ya tume, tatu (3) ziko kwenye majengo binafsi na kumi (10) katika majengo ya ofisi za Serikali (10). Aidha, ofisi zenye uhaba wa majengo ni 12 ambazo ni Mahenge, Mirerani, Mbogwe, Mwanza, Manyara, Kigoma, Iringa, Songwe, Rukwa, Tanga, Dar es Salaam, Dodoma na Maabara ya Tume.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa majengo ya ofisi katika maeneo hayo ni changamoto kwani kunalazimisha watumishi kufanya kazi katika mazingira yasiyoridhisha, jambo linaloathiri usimamizi na uwajibikaji wa watumishi na hivyo kuathiri kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali ichukue hatua madhubuti ili kurekebisha changamoto ya uhaba wa majengo ya ofisi za Afisa Madini wakazi na hivyo kuwawezesha watumishi wa tume ya madini kutimiza wajibu wao kikamilifu katika mazingira bora. Aidha, ni vyema kutambua kwamba mchango wa sekta ya madini kwenye mapato ya Serikali ni mkubwa na makusanyo yanatekelezwa na RMOs, hivyo ni muhimu kuwaboreshea mazingira ya kazi ili kuwaongezea ari ya utendaji kazi.

### (iv) Mkakati wa benki kuu wa ununuzi wa dhahabu

***Mheshimiwa Spika,*** madini ya dhahabu hutumiwa na nchi nyingi duniani kama akiba *(monetary gold reserve*) na hutunzwa ndani (Benki Kuu) au nje ya nchi baada ya kukidhi viwango vya kimataifa vya 999.9 *purity*. Lengo la hatua hiyo ni kutumia dhahabu kama dhamana ya kupata mikopo, katika ulipaji wa madeni na kuilinda thamani ya fedha ya nchi. Aidha, hifadhi ya dhahabu inaweza kutumika wakati wa misukosuko ya kiuchumi inapoathiri nchi husika.
Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilipitisha Mpango wa Ununuzi wa Dhahabu Septemba, 2022 kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa fedha za kigeni nchini hususan dola ya Marekani, kuboresha akiba ya fedha za kigeni na kulinda thamani ya shilingi ya Tanzania. Mpango huo ulilenga kununua kiasi cha tani sita (6) za madini ya dhahabu kwa

mwaka 2023/2024 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo kilogramu 500 kutoka kwa wachimbaji wadogo wa madini; kilogramu 800 kutoka viwanda vya kusafisha dhahabu (refineries) na wafanyabiashara wakubwa (dealers); kilogramu 3,700 (tani 3.7) kutoka kampuni za uchimbaji mkubwa na kati wa madini; na kilogramu 1000 (tani 1) kutoka kwenye malipo ya mrabaha kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Madini, Sura 123.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mpango huu katika mwaka wa fedha 2023/2024 ulipata mafanikio duni kutokana na changamoto zilizobainika na katika kuzitatua, BOT iliwasilisha mapendekezo kadhaa katika Kikosi Kazi Maalum (Think Tank on Tax Reform) kilichoundwa na Wizara ya Fedha kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148, Sheria ya Madini Sura 123 na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania.

Baadhi ya mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye kikosi kazi kwa lengo la kuwezesha BOT kupata dhahabu ni pamoja na kupunguza; kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kiwango cha mrabaha na ada ya ukaguzi, hadi kufikia asilimia sifuri (0%) kwa madini ya dhahabu yatakayouzwa BoT na mchimbaji au mfanyabiashara wa madini; BoT kutokulipa (*exempt*) nyongeza ya mrabaha (*final royalty*) na ada ya ukaguzi kwa dhahabu itakayonunua. Nyingine ni kuoanisha (*harmonize*) Sheria ya Madini Sura 123 na Sheria ya BoT ya Mwaka 2006 ili kutambua jukumu la BoT katika ununuzi wa dhahabu, na BoT kununua dhahabu kwa bei ya soko la dunia inayotolewa na Tume ya Madini kwa siku husika bila kutoa punguzo (*discount price*) kinyume na bei elekezi zinavyoonyeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024, imeridhia kufanya marekebisho ya maeneo yaliyotajwa kikiwemo Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini Sura 123 kwa kuweka sharti la kuwataka wamiliki wa leseni za Haki Madini ya dhahabu na wafanyabiashara wakubwa wa madini ya dhahabu kutenga kiasi kisichopungua asilimia 20 cha dhahabu kwa ajili ya kuchenjuliwa, kuyeyushwa, kusafishwa na kuuzwa nchini. Marekebisho hayo yamesababisha kufanyika kwa marekebisho ya Kanuni ya 3 ya Kanuni

za Madini (Biashara ya Madini na Makinikia) za Mwaka 2018 ili kutekeleza takwa la kisheria Kifungu cha 59.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hatua hizo mpango wa ununuzi wa dhahabu umepata mafanikio makubwa ambapo katika kipindi cha miezi mitatu pekee (tarehe 01 Oktoba – 31 Disemba, 2024) tangu Tume ya Madini ilipotoa tangazo la kuwataka wachimbaji na wafanyabiashara wa dhahabu kuanza kutekeleza kifungu cha 59 cha sheria ya madini Sura 123 kinachowataka kutenga kiasi cha dhahabu kisichopungua asilimia 20 na kuiuzia BOT kupitia viwanda vya usafishaji vilivyoidhinishwa, kiasi cha kilogramu 2,323.34 (tani 2.3) za dhahabu zimenunuliwa kutoka kwa wachimbaji wadogo, wachimbaji wa kati na wafanyabiashara wa dhahabu nchini. Kiasi hicho kina thamani ya **Shilingi bilioni 472.94** kwa mujibu wa bei ya dhahabu ya soko la dunia ya tarehe 06 Januari, 2025 iliyotolewa na Tume ya Madini.

Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto ya kampuni kubwa za madini za Shanta, Buckreef, Geita Gold Mine na Twiga Minerals kushindwa kutekeleza kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini kwa madai kwamba zina mikataba ya kuuza dhahabu wanayozalisha kwa kampuni za nje ya nchi, ambayo haiwaruhusu kuuza au kusafisha dhahabu wanayozalisha kwa kampuni au viwanda visivyo na ithibati ya London Bullion Market Association (LBMA). Kamati ilifahamishwa na Serikali kwamba, BoT imeanza mazungumzo na kampuni hizo ili kuona namna bora ya utekelezaji wa sheria bila kuathiri makubalino mengine ya mauzo yaliyoingiwa na kampuni hizo.

### (v) Utendaji wa viwanda vya kusafisha dhahabu nchini

**Mheshimiwa Spika,** uanzishwaji wa viwanda vya kusafisha madini ni matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Madini ya mwaka 2009, Sheria ya Madini Sura 123 na maelekezo ya viongozi wakuu kuhusu uongezaji thamani madini hapa nchini.

Hadi sasa Tume ya Madini imefanikiwa kutoa leseni saba (7) za viwanda vya kusafisha madini nchini zenye uhai wa miaka 25. Kati ya leseni hizo, sita ni za viwanda vya kusafisha dhahabu, na leseni moja ni ya kiwanda cha kusafisha madini shaba, nikeli, na kobati kilichopo

Shinyanga. Kwa ujumla viwanda hivyo vina uwezo wa kusafisha **kilogramu 1,260** (tani 1.26) za dhahabu kwa siku kwa mgawanyo ufuatao: Geita Gold Refinery (GGR) cha Geita (Kg 600); Mwanza Precious Metal Refinery Co. Ltd cha Mwanza (Kg 480); Banju Ltd cha Dar es Salaam (Kg 75); Sab Gold Ltd cha Shinyanga (Kg 50); Eyes on Africa Ltd cha Dodoma (35) na Africa eyes Ltd cha Katoro, Geita (Kg 20).

**Mheshimiwa Spika,** ili kusaidia viwanda hivyo kupata malighafi kwa urahisi kutoka kwa wachimbaji na wafanyabiashara, Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 ilirekebisha kifungu cha 87(1) cha Sheria ya Madini kwa kupunguza mrabaha kwa madini ya dhahabu yatakayouzwa kwenye viwanda vya kusafisha dhahabu vilivyopo nchini kutoka asilimia sita (6%) hadi asilimia nne (4% ya thamani ya madini. Aidha, Kifungu cha 90A (6) cha Sheria ya Madini kilirekebishwa ili kuondoa asilimia moja (1%) ya ada ya ukaguzi kwa madini yanayouzwa kwenye viwanda hivyo.

Maboresho hayo ya sheria pamoja na elimu kwa wafanyabiashara wa madini na wachimbaji, yamewezesha viwanda hivyo kupata malighafi ya kuviwezesha kufanya kazi. Katika kipindi cha Machi – Disemba, 2024 viwanda vilipokea na kusafisha jumla ya **kilogramu 3,634.68 (tani 3.6**) za dhahabu, zenye thamani ya **Shilingi 724,962,260,122.84** na hivyo kuiwezesha Serikali kukusanya kiasi cha **shilingi 28,998,490.91** kama malipo ya mrabaha. Aidha, katika kiasi kichosafishwa na viwanda hivyo kilogramu 1,987.34 (sawa na asilimia 54.68 kilinunuliwa na Benki Kuu, na sehemu iliyobaki ilinunuliwana viwanda hivyo.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kupeleka BoT kilogramu 1,437.36 za dhahabu iliyosafishwa ili kuhifadhiwa ambapo kiwanda cha Mwanza Precious Metal Refinery kilipeleka Kilogramu 1,300.02 na Eyes of Africa Ltd. kilogramu 137.34. Aidha, kiwanda cha GGR kimetambuliwa na London Bullion Market Association (LBMA) na kutia saini ya mkataba wa ushirikiano, sambamba na kufanya mabadilishano (swapping) ya dhahabu mara mbili kwa niaba ya BOT kwenda Benki Kuu ya Uingereza (Bank of England) kwa ajili ya akiba ya dhahabu ya Taifa, ambapo kilogramu 161.61 zilihusika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya, viwanda vinakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na ukosefu wa malighafi ili kutosheleza mahitaji ya viwanda, uelewa mdogo wa wateja kuhusu kanuni na miongozo ya viwango vya kimataifa vinavyosimamia uendeshaji wa shughuli za dhahabu; na uhaba wa fedha ambao unaathiri utendaji wa viwanda. Mfano; kiwanda cha Africa Eyes Ltd kimeshindwa kufikia viwango vilovyowekwa na BOT kuhusu usafishaji, usalama na uwezo wa kujiendesha kwa miezi mitatu (3).

**vii) Mikutano na ziara za mafunzo katika sekta ya madini**

**Mheshimiwa Spika,** katika kindi cha mwaka 2024 na mwanzoni mwa mwaka 2025 Kamati ilifanya ziara mbalimbali za kimafunzo ndani na nje ya nchi. Baadhi ya ziara hizo ni iliyofanyika wilayani Ileje, mkoani Songwe na, ile iliyofanyika nchini Zambia.

**(a) Mkutano wa sita wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini, Tanzania 2024**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishiriki katika mkutano wa sita wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini uliofanyika nchini kuanzia tarehe 19 hadi 21 Novemba, 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) kwa mwaliko wa Wizara ya Madini. Mkutano huo ulikuwa na kaulimbiu isemayo **"Uongezaji Thamani Madini kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii**" na ulivutia washiriki muhimu zaidi ya 1,500 kutoka Tanzania na nchi mbalimbali duniani. Mkutano ulikuwa jukwaa muhimu kwa wadau wa madini kubadilishana uzoefu, maarifa, na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuongeza tija katika sekta ya madini, maendeleo ya taifa na uchumi kwa ujumla.

Kaulimbiu ya mkutano ilishabihiana na sera ya madini kuhusu uongezaji thamani madini ambapo madini yanayochimbwa nchini yanapaswa kuongezwa thamani nchini kabla ya kusafirishwa nje ya nchi ili kuongeza fursa za ajira katika mnyororo mzima wa thamani madini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mtazamo wa Kamati, mikutano ya aina hii ni muhimu kwa nchi yetu kwani inaongeza fursa za uwekezaji katika

Sekta ya Madini hapa nchini. Aidha, inaweka msingi thabiti wa ushirikiano baina ya wadau, kuimarisha uzalishaji wa madini, na kuhakikisha kuwa rasilimali za madini zinawanufaisha watanzania kiuchumi na kijamii.

Aidha, ni fursa kwa washiriki kujifunza kuhusu sera na mikakati mipya ya serikali, kujadili masuala ya kisheria na kiuchumi yanayohusiana na madini, na kushuhudia teknolojia mpya na ubunifu unaoweza kuleta thamani zaidi katika utafiti, uchimbaji na uongezaji thamani wa madini kupitia mawasilisho na maonesho. Hivyo, ni vyema nchi ikaendelea kuandaa na pia kushiriki katika mikutano ya aina hii duniani, na kutumia maarifa, ujuzi na teknolojia vinavyopatikana kutokana na uzoefu wa washiriki, kwa lengo la kuendelea kuchagiza maendeleo ya sekta ya madini kwa manufaa ya taifa.

**(b) Mradi wa kuzalisha makaa ya mawe Kiwira - Kabulo**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulioko Wilayani Ileje, mkoa wa Songwe unahusu leseni ya uchimbaji mkubwa wa makaa ya mawe Na. SML-233/2005 inayomilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na unatekelezwa katika maeneo matatu ambayo ni Kiwira, Kabulo na Ilima. Kamati ilifanya ziara mwezi Juni, 2024 katika maeneo mawili, Kiwira (mgodi wa chini ya ardhi) na Kabulo (mgodi wa wazi) kwa lengo la kuona na kujifunza namna shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe zinavyofanyika.

Takwimu zinaonesha kwamba, mgodi wa Kiwira una mashapo (reserve) ya makaa ya mawe **tani milioni 35**. Mgodi ulifunguliwa rasmi mwaka 1988 baada ya kujengwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Mwaka 2005 mgodi ulibinafsishwa kwa kampuni ya Tanpower Resources kwa asilimia 70, na asilimia 30 zilibaki chini ya Serikali ya Tanzania, hata hivyo uzalishaji ulifanyika kwa miaka mitatu hadi 2008 na mgodi ukasitisha uzalishaji.

Mwaka 2012 kampuni ya Tanpower Resources ilirudisha mgodi Serikali, baada ya kushindwa kutekeleza mradi kwa mujibu wa makubaliano,

na mwaka 2014 Serikali iliukabidhi mgodi huo kwa STAMICO ili kuuendeleza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mgodi wa wazi wa Kabulo utafiti uliofanyika mwaka 1988 ulibaini kwamba, eneo la Kabulo linakadiriwa kuwa na mashapo ya jumla ya **tani milioni 300**. Uzalishaji katika mgodi huu ulianza mwaka 2017 kwa njia ya uzalishaji wa wazi (open cast).

Baada ya kukadibidhiwa mgodi, STAMICO ilianza juhudi za kufufua na kuboresha maeneo mbalimbali yaliyokuwa kwenye mnyororo wa uchimbaji, uchakataji na uuzaji wa makaa ya mawe. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni ni ukarabati wa mgodi wa chini ya ardhi, nyumba za wafanyakazi, mitambo ya kuchakata makaa ya mawe, na barabara ya kilomita 7 kwenda Kabulo. Aidha, STAMICO imefanya uwekezaji wenye thamani ya **shilingi bilioni 9.253** ambao umehusisha ununuzi wa mitambo, vifaa na magari.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukarabati na uwekezaji uliofanyika, STAMICO imepata mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na ongezeko la mauzo ya makaa ya mawe kutoka **Shilingi milioni 221.34** mwaka 2017/18 hadi **shilingi bilioni 11.28** mwaka 2023/24 (huku mpango ukiwa kuzalisha **shilingi bilioni 4.17** kwa mwezi); fursa za ajira ambapo ajira za kudumu ni 25, ajira za muda mfupi 760 kwa siku kupitia wakandarasi na usafirishaji, na kazi zisizo za moja kwa moja 120. Aidha, mradi unawajibika kwa jamii kwa kutoa huduma za afya na maji bure kwa vijiji vinavyozunguka mgodi.

Aidha, STAMICO inafanya mazungumzo na Shirika la Umeme Tanzani (TANESCO) kuhusu mradi wa kuzalisha umeme Megawati 200 Kiwira kutokana na makaa ya mawe, na inakamilisha usimikaji wa mitambo ya kuzalisha mkaa mbadala ili kusaidia watu kuondokana na uharibu wa mazingira kutokana na matumizi ya kuni na uchomaji mkaa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ambayo STAMICO imeyapata kupitia uendeshaji wa mgodi huu kuna changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi. Changamoto hizo ni pamoja upungufu wa vifaa vya uchimbaji, idadi ndogo ya wafanyakazi, madeni ya zamani kiasi cha shilingi bilioni 1.52 (ikiwemo

bilioni 1.024 ambayo Serikali Kuu iliahidi kulipa) na ubovu wa miundombinu ya barabara.

Kamati inatambua na kupongeza juhudi zinazofanywa na STAMICO hasa kwa kuzingatia kwamba, mgodi huu ulikuwa ukijiendesha kwa hasara, lakini sasa umeanza kutengeneza faida. Serikali inapaswa kuendelea kuunga mkono juhudi za taasisi hii kwa kuiwezesha kwa mtaji na kupata leseni za uchimbaji katika maeneo yenye uhakika ili kuifanya ishindane na kampuni nyingine za madini.

**(c) Uongezaji thamani madini na ushirikishwaji wa jamii katika sekta ya madini, Zambia**

**Mheshimiwa Spika,** ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 12 hadi 15 Januari, 2025 kutokana na mwaliko wa Wizara ya Madini na ilihusisha wajumbe wanne (4) wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa lengo la kwenda kujifunza shughuli za uongezaji thamani madini, na namna wananchi wanavyoshirikishwa katika shughuli za madini. Wajumbe wakiwa nchini Zambia walitembelea Ofisi ya ubalozi wa Tanzania nchini Zambia na Wizara ya Migodi na Maendeleo ya Madini ya Zambia, zilizoko Lusaka. Aidha, ujumbe huo ulisafiri hadi Jimbo la Ukanda wa Shaba (copper belt province) na kutembelea Mgodi wa Shaba wa Mopani ambao ulianza uzalishaji mwaka 1933, katika Mji wa Mufulira, ili kuona shughuli za uzalishaji na uongezaji thamani madini; na Makamo Makuu ya Kampuni ya Mopani katika mji wa Kitwe kwa lengo a kufahamu namna jamii inavyorikishwa katika shughuli za sekta ya madini.

Ujumbe wa Kamati ulipata mawasilisho mbalimbali, pamoja na kutembelea kwa lengo la kuona na kujifunza mnyororo wa uongezaji thamani madini ya shaba, na jamii inavyoshirikishwa katika shughuli za sekta ya madini. Miongoni mwa mambo ambayo Wajumbe walijifunza ni pamoja na:-

i. Sekta ya madini ikisimimamiwa vyema ina mchango mkubwa katika uchumi na mapato ya nchini. Nchini Zambia sekta hiyo inachangia asilimia 17 ya pato la taifa hilo, huku mchango mkubwa ukitoka kwenye madini ya shaba;

ii. Ili nchi inufaike za raslimali madini ni vyema kuwa na makubaliano na wawekezaji kuhusu mgawanyo wa mapato kabla ya kuanza kwa shughuli za uzalishaji. Nchi ya Zambia inajadiliana na wachimbaji wakubwa wa madini ili kuanzisha utaratibu wa mgawanyo wa madini kutokana na uzalishaji halisi (***production sharing agreement***) kwa uwiano wa 35% kwa Serikali na 65% kwa mzalishaji. Mgawanyo huo unaweka ukomo wa gharama za uzalishaji ***(production costs***) kuwa 60% kwa kila mzalishaji. Kwa muktadha huo, mgawanyo wa 35:65 utafanyika kwenye 40% ya kiasi cha madini kilichozalishwa;

iii. Ni muhimu nchi kuweka utaratibu wa raslimali za madini zilizopo kunufaisha vizazi vijavyo. Nchi ya Zambia inakusudia kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Akiba ya Madini (***National Sovereign Mineral Fund***) ili kutunza mapato yatokanayo na madini kwa ajili ya vizazi vijavyo;

iv. Ni muhimu nchi ikapimwa ili kujua maeneo na kiasi cha raslimali zilizopo chini ya ardhi. Zambia imepanga kukamilisha utafiti wa kina wa kijiofizikia wa madini (***High Resolution Geophysical Survey***) ifikapo mwaka 2026, zoezi hilo lilianza mwaka 2023;

v. Uongezaji thamani madini kabla ya kuyasafirisha nje ya nchi ni muhimu kwa ajili ya kuzalisha ajira na kuongeza mapato ya nchi. Baadhi ya migodi ya shaba nchini Zambia inaongeza thamani madini hayo kwa kiwango cha 99.99, ukiwemo mgodi wa shaba wa Mopani;

vi. Uwajibikaji wa kampuni za madini kwa jamii ni muhimu ili kuziwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya uzalishaji kushiriki na kunufaika. Nchini Zambia Serikali inaweka mkazo katika ajira kwa wazawa, afya, elimu na mafunzo, na ushiriki wa wanawake katika shughuli za madini. Kwa mfano; Kampuni ya Mopani inatumia takribani Dola za Marekani milioni 20 (2% ya mapato yake) kwenye maeneo hayo, sambamba na kumiliki na kuendesha kikamilifu hospitali mbili, shule mbili (msingi na sekondari) na chuo cha ufundi. Aidha, inamiliki na kuendesha shule ya michezo (sports

academy), timu ya mpira wa miguu ya Nkana Red Devils na uwanja wa kisasa kwa timu hiyo na timu nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia ziara hiyo ujumbe wa Kamati ulipata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Balozi wa Tanzania nchini Zambia, Luteni Jenerali Mstaafu, Mathew Mkingule ambaye alitumia fursa hiyo kuwaeleza wajumbe kwamba, kutokana na uhusiano mzuri na wa muda mrefu baina ya nchini hizi, zipo fursa nyingi za kiuchumi na biashara ambazo watazanzania wanaweza kunufaika nazo nchini Zambia na kukuza uchumi wao. Ziara za kimafunzo nje ya nchi ni muhimu kwani zinachangia kuwaongezea uelewa Wabunge kuhusu mambo mbalimbali yanayofanyika katika nchi nyingine. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, ziara za aina hii zitolewe kwa Wabunge wengi zaidi ili kuendelea kuwajengea uwezo na hivyo kuwawezesha kuisimamia na kuishauri vizuri Serikali katika utendaji wake kwa manufaa ya taifa na wananchi.

**2.2** Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta za Nishati na Madini

**Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji uliofanywa na Kamati kwa Wizara inazozisimamia kwa mujibu wa Kanuni[6] umeiwezesha Kamati kubaini changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia kukwamisha lengo la nchi katika kuhakikisha ustawi wa wananchi[7]. Katika ufuatiliaji huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

**(i) Katika Sekta ya Nishati**

**2.2.1** Foleni kubwa ya magari katika kujaza gesi asilia kwenye magari; na gharama kubwa (**wastani wa shilingi milioni 2 kwa gari ndogo**) za kufunga mfumo wa gesi;

**2.2.2** Upatikanaji wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka *IMF* kupitia *ECF* hauridhishi (shilingi **Bilioni 53.2** zilizotengwa mwaka 2023/2024 na mwaka 2024/2025 mtawalia hazikutolewa);

[6] Kanuni ya 7 (1) (d) ya Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023
[7] Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

**2.2.3** TPDC ilipunguza uzalishaji wa gesi asilia kutokana na TANESCO kupunguza kiwango cha manunuzi ya gesi hiyo baada ya kuanza kuzalisha umeme wa bwawa la Julius Nyerere (JNHPP);

**2.2.4** Mahitaji ya matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya kuendeshea magari, mitambo viwandani na kupikia majumbani ni makubwa na nafuu ikilinganishwa na nishati nyingine;

**2.2.5** Nchi inazalisha umeme wa ziada kwa takribani **MW 736;**

**2.2.6** Uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha umeme, uchache wa mashine umba na vituo vya kupoza umeme vinasababisha umeme kukatika mara kwa mara au kukosa nguvu ya kutosha kwa baadhi ya maeneo;

**2.2.7** Mikoa ya Rukwa, Kagera, Katavi, Lindi na Mtwara haijaunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa;

**2.2.8** Utekelezaji wa miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa (Gridi imara) awamu ya kwanza unasuasua;

**2.2.9** Vitongoji vingi nchini havijafikiwa na huduma ya umeme;

**2.2.10** Fedha za miradi ya gridi imara zimekuwa hazitolewi kikamilifu kwa miaka miwili mfululizo na hivyo kusababisha madai ya wakandarasi kiasi cha **shilingi bilioni 570.3** mwezi Disemba, 2024;

**2.2.11** Serikali haijafanya tathmini ya matumizi ya mitungi ya gesi inayouzwa kwa bei ya ruzuku;

**2.2.12** Baadhi ya wananchi waliopewa mitungi ya gesi ya kupikia (LPG) wamekuwa wakiiuza kwa wanunuzi wa chuma chakavu;

**2.2.13** Kampuni za ETDCO na TPCM zinakabiliwa na changamoto ya mtaji kwa kuwa hazikuwezeshwa kimtaji pindi zilipoanzishwa;

**2.2.14** TPDC imekuwa ikipata zabuni ndogo za kuagiza mafuta. Mwaka 2023 ilipata zabuni moja na mwaka 2024 ilishinda zabuni moja kati ya zabuni 43;

**2.2.15** Maghala kwa ajili ya kuhifadhia mafuta hayatoshelezi mahitaji ya muda wa kati na muda mrefu;

**2.2.16** Utekelezaji wa miradi ya CSR katika sekta ya nishati kwa kutumia taratibu zinazopendekezwa na wahisani ni wa gharama kubwa;

**2.2.17** Fedha za CSR katika miradi ya gesi asilia hazikutolewa kikamilifu kwa muda mrefu (takribani miaka tisa), isipokuwa kuanzia mwaka 2023/2024; na

**2.2.18** Magari mengi yanayoingizwa nchini hayana mfumo wa kutumia gesi asilia.

**ii. Sekta ya Madini**

**2.3.1** Wachimbaji wadogo wa madini wanakabiliwa na changamoto za uelewa mdogo wa sheria, ukosefu wa taarifa sahihi za uwepo wa mashapo, teknolojia duni na ukosefu wa mitaji;

**2.3.2** Mgawanyo usio sahihi wa mitambo ya uchorongaji unaleta malalamiko na dhana ya upendeleo;

**2.3.3** Baadhi ya maeneo ya wachimbaji wa madini yanakabiliwa na ubovu wa miundombinu, mawasiliano na umeme usio na uhakika;

**2.3.4** Kanuni za usimamizi wa masoko, vituo na minada ya ndani na minada ya kimataifa ya vito zikitekelezwa kwa usahihi zitawezesha nchi kunufaika na madini ya vito;

**2.3.5** Uhaba wa majengo ya afisa madini wakazi (RMOs) katika baadhi ya maeneo unaathiri utendaji na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutokana na madini;

**2.3.6** Utekelezaji wa kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini, Sura 123 ni muhimu katika mkakati wa nchi kuwa na hifadhi ya kutosha ya dhahabu;

**2.3.7** Viwanda vya kusafisha dhahabu vilivyoanzishwa nchini vinakabiliwa na uhaba wa malighafi ya dhahabu;

**2.3.8** Wachimbaji wadogo wa madini nchini wanakabiliwa na ukosefu wa mitaji na hivyo kulazimika kutegemea mitaji ya nje;

**2.3.9** Serikali iendelee kuiwezesha STAMICO kimtaji na kiteknolojia ili iendelee kuongeza uzalishaji katika miradi yake hivyo kuongeza mapato yake na Serikali kwa ujumla.

**2.3.10** Serikali itimize ahadi ya kulipa kulipa deni la Shilingi bilioni 1.52 ambazo ni malipo ya stahiki kwa waliokuwa wafanyakazi na wazabuni wa mgodi wa makaa ya mawe Kiwira.

## SURA YA TATU

**3.0** MAONI NA MAPENDEKEZO
**3.1** Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri zilizotekelezwa na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini katika mwaka 2024, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoathiri juhudi za Wizara hizo kufikia malengo yaliyokusudiwa. Ili kutatua changamoto hizo, Kamati inayo mapendekezo yafuatayo: -

**3.2** Wizara ya Nishati

**3.2.1** Utekelezaji wa Bajeti (upatikanaji wa fedha za nje)

**KWA KUWA,** fedha za *IMF* kupitia *ECF* **shilingi Bilioni 53.2** kwa ajili ya miradi ya gridi imara, umeme vitongojini na matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na taasisi zake hazikutolewa mwaka wa fedha 2023/2024, na nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025;

**NA KWA KUWA,** kutopatikana kwa fedha hizo kumeathiri utekelezaji wa miradi ya gridi imara na umeme vitongojini na hivyo kukwamisha umeme kufikishwa katika baadhi ya maeneo, jambo ambalo limezua malalamiko ya mara kwa mara miongoni mwa wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inapata uhakika (commitment) wa upatikanaji wa fedha za *ECF* zinazotolewa na *IMF* kabla ya kuzitenga katika bajeti husika. Aidha, ifanye ufuatiliaji wa upatikanaji wa fedha zilizotengwa na kuidhinishwa katika bajeti.

**3.2.2** Hali ya usambazaji na upatikanaji wa Umeme nchini

**KWA KUWA,** hali ya usambazaji na upatikanaji wa umeme nchini siyo ya kuridhisha kutokana na uchakavu wa miundombinu, uchache wa mashine umba na vituo vya kupoza umeme, jambo linalochangia pia umeme kukatika mara mara au kukosa nguvu kwenye baadhi ya maeneo;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inaathiri shughuli za kiuchumi na kijamii na hivyo kuzua malalamiko miongoni mwa wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali itatue changamoto hizo kwa kuanza na utekelezaji wa miradi ya gridi imara ya muda mfupi itakayotatua changamoto ya kukatika umeme na umeme kukosa nguvu, katika eneo kubwa.

**3.2.3** Kusuasua kwa utolewaji wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Gridi Imara

**KWA KUWA,** katika jitihada za kutatua changamoto ya umeme wa gridi ya taifa kukatika mara kwa mara, Serikali ilianzisha mradi wa gridi imara mwaka 2022 na kutenga **shilingi Trilioni 1.97** ili kutekeleza miradi 27 ya awamu ya kwanza katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2026;

**NA KWA KUWA**, tangu kuanza utekelezaji wa mradi, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa hauridhishi, na hivyo kusababisha miradi mitano (5) tu kati ya ishirini na saba (27) kukamilika;

**NA KWA KUWA,** kutokutolewa kwa fedha hizo kumekwamisha malipo ya jumla ya **shilingi bilioni 570.53** kwa wakandarasi pamoja na fidia ya maeneo kwa wananchi waliopisha utekelezaji wa miradi hiyo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali itoe fedha zote za mradi wa gridi imara zilizobakia (**shilingi bilioni 340**) katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama ilivyoahidi wakati wa vikao vya bajeti ya mwaka 2024/2025;

(b) Serikali ikamilishe malipo ya wakandarasi na wananchi wote wanaodai mapema na kwa ukamilifu ili kuzuia ongezeko la riba ya ucheleweshaji wa malipo; na

(c) Serikali itekeleze na kumaliza ujenzi wa miradi ishirini na mbili (22) ya gridi imara iliyobakia katika awamu ya kwanza kabla ya mwezi Aprili, 2026.

**3.2.4** Umeme unaozalishwa kukosa matumizi

**KWA KUWA,** umeme unaozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali nchini umevuka kiwango cha mahitaji kwa **MW 736** na ziada hiyo itafikia **MW 1,676** baada ya mashine nne za mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kuanza uzalishaji;

**NA KWA KUWA,** licha ya kuwa na ziada hiyo, **vitongoji 30,702** havijafikishiwa umeme, baadhi ya maeneo ya migodi, viwanda, vijiji miji (peri urban) kukosa umeme wa kutosha na mikoa mitano (Rukwa, Katavi, Kagera, Lindi na Mtwara) kutounganishwa kwenye gridi ya Taifa;

**NA KWA KUWA,** uzalishaji wa umeme huo wa ziada unagharimu fedha nyingi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali iongeze kasi ya kufikisha umeme kwenye vitongoji vilivyobakia kwa kuanzia na **vitongoji 3,060** katika majimbo 204 ya uchaguzi (wastani wa vitongoji 15 kwa jimbo);

(b) Serikali ifikishe umeme kwenye maeneo yenye matumizi makubwa kama vile migodi, viwanda na maeneo ya huduma za jamii, ili kuleta thamani ya pesa kwa umeme unaozalishwa; na

(c) Serikali iunganishe kwenye gridi ya taifa mikoa ambayo haijaunganishwa.

**3.2.5** Uchache wa Maghala ya kuhifadhia Mafuta

**KWA KUWA,** mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja umevutia nchi jirani zinazotumia Bandari ya Dar es Salaam kuagiza mafuta yao kupitia mfumo huo;

**NA KWA KUWA,** uingizaji wa mafuta ya nje na ya mafuta ndani umeongezeka kwa asilimia 100, kutoka tani 300,000 (mwaka 2012) hadi tani 600,000 kwa mwezi (mwaka 2021), huku uwezo wa maghala ya kuhifadhia mafuta ukibaki ule ule;

**NA KWA KUWA**, uwezo mdogo wa maghala ya kuhifadhia mafuta unaathiri nchi jirani zinazotumia maghala hayo kwa kuzuia zisiagize mzigo mkubwa jambo ambalo pia linaikosesha nchi mapato yanayotokana na matumizi ya bandari, tozo na usafirishaji wa mafuta;

**NA KWA KUWA**, nchi yetu pia inapata hasara kwa kushindwa kuhifadhi mafuta ya kutosha kutumika kwa muda mrefu na hivyo kutonufaika na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali iongeze uwezo wa maghala ya kuhifadhi mafuta angalau kufikia **asilimia 300** ya uwezo wa maghala yaliyopo kwa sasa; na

(b) Serikali iiwezeshe TPDC kwa kuijengea mazingira wezeshi katika kuagiza mafuta nchini.

**3.2.6** Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia

**KWA KUWA,** Serikali inatekeleza mradi wa nishati safi ya kupikia kwa kugawa mitungi ya gesi ya kupikia (LPG), majiko banifu, mkaa mbadala wa makaa ya mawe kwa bei ya ruzuku na kuongeza mtandao wa bomba la gesi asilia (LNG) katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es Salaam;

**KWA KUWA,** miongoni mwa nishati safi za kupikia iliyo salama na nafuu ikilinganishwa na nishati nyingine ni gesi asilia (LNG);

**NA KWA KUWA,** sehemu kubwa ya nchi haina mtandao wa LNG, na hivyo juhudi kubwa zimeelekezwa katika ugawaji wa mitungi ya gesi ya kupikia (LPG) kwa bei ya ruzuku;

**NA KWA KUWA,** baadhi ya watu waliopewa mitungi hiyo wameshindwa kuijaza gesi na wengine kuiuza kama chuma chakavu, jambo linaloisababishia Serikali hasara na kuathiri juhudi za kufikia asilimia 80 ya mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifanye tathmini ya matumizi ya mitungi iliyotolewa kwa bei ya ruzuku ili kubaini endapo malengo ya kutolewa kwake yanatekelezwa;

(b) Serikali iongeze mtandao wa bomba la gesi asilia (LNG) kwa ajili ya kupikia kutokana na unafuu na usalama wake; na

(c) Serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya wanaouza na kununua mitungi ya gesi ya kupikia kama chuma chakavu au matumizi mengine yasiyofaa.

**3.2.7** Mahitaji ya matumizi ya gesi asilia (CNG)

**KWA KUWA,** matumizi ya gesi asilia kwenye magari, kupikia na kuendeshea mitambo viwandani ni nafuu ikilinganishwa na nishati nyingine;

**NA KWA KUWA,** kutokana na unafuu huo, mahitaji ya gesi hiyo yameendelea kuongezeka katika maeneo mbalimbali nchini;

**NA KWA KUWA,** magari mengi yanayoingizwa nchini hayana mfumo wa kutumia gesi asilia na hivyo kulazimika kuwekewa mfumo huo nchini kwa wastani wa **shilingi milioni mbili** (2,000,000) kwa gari dogo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ihamasishe uingizaji nchini wa vyombo vya moto vyenye mfumo wa kutumia gesi moja kwa moja; na

b) Serikali iongeze mtandao wa bomba la kusafirishia gesi asilia katika mikoa mingine kutokana na kuwa na manufaa makubwa ikilinganishwa na kutumia magari kusafirisha gesi hiyo.

**3.2.8** Utolewaji wa fedha za CSR katika miradi ya umeme na Gesi Asilia

**KWA KUWA,** sheria ya Petroli ya mwaka 2015 inaweka masharti yanayomtaka mmiliki wa leseni pamoja na mwekezaji katika kitalu cha gesi asilia kuandaa mpango madhubuti wa uwajibikaji kwa jamii kwa kushirikiana na Serikali za mitaa na vijiji husika ili kuwezesha kutolewa kwa CSR kulingana na mpango huo;

**NA KWA KUWA,** tangu mwaka 2014/2015 hadi mwaka 2023/24 wawekezaji katika sekta ya gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara walitoa fedha za CSR kiasi cha **shilingi Bilioni 9.3** tu, na kati ya hizo shilingi **Bilioni 5.4** zilitolewa mwaka 2023/24 pekee, hali inayoleta mashaka iwapo wawekezaji hao walikuwa wakitoa kiwango stahiki kabla ya mwaka 2023/24;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifuatilie na kufanya uhakiki wa fedha za CSR zilizotolewa na kampuni zilizowekeza kwenye miradi ya gesi asilia mkoani Lindi na Mtwara kwa mwaka 2014 hadi 2022 ili kutathmini endapo kiasi kilichotolewa kilikuwa stahiki. Aidha, iwapo itabaini kuwa kiasi kilichotolewa ni pungufu ichukue hatua stahiki kwa wawekezaji hao; na

(b) Serikali itunge kanuni ama miongozo itakayohakikisha fedha za CSR kwenye miradi ya sekta ya nishati zinatolewa kikamilifu na kwa wakati.

**3.3** Wizara ya Madini

**3.3.1** Changamoto zinazowakabili Wachimbaji wadogo wa madini

**KWA KUWA,** Wachimbaji wadogo wa madini wanakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uelewa mdogo kuhusu sheria zinazosimamia Sekta ya Madini; ukosefu wa taarifa sahihi za uwepo wa mashapo katika maeneo ya uchimbaji, matumizi ya teknolojia duni na ukosefu wa mitaji;

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zinawanyima uwezo wa kutumia fursa zilizopo katika kuendeleza shughuli za uchimbaji wa madini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itatue changamoto hizo kwa wachimbaji wadogo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi kuhusu mashapo ili kuepusha upotevu wa mitaji;

(b) Kuwapatia wachimbaji wadogo teknolojia ya kisasa ya uchimbaji madini; na

(c) Kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mitaji au ufadhili kwa ajili ya shughuli zao.

**3.3.2** Mgawanyo wa Mitambo ya uchorongaji katika maeneo ya wachimbaji wadogo

**KWA KUWA,** mitambo mitano (5) ya uchorongaji iliyonunuliwa na kuingizwa nchini na Serikali kwa lengo la kusaidia wachimbaji wadogo ni michache ikilinganishwa na uhitaji wa wachimbaji wadogo;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo ilisababisha malalamiko kutoka kwa wachimbaji wa maeneo ambayo hayakupata mgao wa mitambo na kuleta hisia kwamba kuna upendeleo kwa baadhi ya maeneo;

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe mitambo kumi (10) ambayo iliingizwa nchini mwishoni mwa mwaka 2024 inagawanywa kwa uwiano sawa katika maeneo ya wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kupata huduma ya mitambo hiyo, sambamba na kuondoa malalamiko. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza mitambo hiyo kwani uhitaji wake ni mkubwa ikilinganishwa na idadi yake.

**3.3.3** Uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya wachimbaji

**KWA KUWA**, baadhi ya maeneo ya wachimbaji wa madini yanakabiliwa na ubovu wa miundombinu, ikiwemo barabara, mawasiliano na umeme usio na uhakika (kuongezeka au kupungua nguvu);

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaathiri shughuli za uchimbaji kwa kushindwa au kusafirisha kwa gharama kubwa vifaa na mahitaji mengine, pamoja na vifaa kuungua mara kwa mara, jambo linalosababisha hasara na kukwamisha shughuli za uchimbaji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iboreshe mazingira katika maeneo ya wachimbaji kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kutengeneza miundombinu ya barabara katika maeneo ya machimbo ili kurahisisha na kupunguza gharama za usafirishaji wa vifaa na mitambo muhimu kwa ajili ya shughuli za uchimbaji;

(b) Kupeleka huduma ya umeme katika maeneo ya machimbo ili kurahisisha utendaji kazi na kuwapunguzia gharama za matumizi ya kangavuke na mafuta; na

(c) Kufunga vifaa vya dharura kama vile *automatic voltage regulator* - AVR ili kudhibiti madhara yanayosababishwa na umeme kuongezeka au kupungua nguvu.

**3.3.4** Utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa masoko na Vituo, Minada ya Ndani na Minada ya Kimataifa

**KWA KUWA,** utekelezaji wa maboresho ya Kanuni za Usimamizi wa Masoko na Vituo, Minada ya Ndani na Minada ya Kimataifa ya Vito, unasuasua kutokana na ufinyu wa bajeti na ubovu wa miundombinu ya masoko;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inaifanya nchi kuchelewa kupata manufaa ya kiuchumi yatakayotokana na uendeshaji wa minada hiyo, na wafanyabiashara kukosa sehemu ya kuuza madini yao;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze fedha zinazotengwa kwenye bajeti ya Wizara ya Madini ili kuwezesha shughuli za uendeshaji wa minada hiyo, na kuboresha miundombinu ya majengo ya masoko kwa ajili ya minada hiyo.

**3.3.5** Uhaba wa Ofisi za Afisa Madini Wakazi (RMOs)

**KWA KUWA,** Tume ya Madini inakabiliwa na ukosefu wa majengo ya ofisi kwa ajili ya afisa madini wakazi katika maeneo mengi;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inalazimisha watumishi kufanya kazi katika mazingira yasiyoridhisha na hivyo kuathiri ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutokana na madini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali iongeze bajeti ya Tume ya Madini kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi za afisa madini wakazi. Aidha, fedha hizo zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ili

kutokwamisha miradi ya ujenzi iliyopangwa kutekelezwa sambamba na kusimamia wakandarasi kwa karibu ili watimize wajibu wao.

**3.3.6** Kampuni za madini kutenga asilimia 20 ya madini ili kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

**KWA KUWA,** kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini, Sura 123 kinaweka sharti kwa wamiliki wa leseni za haki madini ya dhahabu na wafanyabiashara wakubwa wa madini ya dhahabu kutenga kiasi kisichopungua asilimia 20 cha dhahabu kwa ajili ya kuchenjuliwa, kuyeyushwa, kusafishwa na kuuzwa nchini;

**NA KWA KUWA,** kampuni kubwa za uzalishaji wa dhahabu zimeshindwa kutekeleza kifungu hicho kwa madai ya kuzuiwa na mikataba na kampuni za nje ya nchi, zisiuze au kusafisha dhahabu inayozalishwa kwa kampuni au viwanda visivyo na ithibati ya *London Bullion Market Association* (LBMA), jambo linaloathiri kiwango cha dhahabu kinachonunuliwa na BoT;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali ihakikishe majadiliano baina ya BoT na kampuni hizo yanakamilika mapema ili kampuni hizo zianze kutekeleza masharti ya kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini na hivyo kuwezesha upatikanaji wa dhahabu ya kutosha kwa BoT; na

(b) Serikali iboreshe mazingira ili kuziwezesha kampuni zenye leseni za kusafisha madini (refinery licence) kupata ithibati inayotambulika na LBMA na hivyo ziweze kuuziwa dhahabu na kampuni kubwa za uchimbaji.

**3.3.7** Viwanda vya kusafisha dhahabu kukosa malighafi

**KWA KUWA,** usimamizi na udhibiti wa biashara ya madini umeleta tija kwa kuhamasisha na kuvutia wafanyabiashara kuanzisha viwanda vya kusafisha madini hususan dhahabu;

**NA KWA KUWA,** viwanda vilivyoanzishwa vinakabiliwa na uhaba wa malighafi ya dhahabu kwa ajili ya kutosheleza uendeshaji wa shughuli za usafishaji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mazingira wezeshi yatakayovutia wachimbaji na wafanyabiashara wa madini kuuza dhahabu kwenye viwanda vya ndani vya kusafisha madini.

**3.3.8** Wachimbaji na wafanyabiashara kuwezeshwa kimtaji

**KWA KUWA,** wachimbaji wadogo wa madini nchini wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mitaji inayowawezesha kuendesha shughuli zao kwa ufanisi;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imewalazimu kutegemea mitaji kutoka nje ya nchi ambayo inaweka masharti magumu ikiwa ni pamoja na kuwauzia dhahabu wawezeshaji wa nje, jambo linalosababisha viwanda vya kusafisha dhahabu vya ndani kukosa malighafi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaanzimia kwamba, Serikali iweke mikakati ambayo itawawezesha wachimbaji wadogo wa ndani kupata mitaji kutoka taasisi za fedha za ndani, ili wawe huru kuuza dhahabu wanayozalisha kwa viwanda vya ndani, na kunufaika na unafuu wa kodi na tozo zilizopo, sambamba na kuchangia kukuza uchumi wa taifa.

**3.3.9** STAMICO kuwezeshwa kimtaji ili iongeze uzalishaji

**KWA KUWA,** uwekezaji wa STAMICO katika mradi wa makaa ya mawe Kiwira – Kabulo umeanza kuleta manufaa kiuchumi kwa kuzalisha faida baada ya kupitia katika kipindi kigumu;

**NA KWA KUWA,** katika eneo hilo kuna mashapo ya kutosha kufanya uzalishaji mkubwa zaidi na wenye manufaa iwapo changamoto za mtaji, miundombinu ya barabara, mitambo na vifaa, zitatuliwa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali iendelee kuiwezesha STAMICO kimtaji na kiteknolojia sambamba na kutatua

changamoto zilizopo ili mradi wa Kiwira – Kabulo na miradi mingine iongeze uzalishaji na hivyo kuongeza mapato ya Shirika na Serikali kwa ujumla.

**3.3.10** Deni shilingi bilioni 1.52 za waliokuwa watumishi na wazabuni wa Mgodi wa makaa ya mawe Kiwira.

**KWA KUWA,** Serikali ilihakiki na kuahidi kulipa deni la **Shilingi bilioni 1.52** lililotokana na mapunjo ya malipo ya stahili kwa waliokuwa wafanyakazi wa mgodi wa makaa ya mawe Kiwira na wazabuni waliokuwa wanatoa huduma kwenye mgodi huo;

**NA KWA KUWA,** hadi sasa Serikali haijalipa deni hilo, jambo linalosababisha wanufaika watarajiwa wa fedha hizo kuendelea kuathirika kiuchumi na wengine kupoteza maisha kabla ya kulipwa stahiki zao;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali itimize ahadi yake kwa kulipa deni husika ili waathirika wapate stahiki zao na waendelee na shughuli za kimaisha na kiuchumi.

## SURA YA NNE

**4.0** HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

**4.1** Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naendelea kukushukuru na kukupongeza wewe Spika wa Bunge letu Tukufu Mhe. Dkt Tulia Aksoni (Mb) kwa kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru  Naibu Spika, Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao na kusaidia katika kuendesha vikao vya Bunge letu.

Napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuniamini mimi pamoja na Makamu Mwenyekiti Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb) na kuendelea kutupa ushirikiano uliowezesha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati katika kipindi chote. Kwa namna ya kipekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb -Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
8. Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb
9. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb
10. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
13. Mhe. John Marko Sallu, Mb
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb
23. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Antony Peter Mavunde (Mb), Waziri wa Madini, kwa ushirikiano wao mzuri wanaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb) Naibu Waziri wa Nishati na Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) Naibu Waziri wa Madini

kwa namna wanavyowasaidia mawaziri wao katika utekelezaji wa majukumu na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Vilevile, ninamshukuru Mhandisi Felschesmi Mramba, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Yahya Ismail Samamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, pamoja na Manaibu wao kwa namna wanavyowaongoza vyema watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mzuri wanaoipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Baraka ildephonce Leonard pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ambao unaisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba.

**4.2** Hoja

**Mheshimiwa Spika,** baada ya shukrani hizo, naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA**
**BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
03 Februari, 2025

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*Hoja ilitolewa Iamuliwe*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa tunaanza uchangiaji, tunaanza na Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Mtaturu na Mheshimiwa Musukuma ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya na nguvu ya kuweza kusimama hapa leo. Nampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa taarifa yake nzuri, nami kama Mjumbe wa Kamati naanza kwa kuunga mkono Maazimio ya Kamati ambayo yapo kwenye taarifa yetu, pamoja na kuunga mkono nitachangia kwenye maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza naipongeza Serikali, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassani, kwa mkutano mkubwa uliofanyika Dar es Salaam wiki iliyopita, na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye mkutano huo. Sisi Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini tunaipongeza sana Wizara kwa maandalizi mazuri, chini yake Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko pamoja na wasaidizi wake wote kwa kufanya mkutano huo kufanikiwa kwa viwango vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nadhani tumebaki nalo kama deni ni kuhakikisha kwamba ndoto hii ya Mheshimiwa Rais inatekelezeka na Watanzania wanaona ikitekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya agenda zilizokuwepo kwenye mkutano huo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na *accessibility* ya nishati ya kutosha kwenye nchi ambazo zilihudhuria. Pili, nishati hii ipatikane kwa bei ambayo wananchi wanao uwezo ya kuinunua. Sasa yapo mambo tumefanikiwa sana kwenye nchi yetu, nami naipongeza Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, nikianza na umeme kabla ya miaka miwili iliyopita *installed capacity* yetu ilikuwa takribani *Megawatt* 2,000. Kwa taarifa ya juzi ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, tumekaribia *megawatt* 3,700, taarifa yetu ya Kamati ni ya mwaka jana nadhani imechelewa kidogo, maana yake ni kwamba *very soon* tutakuwa na *megawatts* 4,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mahitaji yetu mpaka mwezi uliyoisha tunahitaji *Megawatts* 1,900, maana yake ni kwamba katika

kipindi cha mwezi mmoja ujao tutakuwa na *installed capacity* ya *Megawatts* 4,000 lakini tutakuwa tunahitaji *Megawatts* 1,900; 2,000. Kwa ongezeko la takribani asilimia nane mpaka tisa kwa mwaka, maana yake ni kwamba tunazo *Megawatts* zina-*hang* kama 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii haina maana kwamba mahitaji ya umeme, wahitaji wanao umeme wote na kwamba kuna hiyo *surplus.* Bado nauona umeme katika nchi yetu pamoja na uwepo wake ni umeme ambao unaweza kuhesabu ni kama ni kitu cha anasa, kwa sababu unao umeme ndani, lakini huwezi kuutumia kupika chakula, kwa sababu ni gharama kubwa kupikia umeme kuliko kutumia mkaa, na ni gharama kubwa kupikia umeme kuliko kutumia gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zote ambazo zinao umeme mwingi gesi ni *second option*, umeme ndiyo wanaopikia, kwa sababu umeme kama utakuwepo mwingi na utashushwa kwa gharama nafuu, ni vizuri Watanzania wakawa na *option* ya gesi na umeme kwenye matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, juhudi hizi za Mheshimiwa Rais na Wizara nazipongeza sana, lakini tuendelee kutafuta namna ambavyo tutaufanya umeme usiendelee kuogopwa kwenye matumizi. Yaani una umeme ndani matumizi yako ni *TV* na taa peke yake, ukiupikia tu umeme unaonekana ni anasa, jambo hili haliwezi kukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nafikiri bado tunadhani kwamba kadri bei inavyokuwa kubwa ndiyo tunavyopata pesa nyingi? Naamini tukiweka watumiaji wengi wa umeme tukaweka bei ambayo wananchi wanaweza ku-*afford* ndivyo tutakavyoweza kuanza kufanya *return on investment* iwe rahisi kwa sababu tutakusanya fedha nyingi zaidi, lakini tutapunguza matumizi ya nishati ambazo tumefanya mkutano, tunaona kwamba zinaathiri mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuongeza umeme, tuendelee zaidi kuwa na juhudi za kuongeza umeme maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati. Tumezungumza kuhusu umeme wa jua, kuhusu umeme wa joto ardhi, tumezungumza kuhusu miradi mingine ya umeme wa maji kama Ruhuji na kadhalika. Naiona Serikali ikiogopa ogopa kuingia kwenye *EPC+F*, sasa kwa nini nchi nyingine zimeweza, sisi tunaogopa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni *potential investment* ambazo tukifanya leo gharama yake ni ndogo kuliko kufanya miaka 10 ijayo. Unaweza ukakwepa kufanya mradi mwingine leo kwa sababu unauona ni gharama, lakini tumeshuhudia *inflation* ya *exchange rate* inavyokwenda *after ten years* itakuwa ime-*multiply* kuwa *double price*. Kwa hiyo, nafikiri kuna vitu tunaviogopa hapa ambavyo vinaitia hasara Serikali badala ya kuipa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo la umeme naendelea kuiomba sana Serikali, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, tumefanya kazi nzuri kupeleka umeme wa *REA* kwenye vijiji, takribani mitaa yangu yote, Jimbo la Geita Mjini imepata umeme, lakini tuna shida moja. Umeme unafika kwenye mtaa, kwenye kijiji unafikia watu 20 mkandarasi anahama anasema kazi yake imeisha, halafu watu 300 wanataka umeme, hawawezi kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tume-*register* kufikia vijiji vingi, umeme lakini bado tuna tatizo la kwamba wanaopata umeme ni wachache kuliko mahitaji ya umeme. Sasa tuliuliza kwenye Kamati, hivi *REA* ikiondoka pale kwenye Kijiji, ni utaratibu gani mwingine kama *REA* unaendelea kupeleka umeme kwa bei ile ile kwa wananchi wanaotaka umeme uliofika kwenye Kijiji? Ni kama vile Serikali bado haina maandalizi. Naomba kama inawezekana jambo hili lifanyiwe kazi ili watu wanaouona umeme wautumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwenye gesi. Naipongeza Serikali, mkakati wake wa kusambaza takribani mitungi laki nne na ishirini na kitu, ni mkakati kabambe. Sisi Wabunge

tumepata mitungi ya gesi, tumeshaisambaza; shida ipo kwenye *distribution*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi unayempa mtungi wa gesi, umempa bure au umemuuzia, anakaa kilomita 50 kutoka kwenye *source* ya kununua gesi ili aende aka-*refill* hiyo gesi anahitaji shilingi 10,000/= kwenda na shilingi 10,000/= kurudi kununua mtungi wa shilingi 23,000/=, *it is uneconomical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwanza tumefanya jambo jema sana, nami naipongeza hatua hiyo, lakini tufikirie namna ya kutengeneza ruzuku ili mitungi hii iuzwe kwenye mitaa na vijiji ambako watumiaji wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri pia Wizara na Serikali kuwa na mkakati wa kufanya *follow-up* ya mitungi yake. Unaposambaza mitungi 400,000, hivi tuna uhakika gani kama mitungi laki nne inafanya kazi? *Possibly* mitungi 20,000 iko kazini. Tulipata taarifa kwenye Kamati wengine walikuwa wanakamatwa wanakwenda kupima kwenye vyuma chakavu kwa sababu amekosa kazi ya kulifanyia lile dude kule nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuweke mkakati wa kufanya *follow up*, aliyepewa mtungi, tuwe na namna ambavyo tunaweza tuka-*subsidize* matumizi yake, lakini namna ambavyo tutaendelea kuhamasisha waliopewa waendelee kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wapo tayari kutumia gesi. Wananchi wameitikia wito wa Mheshimiwa Rais, *issue* ni *accessibility* pamoja na bei. Lazima tujue Watanzania huko chini kupata shilingi 30,000/=, ni mpaka akauze gunia la mahindi. Sasa unakwenda kuuza gunia la mahindi ukanunue mtungi wa gesi wa kutumia siku 10, wakati ambapo unaweza kwenda kukata kuni za shilingi 10,000/= ukatumia miezi mitatu! Nafikiri tuangalie namna ambavyo tunaweza tukaboresha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, naipongeza Wizara ya Madini, kama nilivyosema tuko kwenye Kamati hii. Mheshimiwa Waziri

anafanya kazi yake vizuri, tulipendekeza kwamba tunataka wachimbaji wadogo wapewe maeneo ya kuchimba. Tunataka wachimbaji wadogo wapelekewe umeme ili kupunguza gharama za matumizi kule wanakosaga madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali, imeanza *follow up* kwa kwenda. Naipongeza pia Serikali kwa kubadilisha matumizi ya Kigosi na sasa imepimia wananchi maeneo leseni za kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo ninaliona pale, nadhani halijaenda sawa sawa sana, bado hata wanaouza vitalu wanauza kama wanapiga ramli kwa sababu wanauza vitalu 2,000 wakiwa hawana uhakika na eneo ambalo lipo *surveyed.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wewe Wizara unaniuzia kitalu cha madini nikikuuliza, wapi pazuri, unasema hujui, halafu unauza kile kitalu shilingi 900,000/=, na Watanzania wengi kwa sababu wanajua kwenye dhahabu kuna fedha nyingi, wamekimbia wanakwenda kununua. Wengi watanunua mashamba na sehemu za kufuga nyuki kwa sababu hata Wizara yenyewe inauza eneo ambalo halijaifanyia *survey.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nitoe ushauri kwamba watumiwe *STAMICO* na *GST* kama tulivyokubaliana hapa, tuwawezeshe. Hawa watu kabla ya kupima hivi viwanja, wawe na *assurance* ya utafiti uliofanyika pale kwa sababu vinginevyo tutakwenda kuzika fedha za watu pale. Watu watashindana, watanunua, watapewa, lakini *at the end of the day* hata anayekuuzia kiwanja, haujui kama alipokuuzia kuna madini? Sasa *this is very unfair.* Kwa nini, wewe unakwenda kuniuzia kitu ambacho unajua mimi siwezi kurudisha gharama zangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba mchakato tuliouanzisha, fedha tuliyowapa Wizara ya Madini wapewe hizo fedha wanunue hizo ndege, wapewe hizo fedha wafanye hiyo *survey* ili kuwafanya wachimbaji wasichimbe tena kwa kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, wajiandae Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Ally Mlaghila.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu ambayo amewasilisha asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti kwa kuwasilisha vizuri, na ninaunga mkono hoja ambayo tuliijadili pamoja kwenye Kamati yetu. Pili, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri ambao wamewasilisha kwenye Kamati; Waziri wa Ujenzi pamoja na Waziri wa Uchukuzi ambao tumekuwa nao kwenye Kamati na wamefanya kazi nzuri katika kipindi cha taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa na moyo wake wa kuwasaidia Watanzania katika maendeleo mbalimbali ambapo tumeona kuwa kumekuwa na nia ya kutoa fedha ambazo zinakwenda kutekeleza miradi hii. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, tumeona mambo yamebadilika katika maeneo yetu na tunaendelea kumwombea katika kazi anayoifanya kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli taarifa yetu imeeleza mambo mengi, lakini nitachangia maeneo machache ili katika kuunga mkono hoja ya Mwenyekiti ambayo ameileta hapa mbele yako. La kwanza ni kuhusu ujenzi wa barabara. Wote tunajua kwamba barabara ni nyenzo muhimu ya uchumi katika kuwasaidia wananchi kufanya shughuli zao. Barabara zikiwa nzuri na ziliboreshwa wananchi wataweza kutoa mazao yao mashambani na kuleta katika maeneo ya masoko; lakini pia kusafirisha kwenye maeneo ya ndani ya mikoa, wilaya pamoja na majimbo yetu. Kwa hiyo, barabara ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba katika kipindi cha *El-Nino* tulipata tatizo kubwa la mvua nyingi, na hata sasa

baadhi ya maeneo yetu tumeona ambavyo barabara zimeharibika, ikiwemo madaraja pamoja na barabara zimevurugika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha taarifa au katika mwaka huu wa fedha ambao tunaujadili, tulitenga kama shilingi trilioni 1.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kimsingi ni kwamba mpaka tunapokea taarifa hii, zimepokelewa shilingi bilioni 743 sawa na 44% ambayo ni pungufu ya fedha ya muda kama huu mwaka uliopita, ambapo tulipokea kwa 64%. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba kama tusipoangalia vizuri, tutaenda kumaliza mwaka wa fedha hatujapata fedha ya kutosha kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka nihimize tu kwamba ni vizuri Serikali ikatazama hili na iendelee kuleta fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi tumekuwa na changamoto ya wakandarasi kulipwa fedha. Wakandarasi hawalipwi fedha, na hivi leo tunavyoongea wakandarasi wengi hawapo *site*. Hawapo *site* kwa sababu hawana fedha za kuendesha kwenye maeneo yetu. Kumekuwa na changamoto, wanasema kwamba hawaja-*raise certificate*. Kuna baadhi ya maeneo ni visingizio tu, wamesha-*raise certificate* zipo kwenye mamlaka zetu, lakini fedha hazitoki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana walipwe fedha ili wapate nguvu ya kutekeleza miradi ambayo ipo kwenye maeneo yetu ili isije ikaathiri miradi na mwaka wa fedha ukapita na baadaye tukaingia kwenye riba ambayo kimsingi italeta gharama kubwa kwa wananchi na kwa Serikali pia. Kwa hiyo, naomba sana walipwe fedha ili barabara zetu majimboni zijengwe ili wananchi waweze kufaidika na barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi tumekuwa na kizungumkuti cha hii miradi ya *EPC+F*. Maeneo mengi ni kilomita 2,100 hivi. Barabara hizo hazijaanza, huu ni mwaka wa pili sasa umeanza lakini hakuna mkandarasi ambaye ameanza kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama huu mfumo ni mgumu, ni Serikali itoke hadharani ieleze wazi kwamba sasa mfumo huu hauwezekani, tuangalie mfumo mwingine. Kwa sababu tumekuwa na barabara nyingi zinasubiri fedha au zinasubiri mradi huu uanze ikiwemo barabara ile ya Singida - Kwa Mtoro kwenda kule Kibaya mpaka Kiberashi - Handeni barabara yenye urefu wa kilomita 460 ambayo kimsingi, mpaka leo wananchi hawajui itajengwa lini? Kwa hiyo, nilitaka nihimize eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili, ni eneo la bandari. Bandari ni kichocheo muhimu cha uchumi wa nchi yetu. Kama ambavyo tunajua kwamba bandari yetu imekaa vizuri kijiografia katika ukanda huu na inahudumia nchi zaidi ya nane. Kimsingi huko nyuma tulikuwa tunazitaja changamoto nyingi sana za bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavyongea mimi na wewe, shehena zimeongezeka baada ya dhamira ya Serikali kuwekeza katika eneo la Bandari ya Dar es Salaam. Leo Bandari ya Dar es Salaam imekuwa ni kivutio kikubwa kwa watu kuja kuleta shehena zao pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kimeboreshwa? Cha kwanza, kasi ya kupakua mizigo imeongezeka sana pale Dar es Salaam. Tani zimeongezeka kwa wastani wa 10.46% kutoka mwaka 2019/2020 ambapo tulikuwa na tani milioni 16 tu ambazo zilikuwa zinashushwa katika kipindi cha taarifa, lakini leo tunavyoongea ni tani takribani milioni 23.69 zinashushwa katika Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema tani hizo maana yake unaongelea kuongezeka kwa mapato. Ukisema hizo maana yake umeongeza wafanyakazi, wanaendelea kupata fedha. Kama haitoshi, tumeweza kuongeza pato la Taifa kutoka katika eneo hilo mapato ya *wharfage* pamoja na mapato ya bandari, kwa maana ya *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushushaji wa makasha umeongezeka ambapo sasa hivi *destination* yetu inavutia kwa watu mbalimbali katika dunia hii. Ninaamini maboresho yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha taarifa tumeambiwa kuwa wanaendelea kuboresha gati zile katika kuhakikisha kwamba tunapata muda. Muda wa kusubiri meli sasa umetoka siku 46 hadi siku saba, kitu ambacho kilikuwa hakijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee *TRC*. Tulikuwa tunasema hapa namna ya kuboresha treni yetu ya *SGR,* tumeanza vizuri, tumeona sasa kwamba kuna huduma kubwa kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, mpaka unakosa tiketi. Maana yake ni kwamba wateja wanavutiwa sana na kazi kubwa inayofanywa na Shirika letu la Reli. Ukiona hivyo, maana yake ni kwamba Serikali imewekeza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto moja ndogo, na tumewaambia *TRC* kwamba wakasimamie suala la treni kusimamasima njiani, kitu ambacho kimekuwa ni kikwazo kwa abiria wetu. Hili liangaliwe vizuri kama ni suala la hitilafu. Tumesema kwenye Kamati kwamba wale ambao wanahujumu, basi wachukuliwe hatua ili kuondokana na hitilafu ambazo zinajitokeza kutokana na watu wachache wasio na nia njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, kwa sasa tumeona tusaini ujenzi wa kile kipande cha mwisho kutoka Uvinza – Msongati - Gitega kilomita 282. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbarawa hongera sana, juzi tumeona kuwa mmesaini, mkandarasi ameingia. Sasa tunakwenda kutekeleza, mpaka tukachukue lile soko lililoko kule kwa ajili ya maeneo ya kule Burundi, ambapo ni soko kubwa sana la kubeba mizigo ya kuleta huku na kupeleka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme, kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja, kazi kubwa imefanyika. Ombi letu ni kuwa, katika muda huu mdogo uliobaki, wa kuelekea mwezi wa sita, kazi zilizobaki zimaliziwe ili tuweze kufikia malengo ambayo yamewekwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuhakikisha

kwamba tunaboresha miundombinu na uchukuzi katika nchi yetu na hatimaye wananchi wafurahie huduma ambayo inatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, nami ninaunga mkono hoja. Nawapongeza sana Mawaziri na Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Mlaghila na jiandae Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri, pamoja na Kamati nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia upande wa madini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Mavunde kwa sababu Mheshimiwa Mavunde amekuwa kwenye *industry* ya madini hata kabla ya kuwa Bungeni. Kwa hiyo, kitu anachokifanya nina imani anakielewa. Kusema ukweli hongera sana kwa sababu migogoro mingi ya wachimbaji wadogo inafikia mwisho wake kwa kuwa inapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia kwa kumteua Samamba ambaye amekuwemo kwenye hii *game* nadhani muda wote wa umri wake. Sasa nina imani kubwa sana na kazi zao wanazozifanya. Nimeona mchangiaji mmoja kwenye *clip* yake amewapigapiga sana kwenye Wizara yetu ya Madini. Ninaomba ange-*deal* na Wizara yake, kwa sababu ukisema ukweli katika hali ya kawaida kwa mchimbaji mdogo wa Tanzania kwa sasa ukichukua malalamiko 100%, 85% yanapata majibu kwa watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani angeiacha hii Wizara ikaendelea na kazi yake, tusikatishane tamaa. Kuna watu wengine walipewa Wizara humu ndani ikawa migogoro kila siku. Wawaache vijana wafanye kazi, nao ni bahati yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia pia kuhusiana na Serikali kukubaliana na wazo letu la kununua dhahabu kwenye *BoT*. Ingekuwa ni Mabunge mengine huko duniani tulitakiwa kupewa hongera wale ambao tuliileta hiyo hoja humu ndani, lakini kwa sababu pengine hii hoja ililetwa na watu wa Darasa la Saba, hamwezi kutoa hiyo hongera. Leo ninaona kabisa hata kwenye taarifa mmekubaliana nami kwamba tuliwashauri. Haya yangefanyika tangu miaka 10 nyuma tungekuwa mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hali ni nzuri na Serikali inapata *stock* kubwa sana ya dhahabu. Sasa wakati mwingine Waheshimiwa Wabunge wawe na shukurani ya kusema, "tunampongeza Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Kishimba, mlileta haya Mawazo"; nasi tukajiona ni watu katika sehemu ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikamilishe ule ununuzi wa helikopta. Ni kweli, kama alivyozungumza mwenzangu Mheshimiwa Kanyasu, tumegawa maeneo, lakini Mheshimiwa Mavunde mwaka 2024 alituambia kwamba anahitaji kupima na sisi bajeti, tukampitishia ili anunue helikopta, atoe kitu kinachoeleweka. Naye ni rafiki yangu na alinisisitiza, nami niombe leseni kule Kigosi. Mimi sijaomba kwa sababu kule tunakwenda kupewa mapori kwa sababu hajapima ila tunahisi kama waganga wa kienyeji. Hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali wameshaona mapato makubwa yanayopatikana kwa wachimbaji wadogo, na wameamua kutoa lile eneo, tumkamilishie ile helikopta na mipango yake ya kupima, atuambie kabisa, iwe pale, hata kama atapandisha bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina shida na mashamba, wala sina shida na eneo la kufuga nyuki, ila nina shida ya kuchimba, lakini naenda kuchimba kwa kubahatisha, tena kupiga ramli ya kuku? Kwa hiyo, nawaomba sana wahusika wanaonisikiliza wampatie fedha ili anunue hiyo ndege na vile vifaa ili wakamilishe upimaji, tuweze kuwa na maeneo ambayo yamepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kuhusiana na Wizara ya Ujenzi. Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, tunaenda kwenye bajeti, lakini mimi kwenye jimbo langu sijawahi kuona lami. Mheshimiwa Rais amenipa lami kilomita 20. Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wamepita, lakini pia na viongozi wote wamekwenda na ninajua fedha zimetoka, naomba tupate *advance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchina ana miezi mitatu yupo pale, nami Mbunge nimetoa mlima bure wa kokoto zote barabara nzima kwenye shamba langu. Tumekwishazungumza akaniahidi na Wachina wananisikia kule nina imani wiki mzigo utaenda wa *advance* angalau tuone sasa barabara ile inaanza kutendewa kazi, kwa sababu zile kilomita ambazo tumepewa, kilomita 20 kule kwingine kote tayari kuna wakandarasi wanarekebisha kwa ajili ya kupita barabara ya vumbi, lakini huku tumesimama, haitengenezwi kwa sababu tayari ina mkandarasi wa Kichina. Namwomba sana Mheshimiwa Ulega, atusaidie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye Wizara hii, ninazungumza siyo kwa ubaya. Mimi ni mfanyabiashara, tumeanzisha treni ya mwendokasi. Naomba sana Shirika letu lisipate hasara huko mbele ya safari; linafanya vizuri na watu wanasafiri. Sisi wote humu tumesafiri duniani. Nataka niambiwe, siyo kwa ubaya, ila kwa sababu naona wanakwenda tena kwenye *elements* za kulifelisha Shirika. Natamani kusema hata kama watu watanielewa vibaya lakini ninasema kwa nia nzuri kwa sababu ni Shirika la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniambie, wanaposafiri huko duniani treni ya mwendokasi, hebu niambiwe imeonekana wapi hiyo treni ya mwendokasi ina wahudumu wanaenda wanauliza tukupe chai, tukupe maziwa au tukupe nini? Tunaweka gharama wakati Shirika ndiyo linaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa, tunataka ajira. Utaratibu duniani kote kuna *buffet* inakaa katikati na nyuma. Tunapanda hizi treni huko duniani, lakini kila mahala kila mara tayari mmeshatengeneza *loss* ili tukifika mbele tena, mtuachie kicheche

kama cha mwendekasi! Hapana. Ni vizuri watuambie, na tutakapokuja hapa kwenye bajeti, tuambizane vizuri tunalipa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechukua treni na yenyewe tumeiweka kama ndege! Karibu kaa, wakati kuna mtu anatangaza unaingia Godegode, unaingia wapi, ipo imewekwa kwenye *system*. Ni vizuri sana mambo mengine kwa kweli tuwaeleze tu ili kama kuna madhara, lakini tumeshapeleka *message*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa kwenye Kamati ya Nishati na Madini mwaka huu ni wa kumi. Nanampongeza sana Mheshimiwa Rais. Mimi nimeanza kwenda Bwawa la Mwalimu Nyerere likiwa kichaka, kukiwa na kimondo, na mpaka mama Mheshimiwa Dkt. Samia anachukua Serikali. Kusema ukweli hongera sana mama, Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kazi aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tulikuwa tukimpiga mwenzetu aliyetoka humu ndani kwa sababu ilikuwa maneno mengi kila siku story, lakini tunampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Aliposhika Wizara hii, cha kwanza amezikwepa *TV*. Unajua *TV* zinaleta matatizo sana. Leo unasema hivi, watu wanasikiliza; kesho unasema hivi, watu wanasikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tukihoji humu tunaambiwa unampiga Mama, lakini leo hongera sana Mama Samia. Kutoka *zero* hadi mitambo nane imewashwa. Sisi tulioko kwenye Kamati tunamshukuru sana Mama Samia kwa kazi kubwa aliyoifanya, na tunamwombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mtanzania haelewi kwa nini umeme bado unakatika? Namwomba Mheshimiwa Waziri, suala la bwawa ni *almost* tumemaliza, na sasa waweke nguvu kwenye miundombinu. Tunapita humo barabarani, unakuta nguzo moja ya zege. Sisi tunaotoka vijijini kuna mito nguzo zimepita mle, ikianguka nguzo mmoja imekata mji mzima. Unakuta nguzo mbili, tatu zimebadilishwa zimewekwa za zege halafu zinazofuata zote za miti ikipiga chini ya miti inavuta ya zege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana sasa hivi tuweke nguvu kwenye miundombinu. Tusiwabadilishie bendi tena Watanzania, kwamba bendi ya bwawa imekwisha, tumerudi kwenye bendi ya miundombinu, hapana. Tutengeneze miundombinu ambayo inaleta kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati yangu, tumefanya kazi kubwa sana, na tumeona. Ni kweli kwamba tumegawa gesi vijijini, lakini hatuna ufuatiliaji. Sitaki kuamini kwamba mpaka tupeleke ruzuku. Ni kuweka mikakati. Tunakutana na mitungi kwenye viwanda vya nondo, ni kwa sababu, kweli kama alivyosema mwenzangu, mimi natoka Jimbo la Geita Vijijini; mtu ana mtungi kule Nkome kwenda Geita shilingi 10,000/=, kurudi shilingi 10,000/=, hajala. Bado ajaze gesi ilhali kuni zinauzwa fungu shilingi 5,000/=, utakwenda wapi? Halafu yanauzwa yanakwenda kusagwa bila sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kuna sheria kwenye mataruma ya reli na vifaa nyeti vya treni? Ni vizuri pia Serikali inapoamua kuingiza fedha, najua tutaweka shilingi bilioni nane, tuweke na sheria, kwamba mtungi na chochote kinachohusiana na gesi kikionekana kinauzwa kwenye viwanda vyetu vya nondo, basi sheria kali zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kuziba masikio kwenye suala la gesi. Sisi wengine tulipigwa kidogo, nami ni mtu niliyekwenda kule Dubai tulivyorudi hapa watu waliruka na helikopta kueleza maneno. Mheshimiwa Rais aliziba masikio. Tunamwombea sana kwa Mungu. Leo matunda yanatokea bandarini, hatuna tena ile kelele, na hii ndiyo kazi ya Bunge. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge, tuliziba masikio tukapitisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mlaghila, halafu Mheshimiwa Kunambi na Mheshimiwa Chaurembo wajiandae.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia kwenye mjadala huu wa Kamati zote mbili. Naunga mkono hoja za Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye Kamati ya Miundombinu, na katika hili namshukuru sana Mwenyekiti wetu akisaidiwa na Makamu wake, Mheshimiwa Anne Kilango, kwa uwasilishaji mzuri wa mawazo yetu na mawazo ambayo yalikuwa yamefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee pale alipoishia Mheshimiwa Musukuma juu ya Bandari yetu ya Dar es Salaam. Wanasema kupanga ni kuchagua, nasi Wabunge tuliamua kuangalia lililo na faida badala ya kuangalia yale maneno ya mtaani. Katika hili, nami naomba nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba aliamua na aliamini katika yale ambayo Serikali, viongozi wetu na Mawaziri wetu walimshauri kwamba uwekezaji kwenye Bandari ya Dar es Salaam ulikuwa ni lazima na matunda yake sasa tumeanza kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba niwashukuru sana Mawaziri wetu, Waziri Mheshimiwa *Prof*. Mbarawa na Waziri Mwakiposa. Kazi mnayofanya ni kubwa, leo tunapata matunda haya kwa sababu mlikubali kutoa *sacrifice* ya maisha yenu na kutukanwa, na kwa vyovyote vile mliendelea kutushauri na Bunge hili liliwasikia na katika hili Bunge tunatakiwa tuendelee kujipongeza kwamba tumepiga hatua kubwa sana kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna jambo ambalo linaendelea pale bandarini, *wharfage* yote ambayo inakusanywa inaenda *TPA* moja kwa moja. Tulikuwa tumeshauri kutoka kwenye Kamati na matunda yake yameanza kupatikana. Leo hii tunavyoongea, bandari yetu pale Ziwa Nyasa kule chini *Mbamba Bay* inajengwa kwa kupitia pesa hizi na hii Bandari itakuwa na manufaa makubwa sana. Haya ndiyo matunda ya Kamati hii na Bunge hili kushauri vizuri Serikali. Katika hili bado tuendelee kujipongeza na tushukuru kwa watendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kuwashukuru Serikali na Mawaziri wetu wa Miundombinu na Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Ulega na Ndugu yetu Mheshimiwa Kasekenya. Hata hivyo tunaposhukuru, bado pia tuendelee kuishauri Serikali. Tuna jambo ambalo linasumbua sana ambalo ni jambo la fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu huko wanahangaika na fidia na wamesimamisha maeneo yote ambayo walikuwa wanafanyia kazi kwa kusubiri kwamba watafidiwa halafu waondoke. Mimi nilikuwa nashauri jambo moja; kama Serikali haijajipanga kutumia maeneo hayo, tuwaachie wananchi waendelee kufanya kazi kuliko kuwasimamisha moja kwa moja. Kama hatutawaachia, basi naomba Serikali ikalipe fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza tuna barabara ya Ibanda, *Itungi Port,* Buloma kwenda *Kiwira Port* ambayo najua tutakwenda kusaini mkataba sasa hivi kwa mujibu wa Serikali, lakini wananchi wanadai fidia ya shilingi bilioni 1.76. Nataka niwaambie Serikali, tunapozidi kuchukua muda bila kulipa hizi fidia, matokeo yake tunaanza kuongeza pesa nyingine ambazo watalipwa watendaji watakaoenda kufanya tathmini tena upya. Kwa sababu ikipita, tunaenda kufanya tathmini upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwalipe wananchi wanaopita barabara hiyo, watu wa Kajunjumele na Makaburi yao ya shilingi milioni 21 tu. Naomba Serikali izilipe na sehemu nyingine ambazo ina uwezo wa kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuishukuru Serikali. Serikali imeendelea kufanya kazi kubwa, lakini bado tuna tatizo kubwa la wakandarasi wazawa kutopewa kipaumbele kwenye miradi. Tumekuwa tukiimba sana juu ya wakandarasi wazawa kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nchi zote zilizoendelea, mfano mmojawapo ni Malaysia, fedha yao ya Serikali waliwapa wazawa wafanyie kazi, fedha hiyo ikawa inazunguka ndani. Kwa hiyo, mzunguko wa pesa ukawa ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi fedha nyingi tunazitoa nje na wenzetu wanalipwa kwa dola, wanalipwa nje. Naiomba sana Serikali iendelee kutilia mkazo wakandarasi wa ndani wapewe kipaumbele, lakini hata wakipewa kazi, walipwe kazi zao mapema na haraka iwezekanavyo ili tusiwaue. Maana safari hii wapo wakandarasi ambao wameshindwa kufanya kazi kwa sababu hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishukuru tena Serikali. Mimi kule kwangu Kyela tumejenga daraja, lilikuwepo daraja la mbao, sasa hivi tumebadilisha limekuwa la chuma. Naendelea kushukuru, lakini naendelea kuomba. Barabara zetu Kyela zinasombwa na mafuriko kila mwaka. Matokeo yake ni kwamba yanatokea badala ya kuwa barabara, yanakuwa ni mashimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza, tuna barabara ya muhimu sana ambayo inatoka Ipyana kwenda Ikoro kuelekea mpaka Katumbasongwe, ni mashimo. Naomba Serikali ipeleke pesa tuitengeneze hii barabara ili iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo juu ya ubovu wa mawasiliano na mawasiliano ambayo hayapo *stable* hasa kwenye mitandao yetu ya simu. Nimekuwa nikizungumza hapa mara nyingi kwamba tuna tatizo kubwa sana tunaposafiri na tunapotembea kwamba sehemu nyingi kunakuwa hakuna mtandao na siyo kwamba hakuna mtandao, sehemu nyingine ni kwamba mtandao upo, lakini unaposhuka tu mlima mawasiliano yanakatika hata kama ulikuwa unaongea na simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, wenzetu wanaohusika na mawasiliano, ndugu yetu Mheshimiwa Silaa na dada yetu Mheshimiwa Mahundi naomba mfuatilie ubora huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu kwenye *vertical modulations* kuna tatizo, tunapigwa. Wenzetu wamepeleka tu *horizontal modulation,* lakini kwenye *vertical modulation* hawajaweka nguvu, ndiyo maana mawasiliano yanakatika. Pia, jambo la wizi wa mtandaoni naomba nalo tuendelee kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* tunaomba sana *TGFA* iwape ndege *ATCL* moja kwa moja, tutakuwa na faida kubwa sana kwa kufanya hivyo. Moja, tutaweka mizania sawa na ambayo itakuwa vizuri ya hesabu za *ATCL*. Pia, tutawapa uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi maana watakuwa na uwezo wa kukopa na kuajiri marubani na kuwalipa vizuri. Sasa hivi kuna tatizo kidogo kwenye malipo ya marubani. Naomba sana tulifanyie kazi hili ili liongeze kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lolote lile litakalohusu nchi yetu na Serikali, halitahusisha ndege zetu tukipeleka kule. Kwa hiyo, naomba tuwapelekee ndege zote ziwe chini ya *ATCL* ili Shirika lifanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba *SGR*, treni zinaposafiri hebu tufanye mpango mabadilishano yawe yanafanyika kwenye vituo vikubwa. Haiwezekani leo tunawasimamisha watu porini halafu tunasema eti tunasubiri treni lingine lipite. Duniani kote, mabadilishano ya treni hayasimami porini, tunaenda kwenye vituo ndiko tunapobadilisha treni nyingine inapopita na kupishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kunambi, wajiandae Mheshimiwa Chaurembo, Mheshimiwa Asenga na Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali anayoiongoza kwenye Sekta ya Miundombinu. Leo hii nitazungumzia jambo kubwa kwenye eneo la barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi na ninadhani nitaungwa mkono katika hili. Yapo mambo yanayoweza kusubiri, lakini siyo barabara. Usafiri wa anga ni muhimu, lakini barabara haihitaji usafiri wa anga, ila usafiri wa anga unahitaji barabara. Usafiri wa reli ni

muhimu, lakini reli inahitaji barabara ila barabara haihitaji reli. Ili msafiri afike kwenye reli inabidi atumie barabara kufika kwenye reli. Kwa hiyo, reli inahitaji barabara, lakini barabara haihitaji reli. Vilevile usafiri wa maji unahitaji barabara, lakini barabara haihitaji usafiri wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini hapa? Kama kuna mambo hayahitaji kusubiri, ni usafiri wa barabara nchini. Leo nitazungumzia barabara moja ya kitaifa, barabara inayounganisha mikoa ya Pwani na Nyanda za Juu Kusini, barabara hii ni *Trunk Road*. Barabara ya kitaifa inayotoka Dar es Salaam inapokea Mkoa wa Pwani inakwenda Tanga inarudi tena Mkoa wa Pwani, inakuja Morogoro inakwenda katika eneo la Mikumi Morogoro, inakwenda Ifakara, inapita Mlimba, inakwenda Masagaki pale, inakwenda Kibena kwa maana inakwenda hapa Taweta - Masagati, inakwenda Lupembe mpakani na Mlimba mwisho inakwenda *Kibena Junction* pale Njombe; na ikitoka pale inakwenda Ruvuma, ikitoka pale inaenda Mbeya, Mbeya itakwenda Rukwa, hatimaye Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sizungumzii barabara ya mkoa na mkoa, sizungumzii barabara ya wilaya na wilaya, ninazungumzia barabara inayounganisha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Vipande vyote nilivyovitaja, tunamshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla, mpaka Ifakara sasa ni lami, lakini ukitoka Ifakara kuitafuta Mlimba, uende uitafute Madeke mpakani mwa Njombe na Mkoa wa Morogoro ni vumbi, tena siyo vumbi, kuna wakati inakata mawasiliano (hakuna mawasiliano).

Mheshimiwa Naibu Spika, sizungumzii barabara ya wilaya na wilaya, ninazungumzia barabara ya kitaifa ambayo kimsingi *TANROADS* ndiyo jukumu lao la msingi, la kwanza mengine hayo yote ya ziada. Walipaswa kuunganisha kwanza nyanda, kwa maana ya kanda na kanda, waje mikoa halafu waunganishe wilaya. Imesahaulika barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa dhati kabisa. Kwa kipindi kirefu kama Mbunge, jukumu langu lilikuwa ni kujenga hoja kuishawishi Serikali. Kazi hiyo nimeifanya, namshukuru tena Mheshimiwa Rais, alisikia kilio changu kupitia Serikali yake,

wakatangaza zabuni. Barabara hii kutoka Ifakara - Mlimba mpaka Madeke, ina urefu wa kilometa 223. Mheshimiwa Rais kwa utashi wake akasikiliza hoja zangu, mwakilishi wa wananchi wa Mlimba akakubali, akaelekeza watu wa ujenzi watangaze zabuni kipande cha kilometa 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, toka Ifakara - Mbingu Kilometa 62.5, mkandarasi *(Highway Engineering Group)* amesaini mkataba tarehe 24 Agosti, 2023, yapata mwaka mmoja na miezi nane. Mkandarasi huyu amefanya jitihada, ameweka mitambo yake *site,* lakini mwaka mmoja na miezi nane kazi haijaanza (barabara ya kitaifa). Ukimuuliza mkandarasi anasema, sijalipwa *advance payment* na anadai shilingi bilioni tisa tu aanze kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sidhani kama maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanatekelezwa ipasavyo. Haya nataka tu wananchi wa Mlimba wasikie na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, mkandarasi wa pili *China First Group Company,* yeye ana kipande cha Mbingu - Chita kilometa 37.5 amesaini mkataba tarehe 28 Januari, 2024 yapata mwaka mmoja hajaanza kazi, hata *mobilization* hajafanya. Nimefanya jitihada kubwa kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha, ninaahidiwa kama Mbunge, nimekuwa nikipewa ahadi na nimeendelea kuishi kwa matumaini na nimeendelea kuwaambia wananchi wangu tuishi kwa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwenye barabara hii, kwenye kipande chenye wakandarasi kama *TANROADS* hawajachukua jitihada mahususi na za dharura kuikarabati. Maana yake inaenda kukata mawasiliano na wananchi wangu wa Mlimba watakosa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Ulega, nampongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya ujenzi, hongera sana. Ameanza vizuri, nimeona jitihada zake *(all starts well, ends well my brother)*. Nampa heshima kubwa. Ila

naomba jambo moja kaka, umefanya ziara pia na Morogoro, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jambo lingine kwa Mheshimiwa Waziri, ikipendeza kwa kuwa tunakwenda kwenye mvua za masika sasa, anipe kibali Mbunge wa Mlimba nikodi mitambo maeneo yote korofi ambayo Serikali imeshindwa, nikakarabati, wananchi wangu wapate huduma ya mawasiliano. Kama nitapata kibali, sawa, nitafanya hiyo kwa kushirikiana na wananchi wangu wa Mlimba ili tuweze kupita. La sivyo, hatutakuwa na mawasiliano kwa kuwa tunategemea reli ya *TAZARA* ambayo kimsingi ina miundombinu yote chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha reli, Mlimba itakuwa kisiwa. Nataka kusema nini? Kwa kuhitimisha, nimeelezea suala la Barabara. Nadhani Waziri atazungumza, kwani ni mtu muungwana sana. katika hili naomba anisaidie mdogo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu reli ya *TAZARA*. Nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa utashi wa kisiasa baina yake na Rais wa Zambia kwa kuwa na utashi wa makusudi kufanya ukarabati wa reli hii. Wachina wamepewa kazi hii, lakini watachukua miaka takribani mitatu. Tunaomba sisi wananchi wa Mlimba tunaitumia sana hii reli ya *TAZARA*. Sasa hivi treni imekuwa bahati nasibu, kuna wakati haisafiri, watu wanakaa siku tatu wapo kwenye treni njiani hawasafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali wakati tunamsubiri huyu Mchina kuanza ukarabati na maboresho ya ile reli, basi kwa kipindi hiki wapeleke fedha *TAZARA* zifanye ukarabati wa mabehewa, ifanye ukarabati wa hata ile reli angalau ipitike na vile vichwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vichwa wanatumia teknolojia ya zamani sana, *DMTU* na *DFH*. *DFH* ni kichwa kilichotengenezwa na Mjerumani tangu enzi hizo; na *MTU* ni Mchina. Wenzetu wameshaondoka kwenye teknolojia hiyo. Kwa hiyo, vile vichwa kwa sasa vimechoka, injini zimechoka, ikifika kwenye mlima kidogo zinarudi nyuma. Hii reli ya *TAZARA* ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Inaunganisha Tanzania na nchi za *SADC*. Leo hii shaba inatoka Lubumbashi *Congo DRC*, shaba inatoka Katanga, Zambia inapita kwenye reli ya *TAZARA* inakwenda kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri jitihada zinazofanywa na Serikali kwenye reli hii ya *SGR* hali kadhalika zifanyike pia kwenye reli ya *TAZARA*. Hii itatusaidia katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema, nirejee kusema, Waziri nisaidie, tukitoka hapa nipe kibali niwe *standby,* nitakodi mitambo kwa sababu mvua zikinyesha, barabara zikikata mawasiliano, mimi Mbunge wa Mlimba nichukue jitihada pale ambapo Serikali mmeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chaurembo, wajiandae Mheshimiwa Asenga na Mheshimiwa Sigula.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunitia afya na leo kuweza kutoa mchango wangu katika mjadala unaoendelea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi; na tatu nampongeza sana Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Miundombinu kwa weledi mkubwa na uwasilishaji mkubwa mzuri alioufanya leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa aliyoifanya kiasi kwamba ukisikiliza ripoti yetu ya Kamati katika kila sekta yapo mambo ambayo yamefanyika na kwa kweli niendelee pia kuwapongeza Mawaziri wote ambao wanaripoti kwenye Kamati yetu, wamefanya kazi kubwa na kazi nzuri ambayo imeenda kutoa faraja kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti yetu yapo mambo mengi ambayo tumeyazungumza. Naomba mambo yale Serikali iende ikayafanyie kazi kwa sababu ukitazama taarifa ya mwaka uliopita yapo mambo ambayo tumeyajadili na tuliiomba Serikali iende ikafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo ambalo tulilijadili na tuliomba Serikali ikalifanyie kazi katika taarifa ya mwaka uliopita, lilikuwa linahusiana na Shirika la Posta, kuhusiana na deni. Ripoti yetu hapa leo imeonesha Shirika la Posta kwa sasa linadaiwa shilingi bilioni 54.7, hivyo, kushindwa kujiendeleza na pia Shirika limeshindwa kukopesheka.

Mheshimwia Spika, naiomba sana Serikali, kama ripoti yetu ilivyoeleza, tunaiomba Serikali ilichukue deni hili ili Shirika hili la Posta liweze sasa kukopesheka. Ukiangalia *asset* walizokuwanazo, Shirika la Posta, kukosekana kwa hili deni, basi shirika lingekuwa na uwezo mkubwa wa kukopesheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti yetu ya mwaka uliopita, tulizungumza suala la *TBA*, kuhusiana na madeni ambayo yamekuwa yakizidai taasisi pamoja na wafanyakazi mbalimbali wa Serikali. Kwa sasa shirika linadai shilingi bilioni 900.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa shirika linadai Shilingi bilioni 900, ambazo ni fedha nyingi sana. Shirika likipata fedha hizi, litaenda kukarabati majengo mbalimbali ambayo kwa sasa yamechakaa. Hata hivyo, litaenda kujenga nyumba ambazo zimekuwa zikihitajika na watumishi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia taasisi hizo, naomba sasa nizungumzie suala zima la ujenzi wa barabara. Wachangiaji waliopita wamezungumzia umuhimu wa barabara kwa kiasi kikubwa sana. Kama tunavyofahamu, bajeti tunayoendelea nayo, Bunge liliidhinisha shilingi trilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa barabara mbalimbali, lakini kwa mujibu wa taarifa yetu tuliyowasilisha hapa ni 47% tu ndiyo pesa ambazo zimepokelewa. Hii inaonesha ni

jinsi gani, katika muda huu uliobaki uwezekano wa kumaliza ile miradi iliyotengewa fedha, unakuwa una tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uletaji wa fedha hizi, lakini yapo mambo ya msingi ambayo yamekuwa yakikwamisha barabara hizi zisiweze kutengenezwa kwa wakati. Moja ya mambo hayo ni fidia ya maeneo ambayo yametwaliwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Taarifa yetu inaeleza, zaidi ya shilingi trilioni 5.5 zinadaiwa katika ulipaji wa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isipolipa fedha hizi kwa wakati, maana yake kila mwaka deni hili litaongezeka, na ndiyo sababu kubwa ya barabara haziwezi kutengenezwa, kwa sababu hauwezi kutengeneza barabara katika eneo ambalo halijalipiwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati fulani tunaweza tukawa tunaona barabara haijatengenezwa, fedha hazijapelekwa, lakini kumbe sababu kubwa, huwezi ukapeleka fedha za ujenzi wakati fidia haijalipwa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tuangalie namna ambavyo tunaenda kulipa fidia kwenye sehemu zote ambazo tume-*commit* fedha za ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza na ninaipongeza Serikali kwa ujumla, ile barabara ambayo nilikuwa nikiipigia kelele miaka yote ya kutoka Kokoto – Kongowe mpaka Mwandege, tunakushukuru sana kwa sababu mmeenda kulipa fidia ya zaidi ya shilingi bilioni 16. Kwa hiyo, sasa nina uhakika barabara ile itaenda kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo naomba sana tuizingatie ni kupeleka *advance* kwa wakandarasi wetu. Barabara nyingi zina wakandarasi, lakini ujenzi umekuwa haufanyiki kwa sababu *advance* hazijapelekwa. Nina ushauri ambao nataka niutoe katika Bunge hili. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba mnisikilize vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana *TANROADS,* wamefanya ubunifu mzuri sana, ukitoka Ikwiriri kwenda Somanga, madaraja yaliyokatika pale, kama tungesema tupeleke fedha kwa

ajili ya ukarabati wa dharura kwa ajili ya kuyatengeneza kitaalamu, tungechukua zaidi ya mwaka mzima kutatua tatizo lile. *TANROADS* wamechukua makontena ya *40 feet, 20 feet* wameweka pale katika yale madaraja yaliyokatika na wakafanya *back fill*. Magari ya zaidi ya tani 60 yanapita pale juu na barabara zimefanyiwa ukarabati wa dharura kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mbinu hii iliyotumiwa na *TANROADS* katika eneo lile, iangaliwe kwa udharura huu na masika haya yanayokuja ili itumike katika madaraja yote yaliyokatika nchi nzima. Tukiweka teknolojia ile, ninasema ni teknolojia kwa sababu mpaka leo inasaidia wakazi wa maeneo yale. Tukiyatumia hayo, maana yake tutapunguza gharama na barabara zitaendelea kupitika katika masika haya yanayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingi zimekatika madaraja na bado hayajafanyiwa ukarabati kwa sasa. Naomba tuwasiliane na *TANROADS* ili zile barabara iwe ni za *TARURA* au za taasisi nyingine, tuweze kutumia makontena kuweza ku-*rescue situation* iliyopo kwa sasa. Ukiangalia bei ya kontena moja sasa hivi, haiwezi kuzidi shilingi milioni 10. Kwa upana wa barabara ukiweka makontena mawili kwa shilingi milioni 20, unakuwa umeenda ku-*save* barabara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule katika Jimbo langu la Mbagala nina Daraja lile la Maji ya Chai, limekatika kwa zaidi ya miezi sita sasa. Wananchi hawana mawasiliano, wanazunguka zaidi ya kilometa 15 kufika sehemu ambayo unaweza kwenda kwa dakika 20. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali wapeleke kontena pale. Nikipelekewa makontena matatu ya *40 feet* pale nitakuwa nimemaliza tatizo lile kwa thamani ya shilingi milioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abubakari Asenga. Mheshimiwa Sigula na Mheshimiwa Mariki mjiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na ni saada na sudi kusimama mbele

yako kuchangia kuunga mkono hoja ya Kamati yetu ya Bunge ya Miundombinu ambayo Mwenyekiti wetu Profesa wa Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Kakoso amewasilisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema, nami niko pamoja ninalandana nao katika kuunga mkono hoja hii, kwamba, Kamati yetu ya Miundombinu katika Wizara tunazozisimamia, zinatoa mchango mkubwa sana katika nchi yetu kwa maana ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Hizi ni Wizara muhimu kweli kweli na sisi mara kadhaa tumepata nafasi ya kutembelea katika miradi mbalimbali inayoendelezwa na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana watu wakawa wamesahau, tangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaapa, watu walikuwa na mashaka na kwisha kwa miradi ile mikubwa iliyokuwa imeanza, lakini leo miradi ile imekamilika na inaonekana kama siyo *story* wala siyo jambo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu, nataka nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwa ujumla na Waheshimiwa Mawaziri wake wote wanaomsaidia katika kufanya kazi hiyo kubwa. Tumeona sasa tunakuja Dodoma kwa *SGR,* Daraja la Kigongo – Busisi limekamilika na miradi mingi mingi ambayo tumeiona inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Kamati yetu tunafuatilia mambo yale ya miundombinu na kwa haraka haraka yanayotugusa ni mambo ya minara ya simu, barabara kuu kwa maana ya *TANROADS*, viwanja vya ndege, *TBA*, Mambo ya Reli ya *SGR* na juzi tumeona kwamba tumesaini shilingi trilioni tano kwa ajili ya hii reli ya kwenda Burundi, mambo ya bandari na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema sana hapa kuhusu bandari, nami nataka kurudia kidogo kwa sababu sasa hivi imekuwa siyo ajenda. Hapa kuna funzo la kujifunza kwamba Serikali yetu na viongozi wetu wanapokuwa na maono wakiamua kuyasimamia, tuwaunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ile vita ya kwamba nchi hii imeuza bandari za nchi nzima, haipo tena. Kwa sababu ilivujishwa hapa, tulizodolewa, maneno yalikuwa mengi na *propaganda*, leo imekuwa kimya. Mheshimiwa Mtaturu amesema hapa, *DP World* imeongeza mapato pale. Leo tunajenga bandari yetu ya makaa ya mawe kule Mgagao. Mheshimiwa Ali amesema kule Nyasa wanajenga bandari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusisitiza, tunajifunza funzo kubwa kwamba, kwenye haya mambo ya msingi tusikubali hata siku moja kuweka siasa za kuwavunja nguvu viongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais na tunamsisitiza awe na kifua kikubwa na moyo mkubwa kwani kazi ya maendeleo ni endelevu na kuongoza binadamu kuna changamoto zake. Mwenyezi Mungu amjaalie awe na moyo mkubwa kwamba, ndiyo kunakucha sasa hivi, mkoko ndiyo kwanza unaalika maua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumpongeza Mheshimiwa Rais, ninazungumza kwa utaratibu kabisa kwa chata na tamwa, wala siyo kwa chonda na kibuhuti kwamba Mheshimiwa Rais Samia ni Rais wa mfano. Tutarudia kulisema hilo mara kwa mara kwa sababu kuna watu ambao, hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu inawakera na sijui wanataka tumpongeze nani badala ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano katika miundombinu, nimelalamika hapa miaka miwili mitatu barabara yangu ya Ifakara – Kidatu haijakamilika, leo ninazungumza barabara imekamilika. Nimezungumza hapa kuhusu reli yangu ya Kidatu – Ifakara kufufuliwa kwa maana ya Kidatu – Kilosa, pesa zimetengwa na reli iko kwenye mchakato wa kufufuliwa. Kwa nini nisimshukuru Mheshimiwa Rais wa nchi yangu kwa kazi kubwa anayoifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema, maendeleo ni mchakato endelevu. Changamoto haziwezi kwisha, nami nataka kuzishauri Wizara zote zinazohusika na Kamati ya Miundombinu, suala la fidia

kwa wananchi wetu walitazame vizuri. Kwa sababu haiwezekani miaka mitano, mwananchi amepisha eneo limepimwa, ameambiwa asiendeleze, ameacha bila kuendeleza; kama wananchi wangu wa Mbasa, Msalabani, Katindiuka katika Barabara ya Mchepuko wa Ifakala, halafu anaambiwa hatakuja kulipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati tumelisema na hapa nataka kusisitiza, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri, Abdallah Ulega atusaidie. Yale maeneo ambayo wananchi wamesubiri fidia kwa muda mrefu, mwone namna ya kuwapa hii fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii Barabara yangu ya Ifaraka – Kidatu, bahati nzuri, jana Mheshimiwa *DC*, Dunstan Kyobya ameniambia kuna Kamati ya Mkoa ilipita na imeshafanya upembuzi. Kuna watu wanaodai kwa haki, basi wapewe stahiki zao ili kuondoa kero nchi nzima kwa wananchi wale wanaopisha fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye ujenzi, Mheshimiwa Waziri yuko hapa na nimeambiwa yeye ni mbui, hata zile sehemu zenye ukame akifika mvua inanyesha. Nimesikia taarifa zake kule kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka, umefika na neema kidogo kwa wakandarasi imeanza. Tunaiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, akusaidie zaidi pesa, wakandarasi wanalalamika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Barabara yangu ya Ifakara – Kidatu ambayo Mheshimiwa Rais alienda kuizindua, yule mkandarasi alikuwa hajamaliza baadhi ya viporo, makaravati na sehemu chache chache, miezi sita iliyopita *Railroad Construction* amesimama kwa sababu amekosa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi amerudi, amesema amepewa fedha kidogo na asipoendelea kupewa fedha atashindwa kuikamilisha barabara hii. Naomba sehemu ambayo Mheshimiwa Rais anapita, ni vizuri tukaacha makandokando ili ionekane kwamba kiongozi wa nchi amepita na vitu vimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Ulega alifika pale Mang'ula Kona na alizungumza kwenye Kamati jambo la Mang'ula Kona na jana nilikuwa pale, umeniahidi nami nina imani na wewe. Mheshimiwa Kunambi amesema kwamba tutapita kule, tutaenda na utaenda mpaka kuiona Barabara ya Ifakara – Mlimba ili utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, kwamba watu wa Ifakara kwenda Mlimba wanapata taabu kubwa sana. Ukitoka tu palepale Ifakara kilometa tatu tu ukivuka Daraja la Lumemo, mbele kuna mashimo ambayo kwa kweli hali ni ngumu. Sisi Morogoro tunaongoza kwa kilimo cha sukari ya miwa, tunalima miwa, tunazalisha sukari na tunaongoza kwa kulima mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulikuja mwenyewe pale kwenye kiwanda cha sukari, umeona. Sasa hivi bila miundombinu kwa mfano kule Malinyi, Ulanga na Mlimba, wasipofikisha mchele au mpunga, Ifakara uchumi wetu kwa kweli unasita. Kwa hiyo, tunaomba barabara hizo zifunguliwe ili Mkoa wa Morogoro ufunguliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara inayopita Ifakara kwenda Ulanga – Lindi, tuna barabara inayopita Ifakara kwenda Malinyi – Ruvuma, tuna barabara inayopita Ifakara kwenda Mlimba – Njombe, amesema Mheshimiwa Kunambi hizi ni barabara za msingi sana. Hivyo, Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku nikimalizia, ninaenda kwenye Wizara ya Mawasiliano. Mheshimiwa Jerry, tunakushukuru sana kwa mambo ya minara ya simu, na tunaomba zile vurugu zilizokuwa Wizara ya Ardhi uzihamishie huku kwenye minara. Sisi tumepewa minara mitatu, lakini mpaka sasa hivi umejengwa mnara mmoja wa Katulukila. Pale Signali, Mbalaji na kule Sululu kuna shida kubwa ya mawasiliano, na wataalamu wamefika pale, lakini tangu wataalamu walipofika, mpaka sasa hivi wamepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushukuru kwa ajili ya *SGR*. Nimesema kuna changamoto ndogo, naomba niseme hapa

nikimalizia, ili Mheshimiwa Waziri atusaidie. Kuna baadhi ya wananchi wetu wamekuwa wakilalamika juu ya ufungaji wa mizigo wanapopanda *SGR*. Naomba mjaribu kuona, mtu anapokuwa na kiroba ametoka Dar es Salaam, anaambiwa akafunge mzigo kwa shilingi 5,000 au 3,000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Asenga kwa mchango mzuri.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanalilalamikia sana jambo hili...

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imelia.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula, Mheshimiwa Mariki na Mheshimiwa Magesa, jiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, nami nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa fursa ya kusimama katika Bunge hili ili kuchangia taarifa zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nimpongeze Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Kakoso. Amewasilisha Taarifa ya Kamati vizuri na kwa weledi mkubwa sana, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hapa ningependa ieleweke wazi, tunapompongeza Mheshimiwa Rais, hatumpongezi tu kwa sababu eti ni uchawa, tunampongeza kwa sababu amefanya mambo makubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu miradi yote mikubwa ya kimkakati wakati anaingia madarakani, miradi hii ilikuwa haijakamilika na miradi mingine ilikuwa katika hatua za awali, lakini Mama amepambana yeye pamoja na viongozi wengine, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, wamepambana kuhakikisha miradi hii inakamilika. Ndiyo maana tunampongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani, zaidi ya vijiji 4,071 vilikuwa havina umeme. Leo tunapozungumza vijiji vyote 12,000 vina umeme. Ndiyo maana tunampongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri ambao wanaripoti kwenye Kamati yetu. Kwa kweli wametupa ushirikiano mkubwa na ni uwazi usiofichika, walipokea sana ushauri na maelekezo ya Wanakamati. Ninawapongeza sana Mawaziri kwa usikivu wao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia Taarifa ya Kamati yetu na hapa ninapenda sana kuanza na sekta ya ujenzi. Tunafahamu kabisa maendeleo yoyote yanachochewa sana na ujenzi wa barabara, na wananchi tunatamani sana kuona barabara hizi zinajengwa katika maeneo yetu na tuko tayari kutoa maeneo yetu ili tupate maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati tulibaini kwamba, utaratibu unaotumiwa na Serikali kulipa fidia kwa wananchi ambao wametoa maeneo yao, ni utaratibu unaoleta kero sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iko wazi kabisa. Inasema, kama mtu atatoa eneo lake ndani ya miaka miwili, awe ameshapewa fidia, na kama itashindikana, tathmini ifanywe tena. Sasa hapa tunapenda kuishauri Serikali kwamba, kama tunakuwa hatujajiandaa kuwapa wananchi wetu fidia kwa wakati, ni bora tuwaache wananchi waendelee kuendeleza maeneo yao. Hii itawauzia wasitishe shughuli zao za kiuchumi, na kuwafanya waache biashara zao. Pia,

kuwacheleweshea fidia tunawakwamisha kimaendeleo na kusababisha umasikini kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niungane kabisa na Kamati. Kama Serikali tutakuwa bado hatujajipanga na bado hatupo tayari kulipa fidia, ni bora tuwaache wananchi mpaka pale tutakapokuwa tayari kuwapa fidia wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, napenda sana kulipongeza Shirika letu la Ndege *ATCL*. Ni ukweli usiofichika, tunaona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kufufua shirika letu. 2016 tulikuwa na vituo vinne tu, lakini leo tunavyozungumza tuna vituo 28. Kwa hiyo, tunaona kabisa dhamira ya dhati ya Serikali ya kufufua shirika letu. Katika vituo hivi 28, vituo 13 ni vya ndani, vituo tisa ni vya kikanda na vituo vitatu ni vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika dhamira hii ya kuhakikisha shirika letu linafufuka na kuanza kutengeneza faida, shirika hili linakabiliwa na changamoto ambazo zinalikwamisha kufikia malengo yake. Hapa changamoto kubwa ni matatizo ya usanifu wa ndege yetu ya *Airbus 220 – 300* ambayo imekuwa na hitilafu kwenye *engine* zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sababu inafanya ndege yetu inakuwa inapata hitilafu mara kwa mara na kulisababishia shirika hasara. Sasa kwa mwaka mmoja tu ndege hizi zimezalisha hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 127.5. Hizi ni hela nyingi ambazo zingeweza kufanya mambo mengine kwa shirika na kusaidia shirika kupiga hatua kama ilivyo dhamira ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaisisitiza Serikali hapa, iharakishe upatikanaji wa *engine* ya ndege hizi ili ndege hizi zilete faida na tuache kuzisema kwamba zinatengeneza hasara kwa sababu matatizo mengine kama haya ya *engine* ni matatizo ambayo yako nje ya uwezo wa kiuendeshaji. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijitahidi kulifanya jambo hili kwa haraka ili kuleta faida katika ndege hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwenye suala la mawasiliano. Nimewahi kuongea hapa, nimeongea kwenye Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa wameongelea suala la mawasiliano. Tunaipongeza Serikali, tulisaini mikataba ya zaidi ya minara 750 mbele ya Mheshimiwa Rais, lakini kwa kweli kasi ya ujenzi wa minara hii iko chini sana. Bado kuna changamoto ya minara katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba sana niungane na Kamati. Bado kuna changamoto ya minara hasa katika maeneo yale maalumu, barabara kuu, mapori tengefu na kwenye mbuga za wanyama. Leo ukiwa unaenda Rukwa, ukipita Mpanda – Katavi ukiwa unatokea Tabora unaweza kutembea zaidi ya kilometa 50 ukiwa hauna mtandao. Sasa hii ni hatari hata kwa usalama wa raia, mali zao na hata usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiwa unatoka Mpanda unaenda Namanyere, unatembea umbali mrefu bila mawasiliano.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sigula, ni kengele ya pili.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali ilifanyie kazi. Naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali ilifanyie kazi, naunga mkono hoja, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariki, halafu Mheshimiwa Magessa na Mheshimiwa Ndulane mjiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia uzima na afya

njema mpaka ameniwezesha mwaka huu 2025 kusimama katika Bunge hili Tukufu na kutoa mawazo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya Kamati na mapendekezo ya Kamati katika Bunge hili. Pia, nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwa uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu la Tanzania. Sote ni mashahidi Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani kulikuwa kuna miradi mikubwa sana ya kimkakati ambayo ilikuwa bado ipo chini katika asilimia za utekelezaji lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama wa Taifa letu kwa utekelezaji mzuri wa mambo yaliyoachwa na mwasisi aliyepita ameweza kusimamia ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na mpaka hivi tunavyozungumza limetekelezwa kwa zaidi ya 99%. Hivyo tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua kubwa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kufikia 99% tu, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa muungwana, ameweza kumlipa mkandarasi kwa zaidi 6.2%, ameweza kulipa trilioni 6.2% sawa na 94%. Huu ni uzalendo mkubwa na ni mapenzi makubwa kwa Taifa hili kuona kwamba mradi mkubwa kama huu unatekelezwa lakini mkandarasi analipwa. Ni Marais wachache sana wanaweza kufanya haya aliyoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuangalia na kumlipa mkandarasi huku mradi ukifikia 99%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi tunaelewa kwamba *megawatt* za umeme katika nchi yetu zilikuwa chini sana, lakini tangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani mpaka sasa tunavyozungumza tuna *megawatt* zaidi ya 3,400, ambapo mahitaji ya nchi nzima ni *megawatt* 1,890 sasa tuna ziada ya *Megawatt* 1,500. Haya ni mapinduzi makubwa sana aliyoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tuna kila sababu ya kumpongeza kwa kuwa nchi ilikuwa na tatizo la kukatika katika kwa umeme, hivyo niwatoe wananchi wasiwasi, sasa Tanzania ina ziada ya *Megawatt* 1,500. Hivyo, niwahakikishie wananchi kwamba tatizo la kukatika katika kwa umeme litakwenda kupungua kwa kiasi kikubwa na hivyo tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa usimamizi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaacha kumpongeza Waziri wa Nishati anayesimamia sekta hii pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika na kuondoa sintofahamu zilizokuwa kwa wananchi waliyokuwa wakisema bwawa hili haliwezi kukamilika, lakini sasa tuna 99%.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningependa kulizungumzia ni suala la gridi ya Taifa. Sote tunaelewa kuwa Mkoa wa Kigoma sasa umeunganishwa katika gridi ya Taifa. Tunaipongeza sana Serikali. Vilevile, tunatambua kuna mikoa michache ambayo bado haijaunganishwa katika gridi ya Taifa ikiwa ni pamoja na Mkoa wangu wa Katavi, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Lindi pamoja na Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiombe sana Serikali lakini tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia sekta hii aweze kusaidia uunganishwaji wa mikoa hii katika gridi ya Taifa ili tunapozungumzia shamrashamra za kukamilika kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere na wananchi wa mikoa hii tuweze kupata matunda kwa kuunganishwa katika gridi ya Taifa na kuepukana sasa kutumia umeme wa majenereta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mkoa wangu wa Katavi. Mkoa wa Katavi ilikuwa uunganishwe katika gridi ya Taifa mwezi wa Kumi, lakini kuna changamoto kidogo iliyojitokeza kutokana na mvua zinazoendelea, lakini Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko alivyokuja katika Mkoa wetu wa Katavi alituhakikishia kuwa wananchi wa Mkoa wa Katavi tutakwenda kuunganishwa katika gridi ya Taifa ifikapo mwezi Februari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri wetu, wananchi wa Mkoa wa Katavi tuna matumaini sana naye, vilevile, tuna matumaini sana na Serikali yetu ya Awamu ya Sita. Nakuomba sana mwezi Februari kama alivyotuahidi wananchi wa Mkoa wa Katavi tuondokane na umeme wa majenereta ambao ni umeme wa kusuasua na sisi tuweze kuunganishwa katika umeme wa gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni changamoto iliyokuwa imejitokeza. Tulivyokuwa tumefanya ziara kama Wajumbe wa Kamati Jijini Dar es Salaam, tuliona changamoto ya vituo vichache vya ujazaji wa gesi kwenye magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kuwa Sikivu. Mwaka 2024 tulikuwa tunazungumzia changamoto ya vituo vichache vya kujaza gesi kwenye magari, lakini mwaka huu wa 2025 Januari mwishoni Kamati tuliweza kufanya ziara na kujionea, ni kwamba Serikali imesikiliza kero hii. Tayari Serikali imejenga kituo cha kujazia gesi katika magari chenye uwezo wa kujaza zaidi ya magari 1,200 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hii yote ni kutokana na jitihada za Mheshimiwa Rais wetu na Mheshimiwa Waziri wetu wa Nishati pamoja na Naibu wake kwa kusikiliza maoni ya Kamati na kuona kero za vijana wanaopambana kukaa pale zaidi ya masaa matatu mpaka masaa matano kujaza gesi na kupoteza muda mwingi sana, lakini changamoto hii inaenda kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe hofu vijana wanaoendesha magari ya *bolt* kwa kutumia mitungi ya gesi ile wanayojaza kwamba changamoto yao imesikilizwa na Serikali yao ni Sikivu, waendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani wataenda kujaziwa magari yao pasipo kupanga foleni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la nishati safi ya kupikia. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa kwanza

wa Afrika kwa kuhakikisha kwamba nishati safi na salama ya kupikia inakuwa inatekelezwa kwa vitendo na siyo maneno. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jitihada za Wizara pamoja na Serikali kutenga pesa zaidi ya shilingi bilioni 8.6 kwa ajili ya ukamilishaji wa ufuatiliaji wa nishati safi, na pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariki ahsante.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa mambo makubwa wanayoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba kuunga mkono hoja kwa kusema kwamba kwenye Wizara ya Madini pia tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa leseni za wachimbaji wadogo na pia Serikali kusimamia ununuzi wa dhahabu yetu kupitia *BoT*. Hii inaonesha kwamba Wizara imejipanga na Mheshimiwa Kaka Mavunde amejipanga na sasa Tanzania tunakwenda kuwa na akiba. Taifa lolote linalotaka kuendelea ni lazima waweze kutunza dhahabu kwa kutumia akiba ya Benki ya *BOT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndulane, na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula jiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii tena. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii tena ya kuweza kuchangia kwenye taarifa zetu ambazo leo zimetolewa ambazo ni za Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ambazo zimetarajiwa, lakini ni dhahiri kwamba yapo mambo

makubwa kwenye Kamati ya Nishati na Madini ambayo tumeyaona, kwamba sasa vijiji vyote 12,000 ndani ya nchi hii vimepata umeme. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu haya ni mambo yanayoonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vitongoji takribani 33,000 ambavyo ni kama 52.3% vimeshawekewa umeme. Hoja yetu, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais ni ombi kwamba Wizara iendelee kusukuma vizuri kazi hii ili vitongoji vyote vilivyobaki 31,000 viweze kupata umeme ili kila Mtanzania aweze ku-*enjoy* mazingira ya kutumia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Yeye ndiyo *champion* wa *clean cooking energy* (nishati safi ya kupikia). Mmeona mkutano uliokuwepo juzi tu hapa na maazimio yaliyotolewa, lakini bado tumeshagawa mitungi takribani 420,000 huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohitajika ni elimu kubwa sasa ili wananchi wasi-*misuse* matumizi ya ile mitungi. Wizara iuchukue ushauri wangu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba elimu ya kutosha inatolewa kwa wananchi wetu ili waweze kuifanya vizuri kazi hiyo ya kutumia nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa jitihada kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba Wizara hii inawapatia wananchi maendeleo tarajiwa. Kama nilivyosema, vipo vitongoji vingi ambavyo vimeanza kupata umeme, lakini ipo mipango mingi ambayo inaendelea kufanyiwa kazi na Wizara hii wakiwemo Katibu Mkuu na wataalamu wote waliopo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kazi kubwa inayoifanywa na ninaamini tukiendelea na utaratibu unaofanyika sasa hivi, tutafikia mahali pazuri zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nampongeza ndugu yangu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Mavunde kwa kazi kubwa

anayoifanya. Mimi ninatoka eneo la wachimbaji wadogo, naweza kuona sasa namna kazi inavyoanza kuwa rahisi kwenye maeneo yale, lakini bado kuna kazi kidogo tu ya kuhakikisha kwamba *GST* wanawezeshwa ili waweze kuonyesha madini yanapatikana wapi ili tusiendelee kubashiri wakati tunatafuta haya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi nitoe ushauri kwenye maeneo haya. Kwenye umeme ni dhahiri kwa ripoti hii tumezalisha sana umeme sasa. Tuna umeme ambao kila mmoja anasema mpaka Desemba tulikuwa na megawati 736 ziada, lakini mpaka sasa tuna zaidi ya megawati 1,000 ambazo ni ziada. Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu Ijumaa tu alisema wazi mtambo wa mwisho mwezi wa Pili huu utakwenda kuwa *commissioned.* Kwa hiyo, nina uhakika kwamba tunakwenda kulitumia Bwawa la Mwalimu Nyerere *full 100%*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo kubwa tulilonalo sasa ambalo linawezekana wananchi wameendelea kuona umeme unakatika, hapa ndipo nataka kuweka ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa ya miundombinu, lakini Serikali imeshaliona, ikaja na Mradi wa Gridi Imara. Kwa hiyo, siyo kitu ambacho tunakishtukiza. Suala kubwa tu ni kwamba bajeti inayotengwa kwa ajili ya Gridi Imara, ipatikane ili kusudi huo usafirishaji na usambazaji wa umeme ufanyike kama tunavyotarajia. Tuna-*upgrade*, tunaboresha miundombinu; kwenye sehemu fulani, zilikuwa na *line* ambayo inasafirisha *KV* 220, sasa tunaweka 400; kuna mahali tulikuwa tunasafirisha *KV* 220, sasa tunasafirisha zaidi ya *KV* 400; nakuna mahali tulikuwa *KV* 66 tunaweka 132 *KV*. Kwa vyovyote vile lazima kuna mabadiliko. Kwa hiyo, fedha zipatikane za kutosha kwenye maeneo haya kuhakikisha kwamba miundombinu hii inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine tumewapatia umeme wananchi wetu ambapo tumesema vitongoji 33,000 vimepata, lakini utasikia wananchi wanasema sasa hivi wanapeana mgao wao, kwamba mashine mbili ziwake mashine mbili zisiwake kwa sababu kuna *transformer* imezidiwa mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ile *model* iliyotumika mwanzo ya kila kijiji kupewa *transformer* ya 50 *kVA* ilikuwa sahihi kwa sababu yalikuwa ni majaribio lakini sasa kutokana na utashi na uhitaji wa umeme, hebu tuibadilishe, tuje na *transformer* kubwa kidogo ili wananchi wetu wasianze kuzima mashine moja na mashine ya pili wakati wanaenda kutumia umeme huu ambao tumewapatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa ile *model* ya kwanza tuliyoitumia ndugu zangu wa *REA* hebu tuibadilishe kidogo sasa tuweke angalau 100 *kVA* ili kusudi matumizi haya yanayotegemewa kule vijijini na yanayotokea yaweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa wazi, kwenye miradi ya Gridi Imara kama nilivyosema mwanzo, tunaona kabisa fedha kutoka nje takribani shilingi bilioni 53.2 hazikupatikana kwenye bajeti. Hizi zinatakiwa zipatikane ili kazi hii ifanyike.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ni kengele ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niguse madini kidogo. Ndugu zangu wa madini wamefanya kazi nzuri sana, *STAMICO* wamepewa mitambo, lakini mitambo yenyewe tuliyopewa bado uhitaji ni mkubwa sana kwa wananchi wetu, kwa sababu huo ulikuwa ni mwanzo. Naomba mitambo hiyo iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi Jimboni Busanda nina kata 14 kati ya 22 wanazochimba madini. Mitambo mitano iliyopelekwa, haitoshi kufanya hizo *exploration* ambazo tunazitegemea hapo. Kwa hiyo, naomba mitambo hii, kama tulianza, sasa tuiongeze ili wananchi wetu wapate urahisi wa kupata madini. Kama nilivyosema mwanzo, *GST* wawezeshwe kwa kiwango kikubwa ili wananchi wetu wasiende kubashiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni *transformer spacing*. Hizi *transformer* ambazo tunaziweka kwa watu, kumekuwa na umeme unaonekana unawaka kidogo. Tulivyozigawa zile *transformer* kwenye maeneo yetu wengine wanapata umeme kutoka mbali sana kwenye *transformer*. Tuhakikishe kwamba *spacing* hii nayo tunaiangalia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ndugu zangu wa barabara kule jimboni kwangu, kuna barabara ilitajwa kutoka Mpomvu kwenda Kakola kwenye bajeti iliyopita, na pia kutoka Katoro kwenye Ushirombo sijaona chochote kinachoendelea labda niombe tu kwa sababu tayari bajeti ipo na utekelezaji unaendelea na ripoti tumesomewa hapa, haya nayo yafanyiwe kazi ili wananchi waweze kupata huduma tarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja na ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, na Mheshimiwa Sophia, jiandae Mheshimiwa Fiyao.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Taarifa zetu mbili za Kamati; Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini. Kwa hakika Waheshimiwa Wenyeviti wetu wameweza kutoa taarifa nzuri zenye kuelezea kwa mapana namna ambavyo Wizara za Kisekta zinazosimamiwa na Kamati hizi zimekuwa zikifanya kazi kwa juhudi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kutumia nafasi hii ningependa kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika tumepiga hatua kubwa katika sekta hizi takribani nne, tano ambazo imezitaja ikiwemo ya barabara, reli, umeme, pamoja na madini na pia mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwaka 2024 tulipata gharika iliyotokana na mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya tayari Serikali imechukua hatua zaidi ya shilingi bilioni 840 zimewekezwa ikiwemo shilingi bilioni 140 katika Mkoa wa Lindi na tunaishukuru Serikali, sisi Mkoa wa Lindi tulikuwa wa kwanza kusaini mikataba ya wakandarasi ambao sasa hivi wapo *site* wanajenga barabara mbalimbali katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi uliyoonyeshwa katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ni ufanisi wa kuigwa Barani Afrika, kwa kweli unaenda vizuri na umeanza kuleta tija kwa kuanza kuleta umeme mwingi katika maeneo yetu au nchini kwetu na ziada imeanza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara tayari uzalishaji wa umeme umeongezeka kwa zaidi ya *Megawatt* 22.5 na ukichanganya sasa zile *megawatt* 22 zilizokuwa zinazalishwa mwanzo, sasa hivi tuna zaidi ya *Megawatt* 44 zinazalishwa na ambazo tumekuwa tukitumia umeme na kusaza kwa sababu matumizi ya Mikoa ya Lindi na Mtwara ni kama *megawatt* 27 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna zaidi ya 14 hazitumiki kwa sasa. Utekelezaji wa Mradi ya *SGR* ni kielelezo tosha kwa namna ambavyo Serikali yetu inazingatia kuweza kutatua changamoto ya miundombinu ya reli ambayo katika siku za nyuma ilikuwa inasumbua kwenye usafirishaji wa abiria pamoja na usafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme kama nilivyosema kwa kweli tumepiga hatua kubwa. Kwa hiyo, ninawanapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri, nikianza na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Naibu wake, na pia rafiki yangu Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kazi nzuri katika Wizara yake ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kwanza kwa kuanzia na zile barabara ambazo zinatengenezwa kwa kupitia zile shilingi bilioni 140 ambazo Serikali imezitafuta. Kazi inaendelea vizuri,

lakini kuna changamoto kwenye wale wakandarasi kufika *site,* baadhi ya wakandarasi hawajafika *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweze kuwasimamia wakandarasi wote wawe *site* kwa sababu, mkataba uliowekwa unadumu kwa miezi kumi. Kwa hiyo, mikataba ilisainiwa tangu tarehe 7 Oktoba, nakumbuka na sisi Wabunge wa Mkoa wa Lindi tulihudhuria, lakini baadhi yao hawajafika *site*, hawajaanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza mkandarasi mmoja, anaitwa *Makapo Contractors,* ambaye wiki moja tu baada ya zile kazi kutolewa na kusaini ile mikataba, tayari alishapeleka vyombo pale *site*. Nampa hongera sana huyu mkandarasi na kwa kweli, anakwenda vizuri sana. Mheshimiwa Waziri mwezi uliopita alikwenda kutembelea na aliona kazi inavyoendelea pale, tena bahati nzuri huyu ni mkandarasi mzalendo. Hii inaonesha ni namna gani wakandarasi wetu wameiva kuweza kufanya kazi kubwa kubwa kama hizi ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, changamoto ya pili katika ile miundombinu ya barabara ni *diversion* kwenye yale madaraja. Wiki iliyopita zaidi ya maeneo manne matano, makaravati madogo ya plastiki yaliyowekwa yamezolewa na mengi yamesukumwa kwenda baharini kutokana na mvua zilizonyesha wiki iliyopita. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara iangalie uwezekano wa ile teknolojia ya kutumia makontena. Yale makontena ambayo Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala, aliyozungumzia hayajawekwa maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda barabara ya njia nne, Kipatimu, makalavati mengi yamezolewa na maji, yameondoka, kutokana na hizo mvua zilizonyesha. Kwa hiyo, kote huko waweke makontena ya futi 40 ili wakati madaraja yanaendelea kutengenezwa, basi magari ya abiria na mizigo yaweze kupita kusudi shughuli za kibinadamu ziweze kuendelea, hali ya maisha iweze kutengemaa na kuwa bora, kwa sababu hali siyo nzuri tangu mwaka uliopita zilipotokea zile tufani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye upande wa umeme napenda kushauri kwamba, sasa wakati umefika wa kuharakisha ule Mradi wa gridi ya Taifa kuchukua umeme kutoka Tunduru kuja Mikoa ya Lindi na Mtwara, ili pale inapotokea dharura, kupitia mitambo yetu iliyopo Mtwara na ule uliopo Somanga, kuwe na *alternative* ya kupata mawasiliano kutoka katika eneo hilo kwa njia hiyo ya umeme ambao unapatikana kupitia grid ya Taifa. Kwa hiyo, naomba huo mradi uharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la *SGR* tumeshuhudia reli yetu inapita katika maeneo ambayo yaliainishwa tangu enzi za wakoloni. Mkoloni wa Kijerumani ndiye ambaye alianzisha *central rail line,* lakini pia kuna reli inayoenda Mikoa ya Kaskazini na ile ambayo ilikuwa inatoka Mtwara kwenda Nachingwea. Reli ya Mtwara – Nachingwea imekufa, lakini reli hii ya kati unakuta *SGR* inapita katika maeneo yale yale ambayo *MGR* inapita. Kwa hiyo, kwa upande wangu hili naona ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naona kabisa kuna uwezekano wa *MGR* kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi kwa sababu, watu wengi watakimbilia kupanda *SGR* na watasafirisha mizigo kupitia *SGR*. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa kufa kwa reli ya *MGR* kwa sababu, itakosa ufanisi wa kushindana na *SGR* kwa kuwa inapita mle mle.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika siku zijazo naomba Serikali kwanza ibuni mfuko wa kujenga hizi *SGR*. Kama tulivyofanya kwenye Mfuko wa Barabara na kama tulivyofanya kwenye Mfuko wa Maji, pia, uundwe mfuko wa kuendeleza miundombinu ya *SGR* ili hatimaye tuweze kuunda ile kama ilivyofanyika kwenye umeme. Tuna *Grid* ya Taifa ya Umeme, kama ilivyofanyika kwenye maji, tuna mwelekeo wa kuwa na *Grid* ya Taifa ya Maji; basi tuwe na *Grid* ya Taifa ya Barabara ambayo pia tutaangalia yale maeneo ambayo hayakupitiwa na hii reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule ambako reli ya *MGR* haikupita, basi huko ndiyo tukupe kipaumbele. Tuone barabara ya reli inatoka Dar es Salaam kwenda Lindi, mpaka Mtwara na kuna ile ya *Mtwara*

*Corridor;* kutoka Mtwara kwenda mpaka huko kwenye madini ya makaa ya mawe Msongo, Kiwira na kwingineko. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, halafu Mheshimiwa Sophia na Mheshimiwa Fiyao wajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa nami kuchangia katika hoja za Kamati hizi mbili zilizoko Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliotangulia kusema katika kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali nzima, hasa katika ule mkutano mkubwa ambao umemalizika hivi karibuni, lakini zaidi sana nampongeza Mheshimiwa Mwalimu Dotto Biteko anayesimamia Wizara ya Nishati, ambaye tumekuwanaye katika Kamati. Kwa kweli, kazi inaonekana na tunawapongeza watumishi wote kwenye ile Wizara kwa sababu, mambo yote yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza katika vipaumbele vyao na ninadhani nitaongea kimoja; kwa zaidi, kile kinachozungumzia habari ya kuendelea kupeleka umeme, likiwemo suala zima la kusambaza na kusafirisha umeme katika maeneo yetu. Kazi hii imefanyika vizuri, na hasa tunapoangalia kwenye suala la uzalishaji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi tu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati amezungumzia hali halisi katika ile mitambo yote minane, imeshaingiza umeme na tuna *Megawatts* zaidi ya 1,880. Hongera sana kwa hilo kwa sababu, tunajua hata yale maeneo,

hususan ile mikoa mitano ambayo ilikuwa haijafikiwa na *grid* ya Taifa nadhani itafikiwa kwa sababu, umeme wa kutosha upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali yote kuhakikisha kwamba, ule ukarabati wa miundombinu inayotakiwa kusafirisha umeme iweze kukarabatiwa haraka kwa sababu, wananchi sasa wanashindwa kuelewa umeme unazalishwa mwingi, lakini unakatika. Wanashindwa kuelewa kwamba, pengine ni suala la miundombinu kuwa chakavu, kwa hiyo, kasi iongezeke kule. Kama ambavyo tumezalisha umeme wa kutosha, basi tuhakikishe na ile miundombinu inakarabatiwa vizuri, ili umeme uweze kuwafikia wananchi. Kinginevyo kazi nzuri sana imefanyika na ninaipongeza Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yale maazimio ambayo yalitolewa na Kamati, ambayo tulitaka yafanyiwe utekelezaji, kati ya yale 26, mawili yamekamilika vizuri, 20 yako kwenye mchakato yanakwenda vizuri na mawili bado. Basi naomba yale ambayo hayajaguswa kabisa yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nizungumzie suala la usambazaji umeme katika vijiji, *REA*. Tuipongeze sana Serikali *almost* vijiji vyote vimefikiwa, na vitongoji ni kama 50% vimeshafikiwa. Rai yangu ni katika ile miji au vile vijiji 15 ambavyo vilitolewa katika kila majimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya habari ya msongo wa umeme ilijitokeza kusema kwamba, vijiji viko mbali na *line* kubwa. Naomba sana kwa sababu, vilikuwa vimeshawekwa katika utaratibu, basi, kutokana na changamoto iliyopo, ule mradi unaofuata waweze kuvikumbuka kwanza hivi vilivyowekwa halafu vikaachwa kwa sababu ya kuwa mbali na *line* kubwa, vinginevyo tutakuwa tumepata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba katika visiwa nchi hii ina visiwa vingi sana, lakini havina umeme wa uhakika. Basi katika ule mpango wa Serikali wa kufikisha umeme katika visiwa vyetu, naomba sana kasi iongezeke. Kwa Mwanza tuna Kisiwa cha Base, tunacho cha

Iginga kule Magu, pia bado kwa jirani yangu Gazba kule Muleba, nao wana visiwa vingi tu. Wale wakipata umeme wa uhakika ni wazalishaji wanaotegemea bidhaa ya ziwani. Pia, watasaidia katika kukuza uchumi wetu. Tuwape unafuu katika suala zima la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nizungumzie suala la ubadilishaji wa mfumo katika magari yetu kwamba, sasa yanatakiwa yatumie gesi. Kasi iliyopo ni ndogo, eneo wanalobadilishia ni moja na gharama ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, inapoagiza magari, basi angalau iagize ambayo tayari yameshafungwa huo mfumo, ili hata ule mwonekano wake uwe mzuri kwa sababu, hapa kwetu tunafunga, lakini mwonekano wa gari pia unakuwa siyo mzuri kwa sababu, *the way* wanavyoweka ile mitungi haifanyi lile gari lionekane katika ule mtazamo wake. Basi, tuagize na Serikali iwe ya kwanza katika kutumia hayo. Tunahamasisha wananchi, lakini Serikali sijaona ni Wizara ngapi zina magari ambayo yanatumia gesi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli yetu.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa hiyo, naomba sana, ili liweze kufanyika, tuweze kuona ni jinsi gani tunakwenda kuwahudumia hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mfupi, naomba nizungumzie suala la madini. Nampongeza Waziri wa Madini na timu yake. Kwa sababu, ile *survey* ya maeneo yaliyo na madini ni 16% tu, lakini wana agenda 2030 ambayo wanakwenda kupima au kufanya *survey* kwa nchi nzima. Naomba sana kasi hiyo iendelee kwa sababu, utajiri wa Tanzania umelala kule. Watu wa *GST* wanafanya kazi nzuri, lakini waongeze kasi ili waweze kufanya na Serikali iwape pesa ya kutosha ili waweze kufanya kazi yao hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amewawezesha wachimbaji wadogo. Tunajua kuna taratibu za Sheria ya Madini na Sheria ya Ardhi, anayemiliki ardhi

ana haki yake ya kumiliki, ile *surface right,* lakini tunaye mtu wa madini, naye ana haki yake *(mineral right)*. Kwa hiyo, ninachotaka kusema tu hapa ni kwamba, habari ya kuwaondoa watu kwenye maeneo yao eti kwa sababu kuna mtu ana *mineral right,* naomba sana angalau waweze kupewa nafasi ya kuwa sehemu ya wamiliki. Hata kama utampa asilimia mbili ya *shares,* bado utamwezesha huyu kufaidika na ardhi yake kwa sababu yuko juu, hajui huku chini kukoje, lakini wewe ukipata kitu chini unataka huyu aondoke, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuone namna bora ya kuwawezesha wachimbaji wetu, ili nao waweze kumiliki. Wale wamiliki wa ardhi wenye *surface right* nao waweze kuwa sehemu ya umiliki wa yale madini yanayopatikana chini ya ardhi zao ambazo hawakuwa wanatambua ni nini kilichopo kule ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba niongelee suala la miundombinu. Nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Ulega na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ombi langu ni kwamba, zabuni nyingi zimetolewa kwa wakandarasi wengi nchi nzima na kwangu kukiwepo; Wilaya ya Ilemela na Jimbo zima lina lami asilimia tatu tu, kuna baadhi ya barabara ambazo wakandarasi wamepewa, lakini mpaka leo hawajaanza ikiwa ni pamoja na majimbo mengine. Kwa hiyo, naomba sana wakandarasi hawa wawezeshwe ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kipindi cha mvua kimeanza na kinakwenda vibaya. Mvua ni kubwa, ni nyingi inanyesha, kama hawatafanya kazi hiyo mapema mwisho wa siku tutarudia yale yale ya mwaka 2024. Gharama kubwa itaenda katika kukarabati miundombinu na ile ambayo imewekwa, kwa ajili ya kuweza kufanyiwa kazi sasa haitawezekana. Naomba sana wawezeshwe ili waweze kufanya kazi zao. Hii ni pamoja na wale wa *TARURA* ambao wamepewa kandarasi, lakini hawajaweza kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kuna wale wapangaji wa *TBA*. Naomba ni-*declare interest* kwamba, kule kwangu kuna wazee waliostaafu muda mrefu, zaidi ya 15, wanakaa katika zile nyumba za Ghana. Walikuwa na kesi na Serikali, kesi ile wameshindwa, lakini

bahati nzuri, Serikali bado imeendelea kuwanao. Serikali ilishinda na wanatakiwa kulipa malimbikizo ya deni la pango walilokuwanalo. Naomba sana, kiwango mlichowapa ni kikubwa, kiwango cha shilingi laki 400,000 kwa mwezi ni kikubwa sana, maana anatakiwa alipe shilingi 450,000, lakini wakati huo huo alipe pango la mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwapunguzie angalau walipe shilingi 300,000 au shilingi 250,000 kwa mwezi. Alipe pango lake la mwezi, lakini awe anapunguza na lile deni ambalo lina-*accumulate* baada ya kuwa wanaendelea na kesi. Naomba sana kwa sababu, hawa ni watu wazima, ni wastaafu na pensheni yao ni shilingi 100,000 tu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Ukimwambia alipe shilingi 450,000 hawezi, atazitoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Sophia, nafasi yenu ni moja kwa hiyo, mnagawana wewe na mwenzio. Msije mkasahau ukaanza kunini.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuchangia. Niendeleze pale alipoishia mwakamati mwenzangu. Wachimbaji wadogo wadogo wanatakiwa walindwe na Serikali yetu kwa sababu, wao ni sehemu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja, tunapokuwa na wachimbaji wadogo na tukapata mwekezaji mmoja, basi, wale wengine watafutiwe sehemu nyingine na wale wachimbaji wadogo wadogo waendelee kukusanya kodi na kuchimba maeneo waliyokuwa wakichimba. Wakati mwingine ni

vema tukawa na diplomasia ya kiuchumi pamoja na watu wetu wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Taifa moja sasa limetoka kuuza maua Kariakoo, limeenda kwa wachimbaji na wanawadhulumu; wanaenda hawana vibali, wanaenda kuandika mikataba kwa kuwadanganya. Wachimbaji wengi sana wamedhulumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isimamie hilo suala tuhakikishe wachimbaji wadogo wadogo wanalindwa kwa nguvu kubwa sana ili waendelee kuchangia uchumi wa Taifa hili kwa sababu, dhahabu kwetu sisi ni baraka na wala siyo laana, kwamba, mtu wa nje akija aonekane wa maana na mzawa aonekani hafai, aondolewe kwenye eneo husika, hii siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizugumzie suala la wakandarasi. Madeni ya wakandarasi sasa yamefika shilingi trilioni 1.3. Madeni haya ni mabaya sana kwa Taifa letu. Tunafahamu kabisa kwamba, tuna mikataba ambayo tumesaini na hawa wakandarasi, hasa wale wa nje. Tunapochelewesha kulipa, basi madeni yanaongezeka kwa sababu tu hatujalipa kwa wakati, lakini wakandarasi wa ndani pia, tunapozuia kuwalipa kwa wakati tunazuia uchumi wa mtu wa kawaida wa ndani ambaye pesa yake inabaki humu ndani anashindwa kuongezeka uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Kamati imezungumza kwamba, shilingi bilioni 70 zitaenda kulipa madeni ya ndani. Mimi nashukuru kwa shilingi bilioni 70 iliyotengwa kwa ajli ya wakandarasi wa ndani kila mwezi. Kamati imetoa ushauri, ni kitu kizuri, lakini je, wale wa nje itakuwaje? Kwa sababu usipolipa ina maana lile deni litaongezeka, mwisho wa siku tunaleta mzigo kwa watu wanaokuja nyuma yetu kuweza kudaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la *EPC+ F* tulilizungumza katika Bunge hili, lakini inaonekana mpaka sasa limekwama. Naomba Serikali irudie tena kwa sababu, tulisema barabara zaidi ya mita 2,000 *plus* zijengwe nchi nzima. Mimi nafikiri tuirudishe na tuhakikishe inatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunazungumzia suala la madeni ambayo tulisema yatalipwa na kuna watu ambao tayari wameshapeleka kesi. Tafadhali, tunaomba sana Wizara isimamie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunafahamu kabisa, Watanzania wengi wamekufa sana kwa sababu ya *pressure* ya yale madeni ambayo hayajalipwa. Wakandarasi wasipopewa hela yao kwa wakati, kuna wengine wamekopa Benki *CRDB, NMB* na benki nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamezungumzia suala la *SNG*. Nashukuru Wizara ya Nishati imefanya kazi nzuri sana na tunaamini kwamba, tunaweza kuisaidia nchi yetu katika uharibifu wa mazingira kwa kutumia gesi tuliyonayo, lakini mwisho wa siku tunaamini Serikali ndiyo mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba magari yote mapya kuanzia bajeti inayokuja yaje yakiwa na mfumo wa kuwekewa *SNG* ndipo tuwatie moyo watu wengine kuweza kujiunganisha na matumizi ya gesi hii. Naomba sana tuhakikishe kabisa Serikali inaongeza matangazo na kupunguza gharama ili watu wote wajiunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa madini ni 16% peke yake tumeshafanya *research*, lakini tunashukuru kwamba, Wizara imesema inakwenda kuongeza fedha kwa ajili ya kupata ndege na mahitaji mengine ya kuweza kufanya utafiti wa madini, ili tuweze kujua tuna asilimia ngapi ya madini kama nchi. Hii itatusaidia sana kupata pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema msemaji mwingine aliyepita, huwezi kutoa vitalu ambavyo huna uhakika kama kweli vina madini, basi tunaomba fedha hizo zitakapoongezwa na zikatoka kwenye Wizara husika, tutakuwa tumewasaidia watendaji wetu kuweza kusimamia suala la kujua ni wapi tuna madini ya aina gani, yana thamani gani na mwisho wa siku Serikali yetu iweze kupata fedha kwa ajili ya kuendesha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nina hakika viongozi tuliowapa dhamana watasimamia na watafanya kazi vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, Naibu Waziri, jiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye taarifa hizi za Kamati. Kwanza nawapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa namna ambavyo wamewasilisha taarifa ambazo kwa kina kabisa zimezingatia maoni ya Kamati na mambo mengine ambayo tumeshauri katika Kamati zetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wenyeviti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kutokana na muda, naomba kabla ya yote, Serikali itupie jicho katika Mji wa Tunduma kuangalia changamoto kubwa ya mlundikano wa malori ambao umekuwa ukiathiri kwa kiwango kikubwa hata uchumi wa wana-Tunduma mmoja mmoja. Tunajua sisi kama Wanatunduma na wananchi wa Mkoa wa Songwe tunafurahia ongezeko la uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoona malori yanatoka kwa asilimia kubwa, mizigo zaidi ya 73% inatoka bandarini kupitia kwenye mpaka wa Tunduma. Sisi kama wananchi wa Tunduma tunajisikia faraja, lakini changamoto ya mlundikano imeanza sasa. Naona kuna hatari kubwa ya kuathiri uchumi wa mwananchi mmoja mmoja, hususan katikati ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii changamoto imekuwa kubwa sana, lakini kwa kiasi kikubwa pia inachangiwa na changamoto ya mizani. mizani iliyopo pale katika Mji wa Mpemba imekuwa ikizidiwa imekuwa ikizidiwa kwa kiwango kikubwa sana, hali inayosababisha mlundikano mkubwa kutoka kule Chimbuya mpaka kufika Mpemba, magari

yanakuwa hayajavuka kwa zaidi ya saa tano, yanasubiri kupita pale mizani. Hebu Serikali iangalie hii changamoto kwa jicho la pili ione ni namna gani inatusaidia kuitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona hali ilivyo, ukitoka Chimbuya kuja kwenye eneo la Mpemba, pale Mizani, humu njiani hakuna vyoo, hakuna chakula, hakuna chochote. Ona ni namna gani ambavyo madereva wa malori wanakutana na changamoto ambayo pia inaweza ikaleta madhara ya kiafya ndani ya Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu hawana mahali pa kujisaidia, hawana mahali pa kuchimba dawa, hawana mahali pa kula chakula, na ni zaidi ya saa tano wanakuwa wamekaa wanasubiri magari yao yapitishwe kwenye mizani pale Mpemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iangalie namna ya kulitatua hili. Pia, ndiyo maana sisi tumeendelea kushauri kwamba, Serikali ione umuhimu wa kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma. Tayari eneo la kujenga lilishatengwa pale Mpemba, ni zaidi ya ekari, ni eka nyingi sana zimetengwa pale. Hebu Serikali ione umuhimu wa kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma. Hii inaweza kusababisha hii changamoto ya malori ikapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye lile eneo la Bandari ambalo limetengwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa bandari, reli imepita pale. Inaweza ikapunguza hii changamoto, mizigo mingi ikaanza kusafiri kwa njia ya reli halafu mwisho wa siku mlundikano wa yale malori ukapungua nasi wananchi wa Tunduma tukaepuka hii changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, hakuna njia ya ziada, au niseme njia ya dharura ambayo inaweza kuwasaidia wananchi wa Mji wa Tunduma kupita. Kuna hii barabara ambayo inajengwa kutoka Mpemba mpaka pale *Transforma*. Barabara hii ni zaidi ya mwaka inasuasua, hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mji wetu mvua zinanyesha, sasa hivi tuko katika msimu wa mvua, mvua zinanyesha, barabara zina

msongamano, halafu ukienda kwenye hii barabara ya kutoka Mpemba *Transformer,* hakuna kitu kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Serikali ituonee huruma wananchi wa Mji wa Tunduma. Tusaidiwe kwenye hili, tuokoleeni muda, kwa sababu muda mwingi sasa tunautumia barabarani, mambo yetu yanalala, yanakwama na kuna hatari hata ya wagonjwa kupoteza maisha wanapokwenda kutafuta huduma za kiafya, kwa sababu barabara imefunga kabisa, hakuna mahali ambapo tunaweza kupita. Changamoto hii imekuwa ikisababisha ajali kwa kiwango kikubwa sana. Hebu angalieni vizuri namna ya kutusaidia kwenye Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka huu unachangia pato kubwa sana kwenye Taifa letu, angalieni namna ya kunusuru wananchi wa Tunduma ili nasi tuweze kunufaika na hiki tunachokiona, lakini mwisho wa siku kisituletee madhara ambayo yanaweza kutuathiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naona nizungumzie pia barabara ya eneo la Mlowo – Kamsamba.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja. Barabara ya Mlowo – Kamsamba imekuwa ni chachu sana kwa uchumi wa wananchi wa Songwe. Hata hivyo, sasa hivi ni zaidi ya miaka mitano tunaimaliza, hapa tunaambiwa itajengwa, itajengwa. Hakuna kinachoendelea na wananchi wa Mkoa wa Songwe wanahoji kila iitwapo leo. Ni lini barabara hii itajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, subiri bajeti barabara itajengwa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Moshi Selemani

Kakoso kwa kuwasilisha taarifa nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta za Wizara wanazozisimamia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taifa letu, sekta zenye kushughulika na miundombinu ya barabara, reli, vivuko na ndege ni sekta muhimu sana. Sekta hizi ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa Taifa letu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwani kwenye miaka ya karibuni imefanya uwekezaji mkubwa wenye lengo la kuboresha miundombinu ya barabara, reli, bandari na usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha hivi karibuni, Tanzania imefanikiwa kujenga miundombinu mingi ya barabara, reli na vivuko ambayo imeboresha huduma za usafirishaji na kukuza uchumi wa nchi. Katika ripoti ya Kamati, kuna miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara, reli na vivuko inayoendelea kutekelezwa. Kwa mfano, ujenzi wa reli ya *SGR* ambayo imeshaanza kutoa huduma za kusafirisha abiria kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ni ushahidi wa mafanikio kwani reli hii imeboresha huduma za usafirishaji. Huu ni mradi mzuri wa kielelezo. Ni vyema mradi huu ukamilike ili ufike Kigoma na Mwanza na wananchi wa maeneo haya wafaidioe na huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali ifikirie kujenga reli ya *SGR* itakayotoa huduma kwenye Mikoa ya Kaskazini yenye vivutio vingi vya utalii kama vile Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru, mbuga za wanyama za Ngurdoto, Arusha, Manyara, Serengeti na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio makubwa katika sekta hizi, bado kuna changamoto nyingi zinazokabili maendeleo ya sekta hizi. Changamoto kubwa ni ile ya uhaba wa rasilimali fedha. Kama tulivyoelezwa na Kamati, kuna utekelezaji wa kusuasua wa miradi mbalimbali ya barabara, ujenzi wa viwanja vya ndege, reli na vivuko kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi ukilinganisha na hati za madai zilizowakilishwa na

wakandarasi. Upatikanaji hafifu wa fedha umesababisha ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hii, ninaendelea kusisitiza kwamba ni muhimu Serikali ilipe madeni ya wakandarasi na qazabuni kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosababishwa na riba. Kwa upande wa ujenzi wa barabara, madaraja na reli, ni muhimu sana Serikali iwasimamie na kuzisaidia taasisi za *TANROADS,* TAMISEMI na *TRC* ili waweze kutekeleza ujenzi wa miradi ya barabara na reli kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kushauri kwamba ni wakati muafaka kwa Serikali kuchukua hatua stahiki za kuboresha uwajibikaji katika sekta hizi kwa kuendelea kutekeleza ahadi zilizotolewa. Hii ni pamoja kutenga fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri wangu huu, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Mbarawa, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Silaa mjiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hamna mambo mengi, ni kushukuru na kupokea kwa sababu hizi ni kazi mlizozifanya na maoni ya Wabunge ni haya. Sasa mnayachukua kwenda kuyafanyia kazi, sawa!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi. Pili, kwa dhati ya moyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mheshimiwa David Mathayo, kwa ripoti nzuri, pia kwa ushirikiano ambao tunapatiana

katika kuhakikisha tunaisimamia vizuri sekta hii ya nishati. Kwa kweli tunaishukuru sana Kamati na tunafanya nao kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yanayoonekana katika sekta ya nishati, ni jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nasi tunaendelea kumshukuru kwa uwekezaji mkubwa unaoendelea katika sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulie kwa kusema kwamba, kama Wizara tunapokea ushauri na maelekezo yote ya Kamati. Nakubaliana na Kamati kwa masuala yote ambayo wamezungumza na kuonesha umuhimu huu, nitakubaliana nao kwa kuonesha katika maeneo matatu na nitasema kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Kamati kuhusiana na umuhimu wa kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta nchini. Kwa umuhimu huo ndiyo maana Serikali imeanza mikakati tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya uhifadhi wa mafuta inayopatikana nchini, inahusisha miundombinu ya kupokelea na uhifadhi wa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga ambapo mpaka sasa tuna jumla wa maghala 23 yenye uwezo wa mita za ujazo 1,637,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta. Moja, kupitia *TPA* tunajenga maghala ya kuwezesha kupokea mafuta kwa wakati mmoja *(single receiving terminal)* ambayo itakuwa ina ukubwa wa tani 360. Mradi huu utahusisha pia kujenga gati litakaloweza kupokea kwa pamoja meli sita, tofauti na sasa ambapo tunashusha kwa meli moja ya petroli na meli moja ya *diesel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Petroli, tunao mradi ambao tunakwenda kuuanza sasa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, kutengeneza hifadhi ya kimkakati ya hifadhi ya mafuta kwa kipindi cha miaka 10 ili tuweze kuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta takribani tani 800,000. Ni

Mradi ambao ndio tunauanza, lakini ndiyo mikakati ambayo Serikali inayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo, kupitia TAZAMA sasa hivi tunakamilisha *feasibility study* kwa ajili ya kujenga bomba jipya la TAZAMA. Vilevile, ni mradi ambao utahusisha kujenga maghala katika maeneo ambayo *feasibility study* itatuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo, tutakwenda pia kujenga boya maalum la kupitisha mafuta haya ya TAZAMA kwa ajili ya kupunguza msongamano katika bandari pia tuweze kupokea mafuta na kuweka *space* ya kupokea mafuta mengi zaidi kwa ajili ya matumizi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaihakikishia Kamati kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Serikali inaliangalia kwa jicho la kipekee sana suala hili la kuongeza uwezo wa uhifadhi wa mafuta hapa nchini. Mikakati tunayo, na kwa umuhimu wa jambo hili walilolisema tunaungana nao ili kuhakikisha kwamba tunasimamia mikakati hii ili tuweze kutimiza azma hii ya kuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Azimio mkalifanyie kazi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru, na kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ulega, jiandae Mheshimiwa Mbarawa, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Silaa mjiandae. Pia watoa hoja mjiandae.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia

katika hoja hii. Pia, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge nikiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini, nami nasema kwamba, sitamwangusha Mheshimiwa Rais na sitaliangusha Bunge hili katika kila hatua ya ushauri itakayokuwa ikitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya hoja ya Kamati, naomba pia niipongeze sana Kamati yetu ya Kudumu ya Miundombinu, inayoongozwa na Komredi Mheshimiwa Moshi Kakoso, kwa ushauri na maelekezo mbalimbali iliyoyatoa, nasi Wizara ya Ujenzi tumeyachukua yote ambayo wameyaeleza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, tumekuwa tukiutumia vema ushauri wanaoutoa na ndiyo maana kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hapa karibuni ndani ya mwezi Januari na Desemba, fedha nyingi sana zimekwenda kwa wakandarasi hususan wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa ushauri huo huo wa Kamati ya Bunge, ndiyo maana miradi yetu ya dharura asilimia isiyopungua 80 yote inafanywa na wakandarasi wazawa, na kwa kusema kweli wanafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine waliyoyashauri na waliyoyaelekeza katika Maazimio ya Bunge, tumeyachukua na tunakwenda kuyafanyia kazi. Nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu sahihi. Mheshimiwa Mbarawa, jiandae Mheshimiwa Mavunde.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchuku fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia kukutana hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nami naipongeza Kamati yangu ya Miundombinu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutushauri na kutuelekeza mambo mbalimbali yanayohusiana na sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kipaumbele cha kipekee anachokipatia sekta ya uchukuzi. Pia, kama mnavyojua, wiki iliyopita tulisaini mkataba mkubwa wenye barabara yenye urefu wa kilomita 282 kutoka Uvinza mpaka Kitega huko Burundi. Vilevile, hivi karibuni tutakwenda eneo lingine la kutoka Burundi hadi *DRC Congo*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwamba, maoni yote tumeyachukua na mapendekezo yote tumeyachukua na tunakwenda kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mbarawa. Mheshimiwa Mavunde, na Mheshimiwa Silaa mjiandae.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Naomba nami nichukue fursa hii kipekee kabisa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushauri walioutoa, maoni na mapendekezo ambayo yametengeneza Azimio la Bunge siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini tunapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwenye Kamati. Yote walioshauri hasa suala la utafiti wa kina. Masuala ya leseni, mitambo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na ununuzi wa dhahabu, yote yana chimbuko kutoka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaahidi tu kwamba, tutaendelea kushirikiana nao bega kwa bega ili kuhakikisha haya yote tunayafanya kwa ukamilifu na kama Wizara, tumeyachukua maoni na tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Silaa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo Mezani. Pia, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ilimpendeza tarehe 8 Desemba, 2024 kuniteua kuhudumu na kumsaidia kazi kama Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Namwahidi kazi kwa imani aliyonipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia. Pia, wakati wote tunapotokea mbele ya Kamati wanatupatia maelekezo, kutusimamia na kutushauri. Wizara, mimi binafsi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, tunaendela kuwashukuru kwa maelekezo wanayotupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa waliyoiwasilisha, naliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, maazimio haya yaliyopendekezwa na Kamati, yakiidhinishwa na Bunge, sisi tunayapokea na tuko tayari kuyatekeleza. Maelekezo haya yanaenda kutuongezea nguvu kwenye maelekezo mahsusi ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akitupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, niendelee kuliahidi Bunge lako kwamba tutaendelea kuyafanyia kazi na tutahakikisha tunayatekeleza hasa pamoja na mambo mengi waliyoyaelekeza kwenye mashirika yetu, kwenye eneo la wizi wa kimtandao ambalo hata Ijumaa tulileta majibu hapa Bungeni. Tutaendelea kuongeza nguvu kupitia *TCRA* ili wananchi wetu wawe salama zaidi kwenye mitandao inayotumika, kwenye mawasiliano mbalimbali na miamala wanayofanya kwenye simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mtoa hoja, Mheshimiwa Kakoso, halafu Mheshimiwa Mathayo jiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana wachangiaji ambao wamechangia hoja ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wapato 12 na Mheshimiwa Waziri ni wa 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru sana wachangiaji wote ambao wameonesha hisia kubwa ya kuiunga mkono Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ambao wamepitia hoja mbalimbali. Hoja kubwa ya kwanza ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa Stella Fiyao, hawa kwa pamoja maombi yao ni ya ujenzi wa barabara ambazo Serikali ilizipitisha na kuwaahidi wananchi kujengewa hizo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Serikali ilipokuja kwenye Kamati ya Bunge, wameeleza maombi yote ya barabara, na Serikali iko tayari kuzifanyia kazi na wana mchakato kwenye bajeti hii zitaingizwa na wengine wameshaanza kupewa fedha za awali kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Kwa hiyo, tutaendelea kuisihi Serikali kadri maombi ya Waheshimiwa Wabunge walivyoeleza. Tunaomba Serikali iendelee kusisitiza na kufanya umuhimu wa kurekebisha au kuanza ujenzi wa barabara zilizokuwa zimekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya pili ambayo imechangiwa na Mheshimiwa Mtaturu, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Sylivia Sigula, wameipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa sana za maboresho ya bandari ambayo yamefanywa kupitia uwekezaji wa *DP World*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote wana kumbukumbu jinsi ambavyo dhamira ya Mheshimiwa Rais, maono na uthubutu alioufanya kwa ajili ya kuweka mradi mkubwa wa uwekezaji wa bandari. Suala hili lilitikisa nchi kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi walipotoshwa, lakini bahati nzuri kwa sasa yale ambayo Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake, kwa maana ya Mawaziri waliohusika na timu yote ya Serikali, imeanza kulipa na inafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada alizozifanya. Hali ilivyo sasa hivi kwa upande wa bandari, inafanya vizuri sana, wanapata mapato zaidi ya yale ambayo yalikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tunampongeza Mheshimiwa Rais, tulipokuwa tunajadili kwenye Bunge lako Tukufu, tulipitisha sheria ya kuwarudishia *wharfage* bandari. Bandari sasa hivi inakusanya fedha nyingi na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu amewaamini vijana wengi kwenye taasisi nyingi za Serikali. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari ambaye yupo sasa anafanya kazi vizuri sana na anawawakilisha vizuri vijana wote nchini ambao wamepewa dhamana na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado yale ambayo tumeieleza Serikali kufanya maboresho kwenye suala zima la bandari, ni pamoja na kuongeza ujenzi wa gati mpya ambazo zitafanya ufanyaji kazi wa bandari uwe rahisi kwa sababu tuna mategemeo uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye shirika la reli, ujenzi wa barabara na kuongezwa kwa bandari zilizopo kwenye Mkoa wa Kigoma, Katavi na kwingineko kutafanya mzigo mkubwa uwe unapitia kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyapitia ni maboresho ya Shirika la Ndege *(ATCL)*. Hili limezungumzwa na Wabunge wengi, wameelezea zaidi kwenye suala zima la ukodishaji wa Shirika la Ndege, kutoka *IGTF* kukodisha ndege kwenye Shirika la *ATCL*. Ninaamini Serikali sikivu imesikia mawazo ya Wabunge, na mawazo ya Kamati na tunaamini

mchakato wa kurejesha suala zima la ukodishaji wa ndege badala ya shirika kukodi ndege kutoka *IGTF*, sasa hivi tunashauri Serikali wawaachie *ATCL* wamiliki hizo ndege na kupunguza mzigo wa madeni ambao upo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia sana ni suala la reli ya *TAZARA*. Waliochangia sana ni Mheshimiwa Ally Jumbe, Mheshimiwa Kunambi, Mheshimiwa Asenga na hao wote wamepitiwa na hilo Shirika la *TAZARA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba Serikali iendelee kufanya mchakato wa kisheria ambao upo, utakaounganisha kati ya nchi ya Tanzania na Zambia ili kuharakisha uwekezaji ambao utakuja kuondoa miundombinu chakavu, pia ununuzi wa vichwa vya treni sambamba na ununuzi wa mabehewa. Hayo yameshauriwa kwa Serikali kupitia Kamati ya Bunge na Wabunge ndani ya Bunge hili wameshauri. Tunaomba hayo yafanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa suala la Barabara, Wabunge karibu wote waliosimama wamezungumzia sana suala la malipo ya Wakandarasi. Naamini huko nyuma kweli kulikuwa na tatizo kubwa sana la wakandarasi kutokulipwa, hasa wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishaanza kuwalipa, na ninyi wenyewe mnaangalia huko ambako mnaishi na wakandarasi. Suala hili limeanza kufanyiwa kazi na ombi letu kwa Serikali ni kuhakikisha kuendelea kuwalipa wakandarasi ili waweze kufanya kazi zilizokuwa zimebaki na zilizofanya miradi mingi ya barabara kusimama. Ni matumaini yangu Serikali watalibeba na kulifanyia kazi kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wamepongeza juhudi za Serikali zilizofanywa hasa kwenye maboresho ya Shirika la Reli kwenye upande wa *SGR*. Kwenye eneo hili Kamati na Wabunge kwa pamoja tumeungana na tunaipongeza sana Serikali kwa ujenzi kwa ujenzi wa reli ya kisasa ambayo imekuwa kielelezo katika nchi yetu na Mataifa

mengine yamekuja kujifunza kuangalia uwekezaji mkubwa ambao umefanywa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaungana na Watanzania wote ambao wanafurahia huduma nzuri zinazotolewa na Shirika la Reli kupitia Mradi wa *SGR*. Mheshimiwa Musukuma amechangia naye anahitaji huduma za viburudisho zisitishwe. Uhalisia ni kwamba, hilo hatuafikiani nalo kwa sababu zile huduma zitaendelea kuboreshwa zaidi na zaidi ili kulifanya shirika sasa liende kisasa kuliko kuturudisha huko kwenye mifumo ya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni suala la fidia. Kwenye fidia ni eneo ambalo linapita kwenye Shirika la Reli, na kwenye eneo la ujenzi wa barabara *(TANROAD)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua maeneo mengi ambayo bado hawajaweza kuyalipa fidia. Eneo hili ni muhimu sana Serikali ikatafakari na kuangalia kwa kina kufanya marejeo ili kuangalia mfumo wa kulipa fidia ambako kuna uwezekano wa shughuli za kiserikali kuweza kufanyika kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara nyingi ambazo takwimu zake za kulipa fidia zinafika shilingi trilioni 5.5 ambazo Serikali imebeba maeneo yale ambayo hawawezi kuyafidia kwa sasa. Ushauri wa Kamati ni kwamba, tunaiomba Serikali iendelee kuangalia upya yale maeneo ambayo ni ya msingi ambayo wanaweza kujenga miundombinu kwa kupanua barabara kwa wakati, mfano Barabara ya kutoka Dar es Salaam kuja Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma. Hizi zinaweza zikabaki kwenye mfumo ambao zinaweza zikabaki kwenye vipimo vile vinavyohitaji kuongezewa suala la ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara nyingine ambazo ukweli kwa sasa Serikali haina uwezo wa kufanya malipo ya kulipa kilomita 60. Maeneo haya wafanye *review* ili kuondoa changamoto ambayo itaiweka Serikali kuwa na madeni makubwa yasiyokuwa na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wameelezea juu ya Shirika la Posta. Serikali ichukue madeni yanayokuwa makubwa sana yenye thamani ya shilingi bilioni 54. Maeneo haya ni muhimu, Serikali ikaangalia ili kulipunguzia Shirika kuwa na mzigo mkubwa. Wameshauri pia suala la *TBA* kuweza kuachiwa nafasi ya kuwa Shirika ambalo linaweza likakopesheka. Serikali ikaondoe vikwazo ambavyo vinaweza vikalifanya shirika hili kubaki likijitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe. Nawapongeza Mawaziri kwa kazi kubwa ambazo wameendelea kuzifanya, na ninawapongeza sana Ofisi yako ya Bunge kwa kazi kubwa ambayo mmetupa ya ushirikiano mkubwa wa kuchambua taarifa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani Serikali wapo wamesikia yale ambayo Waheshimiwa Wabunge na Kamati iliwashauri juu ya maboresho makubwa. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi kubwa ambazo anazifanya za kuboresha miundombinu ambayo ipo na inaendelea kufanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja na ninalishawishi Bunge ku-*support* Kamati ya Miundombinu, ahsante.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa taarifa nzuri. Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati na Mwaka 2024 na yapitishwe kama Maazimio ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati ya Mwaka 2024 yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni. sasa hili ni azimio rasmi ambalo Serikali watakabidhiwa waende wakafanyie kazi maoni ya Kamati pamoja na Bunge Zima.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Nishati na Madini. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia hoja hii kwa kuzungumza. Ninaamini pia kutokana na ufinyu wa muda, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba michango yote tunaithamini na ninaamini kwamba Serikali imeisikia na itayafanyia kazi Maazimio ya Bunge kutokana na hoja ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa wachangiaji nane wamechangia hoja ya Kamati kwa njia ya kuzungumza. Katika michango yao maeneo ambayo yamegusiwa ni haya yafuatayo: matumizi ya nishati safi ya kupikia hasa ugawaji wa mitungi ya gesi; mradi wa umeme wa bwawa la Julius Nyerere; nishati safi ya kupikia, yaani kuwe na matumizi mazuri ya mitungi ya gesi; gharama ya kujaza gesi iwe nafuu; pia vituo vya kujaza gesi visogezwe karibu na watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gridi ya Taifa, mikoa ambayo haijaunganishwa na gridi ya Taifa iunganishwe. Elimu zaidi iendelee kutolewa kuhusu matumizi bora ya mitungi ya bei ya ruzuku, na miundombinu ya usafirishaji wa umeme iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazungumzia Gridi Imara. Fedha za mradi wa Gridi Imara kutoka nje ya nchi hazipatikani kwa wakati na kwa uhakika. *REA* iongeze ukubwa wa mashine ili kuhimili mzigo wa matumizi. Mradi wa umeme wa *REA* katika vijiji na vitongoji fedha zitolewe na utekelezaji ufanyike kwa kazi inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya madini Waheshimiwa Wabunge wameshauri kwamba bajeti ya *GST* iongezwe ili kuweza kuendelea kufanya utafiti ambao unatakiwa. Upimaji wa *high resolution geophysical survey* ufanyike ili kuongeza eneo la nchi lililopimwa kutoka 16% ili watu wachimbe kwenye maeneo yenye uhakika wa mashapu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wachimbaji wadogo waendelee kuwezeshwa mitaji na upimaji ili wachimbe maeneo yenye uhakika. Yaani maana yake ni kwamba kabla mtu hajapewa leseni, basi apewe eneo ambalo limeshafanyiwa utafiti wa awali ili wasizamishe mitaji yao, fedha zao chache walizonazo wasije wakazizamisha maeneo ambayo hawana uhakika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa uhifadhi ya ununuzi wa dhahabu kwa *BoT* uendelee na uendelezwe na usimamiwe kikamilifu ili nchi iweze kuhifadhi dhahabu ya kutosha. Wananchi wanaopisha maeneo yao ili uchimbaji uendelee wafikiriwe, hasa katika masuala ya hisa, mitambo ya uchorongaji iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kuna mitambo inaagizwa na *STAMICO,* wameshaleta mitano lakini wameagiza mingine kumi. Hata hivyo, bado tunaamini kabisa hii mitambo haitoshi na hivyo inabidi iongezwe zaidi ili wachimbaji wadogo waweze kupata msaada wa kufanya utafiti maeneo kadhaa ambayo yanaweza kuwasaidia kuendeleza uchimbaji wao wa madini, hasa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunathamini michango ya Waheshimiwa iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja hii. Ni imani yangu kwamba Serikali itazingatia michango yote na kuifanyia kazi ili kuendelea kuboresha utendaji na

kuendelea kuboresha maisha ya Watanzania kupitia sekta hizi mbili za nishati na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, na pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya mambo mengi ambayo yamerahisisha hata uchangiaji wa ripoti yetu hii kuwa ni rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, na kwa kuwa mambo mengi yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, yapo kwenye ripoti yetu ya Kamati, naomba kutoa hoja.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati za mwaka 2024 yapitishwe kama maazimio ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati ya mwaka 2024 yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki na sasa hii ni taarifa rasmi na Azimio la Bunge kwa Serikali kwa upande wa Kamati hii. Nawashukuru sana Wenyeviti hawa wawili na Kamati zenu kwa kazi nzuri mlizofanya.

Mheshimiwa Kakoso wewe unaonekana bingwa kwenye Kamati hii na utaendelea kuwa huko kwa sababu tumekuamini. Mheshimiwa Mathayo nawe ni bingwa wa siku nyingi sana kwenye Kamati hii, pamoja na Wabunge ambao mnawasaidia Wenyeviti wenu kufanya kazi nzuri sana kwa kushirikiana na kufanya kazi na Serikali. *This is how it works, united we stand.*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye atakuwa nje ya Mkoa wa Dodoma kwa shughuli maalum za kikazi na nafasi yake amemkaimisha Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu. Anasema, "Hapa wakati sipo utakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi hapo nitakaporejea." Atakaporejea unamrudishia nafasi yake. *(Kicheko)*

Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.47 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 4 Februari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*